**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 28 Mei, 2020**

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 356

**Hitaji la Walimu wa Sayansi – Mafinga Mjini**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Serikali ilipopanga walimu wa sayansi na hesabu katika Halmashauri za Miji, Halmashauri ya Mafinga Mjini haikupata mwalimu hata mmoja.

Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa sayansi na hesabu Mafinga Mjini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2015/ 2016 hadi Februari, 2020 Serikali imeajiri watumishi 7,218 wa shule za sekondari wakiwemo walimu 6,921 na mafundi sanifu wa maabara 297ambapo Halmashauri ya Mji Mafinga imepatiwa walimu 25. Serikali itaendelea kuajiri na kuwapanga walimu wa sayansi na mafundi sanifu maabara kadri ya upatikanaji wa fedha.

Na. 357

**Ukosefu wa Dawa kwa Wanachama wa Bima ya Afya –Biharamulo**

**MHE. OSCAR R. MUKASA** aliuliza:-

Wananchi wa Wilaya ya Biharamulo wanahamasishwa na wana mwitikio mkubwa wa kujiunga na bima ya afya lakini wanakatishwa tamaa na usugu wa hali ya kukosekana kwa dawa wanapokwenda kupata huduma za matibabu.

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya suala hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wagonjwa wa bima ya afya *(NHIF)* katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamuro wanatibiwa kwenye Hospitali Teule ya Biharamulo ambapo upatikanaji wa dawa ni zaidi ya asilimia 95. Aidha, hospitali imetenga sehemu maalumu kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wa bima ya afya *(NHIF).* Hospitali pia ina duka la dawa kwa ajili ya

kusaidia wagonjwa kupata huduma kwa karibu kwa dawa ambazo zinakuwa hazipatikani hospitali kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, aina nyingine ya bima inayotoa huduma kwa wananchi ni Mfuko wa Afya ya Jamii *(CHF)* ambayo wananchi ambao hawapo kwenye ajira rasmi wanahamasishwa kujiunga. Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo inahudumia wananchi waliojiunga na mfuko huu kupitia Vituo vya Afya vitano na Zahanati 18 na upatikanaji wa dawa kwenye vituo vya afya na zahanati hizo ni asilimia 95.

Na. 358

**Wakazi wa Liwale Kutonufaika na Uwepo wa Hifadhi ya Selous**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Liwale ni miongoni mwa Wilaya zinazopakana na Hifadhi ya Selous lakini hadi leo hakuna uwekezaji wowote uliofanywa ili wakazi wa Liwale nao waone matunda ya kupakana na Hifadhi hiyo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na hoteli ili kukuza ajira kwa wakazi wa Wilaya ya Liwale?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale**,** kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba Selous ni mojawapo ya mapori ya akiba nchini yanayosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania *(TAWA).* Pori hili lina ukubwa wa kilometa za mraba 18,000. Ili kurahisisha usimamizi wake, pori hili limegawanywa katika kanda tatu ambazo ni kanda ya Kingupira iliyopo Wilaya ya Rufiji, Kanda ya

Miguruwe iliyopo Wilaya ya Kilwa na Kanda ya Liwale iliyopo Wilaya ya Liwale.

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba Selous katika Kanda ya Liwale linapakana na vijiji vinne vya Barikiwa, Chimbuko, Kikulyungu na Kimambi vya Wilaya ya Liwale. Kupitia shughuli za uwindaji wa kitalii zinazofanyika katika Pori la Akiba la Selous, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale imeweza kupata jumla ya shilingi 476,086,331kwa kipindi cha mwaka 2008/2009 hadi 2017/2018 ikiwa ni asilimia 25 ya ada ya wanyamapori waliowindwa katika vitalu. Fedha hizo hutumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ndani ya Wilaya kulingana na vipaumbele vya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, aidha, Pori la Akiba Selous kwa kushirikiana wadau wengine hasa kampuni zinazofanya shughuli za uwindaji katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020 iliweza kusaidia miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya ya Liwale yenye thamani ya shilingi 151,875,000.

Na. 359

## Barabara ya Kutoka Muheza Mjini Hadi Amani

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA** aliuliza:-

Zipo ahadi mbalimbali za ujenzi wa barabara ya kutoka Muheza Mjini kwenda Amani kwa kiwango cha lami zaidi ya kilometa kumi.

(a) Je, ni fedha kiasi gani mpaka sasa zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo?

(b) Je, ni lini wananchi wa Tarafa ya Amani wategemee kupata usafiri wa uhakika kupitia barabara hiyo itakayokamilika?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba, Mbunge Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Muheza – Amani yenye urefu wa kilometa 40 ni barabara ya mkoa na inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANRAODS)* Mkoa wa Tanga ambapo kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ilikamilika tarehe 5 Februari, 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) ilitenga shilingi milioni 1,450 katika mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa saba za barabara hiyo. Hadi sasa mkandarasi wa ujenzi amepatikana na amesaini mkataba wa ujenzi tarehe 23 Oktoba, 2019 ambapo ujenzi umepangwa kuchukua miezi tisa. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 mradi huu umetengewa shilingi milioni 1,590 ili kuendelea na ujenzi.

Na. 360

**Nafasi ya Kilimo Kufanikisha Sera ya Uchumi wa Viwanda**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Nchi yetu inatekeleza sera mbalimbali ili kuwa na uchumi wa viwanda.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula, matunda na viungo katika kufanikisha sera ya viwanda?

(b) Je, kuna wawekezaji wangapi wa mazao ya vyakula ambao wamejitokeza kuwekeza katika sekta ya kilimo tangu kuanza kwa utekelezaji wa mpango wa Tanzania kuwa na uchumi wa viwanda?

(c) Je, Serikali imechukua hatua gani katika kuwaondoa wananchi katika kilimo cha asili na kuwaingiza katika kilimo cha kisasa?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Jimbo la Chumbuni lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo ili kufanikisha sera ya viwanda nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha mfumo wa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo kwa kushirikisha sekta ya umma na sekta binafsi; kuendelea kutathmini mahitaji na uwezo wa viwanda na kuviunganisha na wazalishaji wa mazao hayo; kusajili wakulima na wadau wa mazao hayo kwa ajili ya kuratibu uwekezaji na upatikanaji wa huduma na taarifa; kuendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA; kuimarisha majadiliano na taasisi za fedha ili kuongeza ugharamiaji katika mnyororo wa thamani wa mazao hayo na kuendelea na majadajiliano kati ya Serikali na kampuni za bima ili kutekeleza bima ya mazao katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2015/2016 hadi 2019/2020 jumla ya wawekezaji 109 wamewekeza katika uzalishaji na viwanda vipya vya kuchakata mazao ya kilimo ikiwemo mazao ya chakula na kuongeza ajira kutoka wastani wa watu 3,880,262 hadi kufikia wastani wa watu 5,204,607.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati ya kuboresha kilimo nchini ili kuwaondoa wakulima katika kilimo cha asili na kulima kwa mfumo wa kisasa. Mikakati hiyo ni pamoja na kufanya utafiti wa teknolojia za zana za kilimo katika kulima, kupanda, kuvuna na kusindika na kuhamasisha matumizi ya matrekta badala ya jembe la mkono ambapo matrekta makubwa na matrekta ya kukokotwa na mkono

yameongezeka kutoka 14,200 na 6,348 mwaka 2015 hadi 18,088 na 8,883 mwaka 2019 mtawalia.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ni kufanya utafiti wa magonjwa na visumbufu vya mimea vinavyoathiri mazao ili kuongeza tija, ubora na uzalishaji wa mazao nchini ambapo kutoka mwaka 2015/2016 hadi 2019/2020, *TARI* imegundua aina 124 za mbegu bora.

Aidha, makampuni binafsi yamegundua aina 35 za mbegu bora za mazao ya kilimo. Jitihada nyingine ni kuongeza matumizi ya mbegu kutoka tani 10,946 za hadi 76,725.52 na mbolea kutoka tani 302,482 mwaka 2015/2016 hadi tani 604,978 mwaka 2019/2020.

Na. 361

## Kudhibiti Uingizaji wa Mbolea Nchini

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Moja ya sababu ya kushuka kwa uzalishaji wa baadhi ya mazao nchini ni kutokana na uingizaji wa mbolea nchini kutoka nchi zisizokuwa na viwango bora.

Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti uingizaji wa mbolea zisizo na viwango bora nchini?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzalishaji wa ndani kutokutosheleza mahitaji ya nchi, Serikali huratibu na kusimamia uagizaji wa mbolea kutoka nje ya nchi ili kukidhi mahitaji. Baadhi ya nchi wazalishaji wa mbolea ni Morocco, Saudi Arabia, Ukraine, China, Italia, Ubelgiji, Madagascar na Norway.

Mheshimiwa Spika, uingizaji wa mbolea nchini hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Mbolea Na. 9 ya mwaka 2009 ambayo imeweka utaratibu wa mifumo miwili ya uagizaji wa mbolea kutoka nje ya nchi. Mifumo hiyo ni Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja *(Fertilizer Bulk Procurement System)* na uingizaji kupitia kampuni binafsi za mbolea ambazo huagiza moja kwa moja kutoka nchi wazalishaji wa mbolea.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea *(TFRA)* hutoa vibali vya kuingiza mbolea nchini na hufanya ukaguzi ili kuhakikisha ubora wa mbolea kabla ya kuruhusu kusambazwa kwa wakulima kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS),* Tume ya Mionzi *(TAEC)* na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali *(GCLA).*

Aidha, *TFRA* hufanya ukaguzi mara kwa mara kwenye maghala na maduka ya wauzaji wa mbolea kwa lengo la kuhakikisha kuwa mbolea zinazouzwa na kusambazwa kwa wakulima zina ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa mbolea kutoka Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa ili kuimarisha udhibiti wa ubora wa mbolea zinazoingizwa na kusambazwa kwa wakulima. Mwaka 2019/2020 jumla ya wakaguzi 150 wamepatiwa mafunzo ya ukaguzi wa mbolea na mawakala 1,446 wamepatiwa mafunzo ya utunzaji, usambazaji na uuzaji wa mbolea kutoka katika Halmashauri na Mikoa mbalimbali hapa nchini.

Aidha, katika mwaka 2019/2020 Wizara imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya mbolea ili kuongeza na kuimarisha udhibiti wa ubora wa mbolea zinazozalishwa, kuingizwa, kusambazwa na kutumika hapa nchini. Vilevile Serikali itaendelea kudhibiti uingizaji wa mbolea kupitia njia zisizo halali ili kuhakikisha kuwa mbolea yote inayoingizwa nchini ina viwango vya ubora vinavyotakiwa.

Na. 362

**Ukosefu wa Mikopo kwa Wanafunzi wa Vyuo Vya Ufundi Stadi**

**MHE. ZUBEDA H. SAKURU** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaojiunga na Vyuo vya Ufundi Stadi *(VETA)*, lakini wanafunzi waliojiunga na vyuo hivyo hawapati mikopo kutoka Serikali.

Je, Serikali itaanza lini kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaojiunga na Vyuo vya Ufundi Stadi?

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mikopo ya elimu ya juu inayotolewa na Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inaongozwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo (Sura 178) ambayo inawabainisha walengwa kuwa ni Watanzania wahitaji walioomba mkopo na wenye sifa za kujiunga na taasisi za elimu ya juu na sio vyuo vya ufundi stadi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutambua kuwepo kwa umuhimu mkubwa wa mafunzo ya ufundi stadi kama kipaumbele chetu cha kujenga uchumi wa viwanda. Hivyo Serikali imeendelea kubeba gharama nyingi za Vyuo vya Ufundi Stadi vya Serikali ambavyo havilengwi na sheria hiyo ili ada zao ziwe nafuu na Watanzania wa kawaida waweze kumudu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inaendelea kupanua upatikanaji wa fursa hizi za masomo hayo ya ufundi stadi kwa kujenga vyuo vipya hasa maeneo ya vijijini ambayo yalikuwa hayana vyuo hivi. Kwa sasa utaratibu utaendelea

kuwa huo huo wa Serikali kuvipa vyuo hivyo vya ufundi stadi ruzuku ili kumpunguzia mwananchi wa kawaida gharama za kusoma. Hata hivyo, maoni ya Mheshimiwa Zubeda Sukuru na wadau wengine yanaendelea kupokelewa ili kuboresha utaratibu wa sasa kwa kadri uchumi wetu unavyoendelea kuimarika.

Na. 363

**Kutatua Tatizo la Maji Vijiji vya Mkoa wa Iringa**

**MHE. ZAINAB N. MWAMWINDI** aliuliza:-

Tatizo la maji safi na salama bado ni kubwa licha jitihada zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Je, ni lini Serikali itatatua tatizo hilo katika vijiji vya Kipera, Wangi Juu, Ilangi na Unywangila Mkoani Iringa?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Nuhu Mwamwindi, Mbunge wa Viti Maalum - Iringa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kipera ni miongoni mwa vijiji sita vinavyounda Kata ya Nzihi iliyopo Wilayani Iringa. Kijiji hiki chenye idadi ya watu zaidi ya 2,462 kinaundwa na vitongoji kumi ambapo watu waishio katika kijiji hicho wanapata huduma ya maji kupitia Mradi wa Maji Magubike unaohudumia vijiji vyote sita vya Kata ya Nzihi.

Mheshimiwa Spika, Kitongoji cha Wangu Juu kipo katika Kijiji cha Kalenga chenye jumla ya watu zaidi ya 2,418 na Vitongoji vya Ilangi na Unywangila vipo katika Kijiji cha Tosamaganga chenye jumla ya watu zaidi ya 3,511. Huduma ya maji katika vijiji hivi inapatikana kupitia Mradi wa Pamoja na Tanangozi –Kalenga. Mradi huu ulijengwa na wadau wa maendeleo *(DANIDA)* mwaka 1980. Changamoto kubwa iliyopo katika mradi huu ni kushindwa kutoa huduma kwa

watu wote waishio katika vijiji hivi kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na uchakavu wa miundombinu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua changamoto hiyo, Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo *WARIDI/ USAID* inafanya uboreshaji wa huduma ya maji katika vijiji hivyo kwa kufanya upanuzi wa mtandao wa kusambaza maji wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Iringa *(IRUWASA).* Uboreshaji huo upo kwenye hatua za mwisho kukamilika.

Na. 364

## Asilimia 10 ya Kodi ya Pango Hulipwa na Wapangaji

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

Asilimia 10 ya Kodi ya Pango inapaswa kulipwa na mwenye nyumba za biashara lakini kwa sasa hulipwa na wapangaji.

Je, ni lini utaratibu huo utabadilika?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, Mbunge wa Babati Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 86(1)(c) cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332, kinamtaka mmiliki wa nyumba ya biashara mwenye mapato yanayozidi shilingi 500,000 kulipa Kodi ya Zuio *(Withholding Tax)* kutokana na mapato yanayotokana na upangishaji wa pango *(rental tax)* kwa kiwango cha asimilia 10 ya mapato ya kodi ya pango husika.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha ukusanyaji wa kodi hii, Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 inaruhusu mpangaji anayeendesha biashara katika nyumba husika na kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato kuwa Wakala wa Ukusanyaji wa Kodi

hiyo *(Withholding Tax Agent).* Kwa kuwa kodi hii siyo ya mpangaji, kiasi cha kodi ya pango ambacho kimelipwa na mpangaji huhesabiwa kama sehemu ya fedha ambazo anapaswa kurejeshewa na mwenye nyumba.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu umewekwa ili kurahisisha ukusanyaji wa kodi hii ya pango kwani inarahisisha kwenye ukusanyaji wa kodi hasa pale ambapo mpangishaji hajasajiliwa na Mamlaka ya Mapato kama mlipakodi. Hata hivyo, Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332, kifungu cha 82(2)(a) mpangaji ambaye sio mfanyabiashara na hajasajiliwa na TRA kama mlipakodi hapaswi kukusanya kodi hii.

Na. 365

**Vyakula Vinavyosindikwa Viwandani**

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI** aliuliza:-

Usalama wa vyakula vinavyosindikwa viwandani ni muhimu kwa kulinda afya za wananchi pale vinapotayarishwa kwenye viwanda hivyo.

(a) Je, kuna vigezo gani vya kulinda vyakula hivyo vinavyozalishwa kwenye maeneo hayo?

(b) Je, ni hatua gani zimekuwa zikichukuliwa dhidi ya wazalishaji wa viwango dhaifu vya vyakula?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* linavyo vigezo mbalimbali vya kudhibiti ubora na usalama wa chakula katika viwanda vya usindikaji vyakula vya ndani na nje ya nchi. Vigezo hivyo vimejengwa kwa

mujibu wa Sheria ya Viwango ya mwaka 2009 pamoja na kanuni zake. Pia vigezo hufuata miongozo ya kimataifa ya Shirika la Viwango Duniani na Shirika la Viwango vya Usalama wa Chakula Duniani.

Mheshimiwa Spika, viwanda vinavyosindika vyakula nchini vinapaswa kupata ithibati ya ubora kwa vyakula wanavyozalisha. Vilevile viwanda vya ndani ya nchi, kabla ya kupata ithibati ya ubora kwa vyakula wanavyozalisha kwanza, viwanda hivyo hukaguliwa kuangalia kama wanayo mifumo bora ya uzalishaji *(Good Manufacturing Practices - GMP)* na mifumo bora ya usafi *(Good Hygienic Practices - GHP)* ambayo huhakikisha uzalishaji endelevu wa chakula salama na bora.

Pili, sampuli ya bidhaa za chakula zinazozalishwa huchukuliwa na kupimwa kwenye maabara kuangalia kama zinakidhi matakwa ya ubora na usalama yaliyoainishwa kwenye kiwango husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupata ithibati ya ubora, *TBS* hufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye viwanda vyote vya chakula nchini. Pia *TBS* inafanya ukaguzi kwenye soko kuangalia usalama wa vyakula.

Mheshimiwa Spika, kwa bidhaa zinazozalishwa nje ya nchi, bidhaa hizo hupimwa huko huko nje ya nchi kwa kutumia mawakala wanaotambuliwa na *TBS* kupitia mfumo wa *(Pre Shipment Verification of Conformity to Standards - PVoC)*. Bidhaa ambazo hufika nchini bila kupimwa *TBS* huzikagua na kuzipima.

(b) Mheshimiwa Spika, *TBS* huchukua hatua mbalimbali dhidi ya wazalishaji wanaozalisha vyakula visivyokidhi matakwa ya ubora na usalama. Hatua hizo ni kuondoa vyakula hafifu sokoni na kuviharibu, kufuta leseni ya kutumia nembo ya ubora kwa mzalishaji chakula hafifu, kurudisha bidhaa hafifu zinazotoka nje ya nchi, kuwapeleka mahakamani waingizaji na wazalishaji wa vyakula hafifu na

kuwatoza faini, kuwafunga au vyote kwa pamoja na kufifilisha kosa kwa mujibu wa sheria iwapo mkosaji atalikubali.

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa za Ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2019**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Anastazia Wambura, atafuatiwa na Mheshimiwa Martin Msuha na Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Kamati ya *LAAC* ambayo mimi pia ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kunijalia afya njema, lakini kwa kusimamia katika harakati hizi za kupambana na ugonjwa wa Corana. Niseme tu Watanzania tuna kila sababu ya kumshushukuru Mwenyenzi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuunga mkono hoja ya Kamati lakini pia kuwashauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu ili kusudi tuweze kuunga mkono mapendekezo ya Kamati yetu ya *LAAC.* Nitakayazungumza nikuongezea tu labda na kuweka ufafanuzi kidogo katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa suala moja ambao Kamati yetu imeliona, ni suala la *POS* kutotumiaka ipasavyo. Haingii akili kabisa kwamba Halmashauri 65 zote hizi zisionekane kwa muda wa zaidi ya siku 100, zisionekane kabisa. Hakuna makusanyo wala hazionekani kufanya kazi yoyote na tafisiri yake ni kwamba mapato zaidi ya kipindi cha robo mwaka katika vituo hivi 65 yanaweza kuwa yamepotea na cha kujiuliza, tumejiuliza sana Kamati kwamba hivi Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kinafanya kazi gani hadi kufukia kwamba *CAG* ndiyo agundue hili tatizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hili niongee kwenye ushauri wa kamati kwa kusema kwamba pamoja na hatua zote ambazo Serikali itachukua kwa sababu tumetoa ushauri sisi. Lakini pamoja na hatua zote Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kiwezeshwe vizuri ili kusudi kiweze kutekeleza ipasavyo wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala jingine ambalo ni tatizo la *MSD* kutofikisha mzigo wa dawa kwenye Halmashauri kulinga na fedha ambazo zimetolewa Serikalini. Halmashauri ambazo tumezihoji nyingi wameshindwa kutoa sababu ya hili tatizo. Lakini hapa tumekuwa na maswali ambayo tukijiuliza hivi ni kwamba *MSD* haina dawa za kutosha? Kwa sababu kama Serikali imetoa shilingi milioni 100, lakini unakuta Halmashauri inapokea dawa za shilingi milioni 65. Sasa tatizo nini walishindwa kutujibu, sasa tunajiuliza hakuna dawa za kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna suala ambalo limejitokeza kwamba Serikali inadaiwa fedha nyingi sana na *MSD,* sasa tunajiuliza kwamba *MSD* imeamua kufanya makato juu kwa juu ya deni lile ambalo inalolidai Serikali? Tumekosa majibu. Lakini pia kuna suala nyingine la kujiuliza, je, Serikali inaweka kumbukumbu sahihi kuhusu bakaa ya deni hili la dawa na Halmashauri zote? Kwa sababu hapa utaona kutakuwa na mkanganyika kama Serikali haiweki kumbukumbu sahihi. Lakini ushauri wangu niongeze tu kwenye ushauri wa Kamati kwamba kama taratibu zinaruhusu ni bora wakatiane deni hili ili kusudi deni la Serikali liweze kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mafanikio ya Kamati ni kwamba katika mwaka 2018/2019 hakukuwa na hoja inayohusu ile asilimia kumi ya ile ya mikopo wanawake, vijana na watu wenye ulemavu haya ni mafanikio makubwa na hii hakuwa hoja kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nitoe angalizo kwamba sasa Halmashauri zetu zisibweteke tuendelee kufanya kazi ya kuangali kama kuna tija kweli hii mikopo na ninasema hivi kwa sababu ukiangalia marejesho hayaridhishi, marejesho ya mikopo hayaridhishi. Kwa hiyo kuna swali hapa je, hii mikopo inayotolewa ina tija? Sasa mimi nipendekeze *CAG* ajipange kufanya *performance audit* ili kusudi hii mikopo iwe na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la watu wenye ulemavu ambapo mimi nipendekeze kanuni ziangaliwe upya hili suala, kwa sababu walemavu wapo katika maeneo tofauti na kanuni zinataka wakopeshwe watu kwenye vikundi inakuwa ngumu kuwapata walemavu wa aina moja katika sehemu moja na kwa kweli mimi nadhani itakuwa muhimu sana watu wenye ulemavu wakapewa *special consideration* ili kusudi mikopo hii iweze kuwa na tija kwa hawa watu. *(Makofi)*

Lakini pia ingaliwe kama kuna uwezekana basi angalau baadhi ya watu wenye ulewamvu wape *grand* balada ya kupata mkopo kwa sababu si wote ambao wanaweza wakafanya kazi vizuri na kurudisha mkopo. Sana sana tutakuwa tutakuwa tunawasidia kujikimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache nimalizie kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, pamoja na Wanakamati kwa kazi nzuri walioifanya mpaka tukaja na hii ripoti na wachangaji wote ambao wamechangia vizuri. Lakini zaidi sana nimpongeze Mheshimiwa Rais, nimpongeze Mheshimiwa Spika kwa jinsi ambavyo wamesimimia vizuri suala la kudhibiti ugonjwa wa Corona. Kwa kweli utuvulivu na ujasiri wa viongozi wetu hawa unaonesha dalili kwamba watafanya miujiza. Nchi yetu

itakuwa imefanya miujiza katika kupamba na janga hili la Corona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba wamekuwa ni kama mfano wa yule rubani wa Marekani ambaye anaitwa Sullenberger ambaye utulivu na ujasiri ulimwezesha kuwaokoa abiria kwa kutua katika Mto Hudson ambapo hakuwakurupusha wale abiria. Lakini aliweza kuwaokoa abiria wote 155 na ilipotokea ajali yeye alikuwa akiwaambia *bless, bless, bless heart,* abiria walitulia na matokeo yake walitoka wote salama, waliolazwa wakiwa mahututi ni abiria wawili na wote walipona kiasi kwamba tukio hili waliita *the miracle of the Hudson*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi niseme Mheshimiwa Rais alivyotuondoa hofu, hakuweka *lockdown,* akaturuhusu kufanya ibada, akatuambia tumuombe Mungu, kwa kweli muujiza unaonekana ni kwamba nchi nyingi zimefuata nyayo zake sasa, ni juzi tu Marekani wametoa amri za kufungua Makanisa, Misikiti, Masinagogi na nchi nyingi sasa hivi zimefungulia *lockdown*.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba jana nimesikia madaktari wetu wanakiri kwamba ugonjwa wa Corona umepungua na wanasema mwezi wa nne na tano. Wiki ya kwanza ya mwezi wa tano ilikuwa ni wiki ngumu sana hizi wiki mbili zilikuwa ni wiki ngumu sana kwao. Lakini sasa hivi wanasema wagonjwa wa corona wamepungua *cases* zimepunuga na kwa hiyo mimi niseme tunakila sababu ya kumshukuru Rais na Mwenyenzi Mungu na hii inadhihirisha wazi kwamba wamtumainio Mungu hawatatikisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafikiri tutaendelea kupata miujiza zaidi kwa sababu muujiza mmojawapo tuliupata 25 Aprili, 2019 kimbunga kilitupita kimiujiza, watu dunia nzima walikuwa wanatuonea huruma, wakawa wanatuombea lakini tukaokoa na mwaka huu ni mwezi huu wa nne. Lakini naamini kabisa huu utakuja kuandikwa zaidi kama muujiza katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo nikushukuru sana kwa jinsi ambavyo unamsaidia Spika wetu kwa sababu najua mpo bega kwa bega kwa maamuzi yote haya yanayofanyika kiasi kwamba sasa hivi tunaendesha Bunge letu kwa amani na kipindi cha Bajeti kinaisha na mambo yanaenda vizuri. Kwa hiyo, mimi niseme Mwenyenzi Mungu awabiriki sana, abariki uongozi wote wa Bunge, ambariki Mheshimiwa Rais, awabariki Waheshmiwa Mawaziri wetu, Serikali na kwa kumalizia nimpongeze Mheshimiwa Mollel kwa kushika nafasi hii mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme ahsante sana, niwatakieni kheri Waheshimiwa Wabunge, niwatakieni afya njema, nashukuru sana Mungu aibariki nchi yetu, Mungu alibariki Bunge letu, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja, leo sina kishikwambi samahani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Martin Msuha atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Aisharose Matembe ajiandae.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi kupatiwa nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mezani. Kabla ya yote na mimi pia niweze kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kuendelea kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele Bunge lako tukufu leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa naomba nimshukuru Mheshimiwa Spika, pamoja na wewe pamoja na ofisi yako yote kwa kuniteua kuwa mjumbe wa Kamati ya *LAAC* kwa kipindi chote cha miaka mitano, nimepata uzoefu mkubwa sana kutoka kwenye Kamati hii. Uzoefu niliupata umeniongezea tija ukizingatia fani yangu pia ni ya uhasibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hili niungane na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Elias Kwandikwa katika kutumikia Kamati hii tumejengewa uwezo mkubwa

sana wa kitaaluma na Ofisi ya Bunge, lakini pia Ofisi ya *CAG.* Kwa taratibu ya sisi wahasibu tuliosajiliwa tunahitaji kuingiza masaa *CPD hours* inaitwa. Sasa niiombe Wizara kupitia *NBAA* iangalie wahasibu ambao wapo katika kwenye kamati hii yale mafunzo ambayo yanakuwa wamejengewa uwezo kupitia Ofisi ya Bunge na Ofisi ya *CAG* yangeingizwa kwenye mfumo kwenye masaa yale ambayo yanatakiwa kuhesabika kule kwenye bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo maneno ya utangulizi, nianzie kwa kusema kwamba hoja ambazo zimeibuliwa katika Taarifa za *CAG* kwa mfululizo wa miaka yote mitano zimekuwa zikijirudia rudia. Baadhi ya hoja hizo ni kama ifuatavyo; baadhi ya malipo kufanyika bila kupata vibali vya Maafisa Masuuli, lakini upungufu wa watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa imekuwa ya kudumu katika Taarifa ya *CAG,* matumizi yasiyo sahihi ya mashine ya kukusanyia mapato kwa maana ya *POS* yamesemwa sana na Wajumbe wote waliotangulia, lakini kuna malipo mengine ambayo yamefanyika bila kuwa na viambatanisho husika *(unsupported payments),* lakini jambo lingine ambalo limekuwa likijirudia rudua ni makusanyo ya ndani kutokupelewa benki kwa wakati jambo ambalo linachochea wizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hizo zimekuwa zikisababishwa na mambo yafuatayo; jambo la kwanza, kutozingatia kanuni na miongozo ya fedha na sheria na kanunu za manunuzi jambo ambalo linawapelekea Watendaji wetu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya kazi kwa mazoea. Lakini sababu nyingine ambayo inapelekea hoja hizo kujirudiarudia ni utunzaji mbaya wa nyaraka mbalimbali zikiwemo nyaraka za malipo jambo ambalo linapelekea nyaraka hizo kupotea na hatimaye wakati ukaguzi unafanyika nyaraka hizo haziwezi kuwasilishwa kwa wakaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni uwezo mdogo baadhi wa watendaji wetu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Lakini jambo lingine linalosababisha hoja hizo ni

Halmashauri zetu kutokuitwa kwa muda mrefu kwa Kamati ya *LAAC* kwa hiyo kuwafanya wajisahau.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ili kuzuia mambo hayo ni kama ifuatavyo; jambo la kwanza Kitengo cha Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha za Mikoa na Mamlaka za Halmashauri za Serikali za Mitaa kiimarishwe ili kukiwezesha kitengo hiki ili kuzifikia Halmashauri zote kwa mwaka. Lakini pia Serikali ingalie namna ya kufanya mafunzo ya mara kwa mara kwa watendaji wetu wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine utolewa waraka utakaowataka Watendaji wa Mamlaka Serikali za Mitaa kwa maana ywa wakurugenzi na Wakuu wa Idara ushiriki zoezi la ukaguzi kwani hoja zingine zinapelekewa kuandikwa kwenye taarifa ya mwisho kwa vile wakaguzi hawa hawapati ushirikiano wakiwa *site* na hatimaye hoja zingine ambazo zingeweze kupatiwa majibu kipingi cha ukaguzi unaendelea kukosa kupewa ufafanuzi na hivyo wakaguzi wanalazimika kuzipeleka kwenye *management letter*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize mchango wangu kwa kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wenye mapenzi mema na nchi, kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa na ya kutukuka ambayo anaendelea kuifanya. Mambo mengi yamefanyika, mambo mengi yametekelewa na Serikali ya Awamu ya Tano, mambo mengi yamesemwa na waliotangulia sitahitaji kuyarudia, mambo hayo yanonekana kwa macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda kwa namna ya pekee kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mbinga Vijijini kwa kunipa ridhaa ya kuwawakilisha kama Mheshimiwa Mbunge wao na kwa ushirikiano ambao wameendelea kunipatia hadi sasa hivi. *(Makofi)*

Lakini mwisho kabisa sio kwa umuhimu niwashukuru wananchi wa Mtaa wa Msingwa uliopo Kata ya Msigani,

Ubungo kwani wao ndiyo walinitengenezea njia ya kwenda Mbinga baada ya kunipa nfasi ya kuwawakilisha kama Mwenyekiti wao wa Serikali wa mtaa wa kwanza mwaka, 2014. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa sababu wao wameendelea pia kunilea na mimi kama mkazi pia wa eneo hilo nitaendelea kushirikiana nao kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ritta Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Aisharose Matembe na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ajiandae.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja ya *CAG.* Nianze kwa kukupongeza wewe mwenyewe Naibu Spika kwa kazi zako nzuri za ndani hapa na nje ya Bunge letu, hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani huwezi kuacha kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambazo amezifanya. Kwa kweli Mheshimiwa Rais tunampongeza sana sana sana kwa sababu Halmashauri zetu hapo zamani hazikuwa kama hivi zilivyo, fedha zinaletwa katika Halmashauri zetu, lakini tunaona kwamba miradi haionekani. Walikuwa wanaita kwamba Halmashauri kama mchwa, fedha zinaingia lakini hatuoni kinachoonekana. Kwa hiyo kwa kweli lazima tumpongeze sana sana Mheshimiwa Rais wa Awamu hii ya Tano na watendaji wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimtendee haki *CAG* wetu Ndugu Kichere, amefanya kazi kubwa sana, nzuri sana na kwa kweli ukiwauliza hata wa Wajumbe wa Kamati ushirikiano wake mzuri umewafanya hata wao wakafanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo, niwapongeze hata Wajumbe wa Kamati hii ya *LAAC* kwa kuonesha ushirikiano na *CAG.(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ripoti ya *CAG* inaonesha kwamba sasa hivi katika Halmashauri zetu hawa Maafisa Masuuli pia wanafanya kazi nzuri baadhi ya Halmashauri. Unaona kwamba pia hata vitendo vya rushwa vimepungua katika Halmashauri, kwa hiyo mimi niendelee tu kupongeza kazi nzuri inayofanywa ukitofautisha na pale zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie yafuatayo; najua wengi wamechangia lakini na mimi niunge mkono yale waliyochangia nichangie ya kwangu.

La kwanza ni ucheleweshaji wa fedha za ruzuku za maendeleo katika Halmashauri zetu. Kucheleweshwa kwa fedha hizi kumefanya miradi mingi katika Halmashauri kutokukamilika kwa wakati, vilevile gharama ya miradi inakuwa kubwa. Kwa hiyo, tu niombe Serikali iweze kutoa fedha kwa haraka ili miradi iweze kukamilika kwa wakati ili pia gharama tunazozitumia ziwe kiasi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukulia tu mfano katika Halmashauri yetu ya Iringa iko baadhi ya miradi kwa mfano Mradi wa Machinjio ulianza toka mwaka 2008, zaidi ya miaka 10. Unaona kama huu mradi ungekuwa ulitetewa fedha mapema leo hii huu mradi ungeweza kusaidia hata maendeleo katika Halmashauri yetu ya Manispaa ya Iringa. Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka fedha mapema katika Halmashauri ili miradi iweze kukamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nielezee pia kuhusu Mfuko wa Maendeleo kwa ajili ya mikopo ya wanawake zile asilimia nne ya wanawake, asilimia nne vijana na asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu. Kwa kweli nafikiri hii ni sheria kabisa tumepitisha hapa Bungeni hawa wanawake, vijana na walemavu waweze kupatiwa hizi fedha. Lakini utaona kwamba kuna baadhi ya Halmashauri ambazo bado hazitendi haki, kwamba zile asilimia 10 ya mapato ya ndani bado hazitengi na tumeona kuna hoja kabisa ya *CAG. (Makofi)*

Sasa mimi niombe kama tumependa kisheria, je, hatua gani zinachukuliwa kwa Halmashauri ambazo hazitengi hizi fedha kwa ajili ya kuwapatia wanawake, vijana na watu wenye ulemavu? Kwa sababu hii ni sheria na ninaamini kwamba hizi fedha zinasaidia sana kwa ajili ya mikopo hii ya wanawake na tunaona kwamba Serikali yetu ina nzuri kabisa kwamba hizi fedha badala ya wanawake kudhalilishwa, japokuwa wanawake wengi wanadhalilishwa, lakini toka fedha hizi zimetoka tunaona wanawake wengi wameweza kufanya biashara ndogo ndogo.

Kwa hiyo, mimi niiombe kabisa Serikali iangalie uwezekano wa kuwachukulia hatua zile Halmashauri ambazo hazifuati hii sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikija pia kwenye ucheleweshaji wa malipo ya wastaafu, kwa kweli hili jambo Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamelichangia na inaumiza sana kuona mstaafu anastaafu, akishastaafu fedha yake haipati kwa wakati. Kuna walimu, kuna wauguzi na watu wengi sana wamekuwa wakistaafu lakini fedha yao hawapati kwa wakati. Inaumiza sana kwa sababu unamkuta mstaafu kila siku anakwenda kufuatilia fedha yake ya malipo ya uzeeni, lakini majibu atakayopewa kwanza pale yanaweza yakamfanya akachanganyikiwa. Atakuambia labda fedha bado au ataambiwa majina yako labda..., yaani siyo mazuri yaana majibu wanayowapatia yanakuwa kama vile tu wanawapa moyo wa kwamba wasubiri lakini siyo kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo unakuta kwa mfano Iringa, mimi nilikuwa naongea na Mwenyekiti wetu wa Walimu Ndugu Mwongole. Anasema kwamba kuna baadhi ya walimu toka mwaka 2017 hata zile posho tu, fedha zile kwa ajili ya kusafirishia mizigo hawajapatiwa. Sasa hawa wastaafu wanategemea hizi fedha zao warudi nyumbani kwao, wengine siyo wanapofanyia kazi wanataka kurudi kwenye majumba yao, kwenye mikoa yao kwenda kustaafu yaani wakapumzike pale waweze kufanya biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe Serikali kwa kweli hili iliangalie na ikiwezekana kwanini sasa Serikali, nafikiri tuna *database* ya wastaafu kwamba mwaka kesho tuna wastaafu fulani watastaafu. Kwa nini wasiwe wanaweka kabisa, wanaanda kabisa zile posho zao au wakati wakipewa barua wapatiwe kabisa na *cheque* yao ili wakiondoka kusiwe na usumbufu ambao wamekuwa wakiupata kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna jambo lingine, urakishaji wa uteuzi wa uthibitisho wa Wakuu wa Idara. Wakuu wengi wa Idara wamekuwa wakikaimu hizi nafasi kwa muda mrefu sana. Unaweza kukuta katika Halmashauri karibu Wakuu wa Idara watatu, wanne, watano wanakaimu, tena wanakaimu zaidi ya miezi sita. Maana yake nafikiri ukikaimu miezi sita unaweza ukathibitishwa, lakini unakuta anakaimu, anakaimu, anakaimu, anakaimu, sasa inamfanya hata yule anayekaimu kutofanya vizuri kwa sababu hana uhakika na sehemu aliyonayo na anaweza akakaimu akafanya vizuri anakuja analetwa mtu mwingine. Kwa hiyo bado huyu mfanyakazi morali wake wa kazi unakuwa siyo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nielezee kuhusiana na ucheleweshaji wa posho za Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa. Kwa kweli mimi niombe hili liangaliwe. Halmashauri yangu siyo kwamba haicheleweshewi lakini kuna Halmashauri nyingi sana wanawacheleweshea Madiwani wengi unakuta mpaka sasa hivi unakuta bado posho hawajapata. Lakini vilevile hao Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wanacheleweshewa sana posho zao pia pamoja na kwamba posho yao siyo kubwa sana, lakini ni muhimu sana Wenyeviti wa Serikali za Mitaa pia wakapewa posho yao kwa wakati. Kwa sababu utakuta baadhi ya Wenyeviti wa Serikali za Mitaa bado hawana hata ofisi, wanafanya hizi kazi kwenye nyumba zao wenyewe, lakini bado mpaka sasa hivi wanacheleweshewa posho.

Mimi niombe Serikali yetu kwa kweli iangalie uwezekano wa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Waheshimiwa Madiwani tena hawana mishahara ni posho tu, posho

wapewe kwa wakati ili waendelee kutumikia Taifa lao bila kinyongo chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nielezee kuhusu urasimu wa malipo ya wakandarasi wanapofanya kazi kwenye Halmashauri. Unakuta kwamba malipo yanakwenda sehemu nyingi sana kiasi kwamba ule urasimu unafanya miradi mingi kuchelewa. Wangeangalia njia nzuri ya kufanya kwamba haya malipo, sasa hivi tuna kompyuta, tuna kila kitu, haina haja ya kuchukua muda mrefu sana kwa sababu bado mnaweza mkafanya kazi wote kwa pamoja kwamba ukatuma tu kwenye kompyuta na yule mtu akapokea na ikawezekana kabisa kwamba malipo yakatoka kwa wakati ili miradi yetu iweze kwenda kwa wakati. Kwa hiyo, mimi niombe pia Serikali iangalie hii hoja ili hawa wakandarasi wanaofanya kazi katika Halmashauri waweze kupatiwa fedha zao mapema na miradi iweze kukamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba pia niendelee kupongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Lakini pia nipongeze sana hata Waheshimiwa Mawaziri wetu wanawake, kwa kweli wametutendea haki sisi hapa, wamefanya kazi nzuri sana wote walioteuliwa wanawake Mawaziri na Naibu Mawaziri wamefanya kazi nzuri sana. Mimi niwape moyo kwamba waendelee kufanya kazi kuchapa mzigo, siyo kwamba wanaume hawajafanya vizuri, lakini wakina mama wamefanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo niwashukuru sana Wakurugenzi wa Halmashauri zote za Mkoa wa Iringa kwa kunipa *support* kubwa katika kazi zangu za Ubunge. Naomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki. Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimwa Aisharose Matembe atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso na Mheshimiwa Susan Lyimo ajiandae.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Taarifa ya Kamati ya *LAAC* kwa mwaka wa fedha inayoishia 30 Juni, 2019. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kutujalia uzima na afya njema si kwa ujanja wetu bali ni kwa ukarimu na upole wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupongeze wewe kwa kazi nzuri ulizofanya Jijini Mbeya, nina uhakika kabisa Wanambeya watakupitisha kwa kishindo itakapofika wakati wa uchaguzi, hongera sana. Nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati, Makamu wake, Wajumbe wote, Makatibu wake kwa taarifa nzuri walioiwasilisha ya Kamati ya *LAAC,* nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uhai wa kipindi cha Bunge kilichopita nilikuwa ni mjumbe wa Kamati ya *LAAC,* ninakushukuru sana wewe pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kuniteuwa katika Kamati hiyo. Lakini kwa sasa ni mjumbe wa Kamati ya *PAC,* hakika uwepo wangu katika Kamati zote hizi mbili nimepata uzoefu mkubwa sana na ninawashukuru sana, namshukuru sana Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana *CAG* na timu yake kwa kazi nzuri walioifanya ya kukaguwa Halmashauri 185 katika mwaka wa fedha 2018/2019. Kazi hii siyo nyepesi, inahitaji uwajibikaji na moyo wa kizalendo, ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya Halmashauri hizo, Halmashauri 176 zilipata hati safi na tisa zilipata hati zenye mashaka. Tafsiri yake nini, ni kwamba Halmashauri hizi zilizokaguliwa na kupata hati safi taarifa ya hesabu zake zilikuwa zimezingatia miongozo ya matumizi ya fedha. Nazipongeza sana Halmashauri hizo zilizopata hati safi na nina mpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuimarisha uwajibikaji wa kazi na matumizi ya fedha za umma, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo bado zipo changamoto za matumizi mabaya ya fedha za umma ambayo yamechangiwa aidha na Serikali Kuu au na Halmashauri zenyewe. Taarifa ya Kamati imebainisha zipo baadhi ya Halmashauri zinapokea mgao wa ruzuku ya maendeleo zaidi ya kiasi kilichotengwa na zipo Halmashauri zinazopokea pungufu ya fedha zilizotengwa na zipo pia Halmashauri zinazopokea stahiki ya fedha, lakini zinafika kwa kuchelewa. Mfano katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri 26 zilipokea kiasi cha shilingi bilioni 22.8 zikiwa zaidi ya fedha zilizotengwa katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi hiki ni sawa na 31% iliyotengwa kutumika katika Halmshauri zote nchini, unaweza kuona ni kiasi kikubwa sana cha fedha. Hapa kuna maswali mengi ya kujiuliza, ni kwa nini Halmashauri nyingine zitengewe fedha nyingi kuliko Halmashauri nyingine? Na ni kwa nini Halmashauri nyingine zinatengewa fedha pungufu ya bajeti yake?

Ninaiomba sana Serikali kuangalia suala hili, inapotenga bajeti ihakikishe kwamba Halmashauri zote zinatengewa bajeti sawa na zinapelekewa bajeti stahiki kwa namna inavyotakiwa. Ninamtaka Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuja kufanya majumuisho atuambie ni kwa nini suala hili limekuwa likijirudia mara kwa mara. Ni kwa nini Halmashauri nyingine zipewe fedha nje ya mpango wa bajeti? Jambo hili limechangia miradi mingi ya maendeleo kukwama na wananchi kutokupata huduma stahiki kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni ukiukwaji wa Sheria za Manunuzi ya Umma. Uwepo wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ilikuwa ni kuhakikisha manunuzi hayo yanakuwa na tija kwa Taifa, lakini baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikikiukwa miongozo ya sheria hii ya umma. Kupitia Kamati ya *LAAC* ilibaini manunuzi mabaya ya huduma ya bidhaa ya jumla ya shilingi bilioni 9.2 yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni. Na Halmashauri 43 zilifanya manunuzi yenye thamani ya shilingi

bilioni 5.0 na kuzitumia bidhaa hizo kabla ya kukaguliwa na kamati ya ukaguzi na upokeaji wa bidhaa hizo. Serikali imekuwa ikipata hasara kubwa hutokana na ukiukwaji wa sheria za manunuzi ya umma kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kupitia Halmashauri zetu izingatie Sheria hii ya Manunuzi ya Umma na wale ambao watakiukwa sheria hii basi sheria kali zichukuliwe dhidi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni kutokurejeshwa kwa gharama za matibabu kutoka kwa *NHIF.* Wananchi wengi katika Halmashauri zetu hupata matibabu katika vituo vya afya na zahanati. Lakini Halmashauri hutoa fedha kwa ajili ya kununua dawa hizo na vifaa tiba kutoka *MSD* na baadae wananchi hupata dawa na vifaa tiba kutumia kadi ya mfuko *CHF* uliochini ya Mfuko wa Bima ya Taifa. Lakini cha kushangaza baadhi ya Halmashauri zimekuwa hazirejeshewi gharama hizo kwa madai kwamba fomu za marejesho zimekosewa. Mfano, kwa mwaka 2018/2019 jumla ya kiasi cha shilingi milioni 2.02 hazikurejeshwa kwa baadhi ya Halmashauri kama vile Ukerewe, Rungwe, Mbarali na Kyela.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna maswali ya kujiuliza, iwapo hospitali binafsi zinalipwa marejesho hayo ni kwa nini Hospitali za Halmashauri hazilipwi marejesho hayo kwa kisingizio cha kusingizia kwamba fomu zimejazwa vibaya? Na iwapo *NHIF* inasema fomu hizo zimekosewa kujazwa, kwa nini *NHIF* wasitoe elimu ya namna ya kujaza fomu hizo? Lakini hapo hapo kiasi hicho cha fedha ambazo kinakuwa hakijalipwa kiasi cha bilioni mbili kimekataliwa na *NHIF* kimekwenda wapi kama hakijalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali, ni wakati muafaka wa Wizara ya Afya na TAMISEMI kukaa kwa pamoja ili kutengeneza *mechanism* itakayosaidia changamoto hii isiweze kujitokeza tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia nichangie posho kwa Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa. Waheshimiwa Madiwani wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana na wamekuwa wakikosa stahiki/posho zao mara kwa mara. Niiombe sana Serikali iweze kuangalia jambo hili ili Waheshimiwa Madiwani hao waweze kupata stahiki zao kwa muda muafaka unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nizungumzie suala la asilimia 10 za wanawake, vijana na walemavu. Sheria ipo, lakini fedha hizi zimekuwa hazipelekwi kwa wakati katika baadhi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizipongeze Halmashauri ambazo zinatekeleza sheria hii, lakini zile ambazo hazipeleki zinawanyima fursa wanawake, vijana na walemavu kutokupata mitaji. Kwa kuwa wanawake hawa, vijana na walemavu hawana dhamana ya kukopa katika vyombo vya fedha niiombe sana Serikali kwa mara nyingine tena iangalie jambo hili ili wananchi hawa waweze kupata mitaji katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimalizie pia na mimi kwa kuwapongeza sana Wakurugenzi wa Mkoa wa Singida pamoja na Madiwani kwa kusimamia vyema maendeleo. Nawapongeza sana chini ya Mkuu wangu wa Mkoa mama yangu Mheshimiwa Dkt. Rehema Nchimbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache naunga mkono hoja, nakushuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kura zinaendelea kupigwa lakini nilikuwa naangalia hapa na Mheshimiwa Spika aliwakumbusha wakati wa mjadala wa *PAC,* hii taarifa ni ya Kamati ya Bunge, sasa Mheshimiwa Mbunge ambaye anaunga mkono hoja anapiga kura ya hapana. Sasa hii siyo bajeti Waheshimiwa Wabunge tukumbuke hivyo. *(Kicheko)*

Hii ni Taarifa ya Kamati ya Bunge yaani ni ya kwetu sisi tunampa maelekezo *CAG,* siyo *CAG* peke yake lakini pia tunaipa maelekezo Serikali nini cha kwenda kufanya. Sasa kama tunakataa sisi wenyewe yale ambayo tunaunga mkono kidogo tunakuwa hatujaelewana vizuri kwamba hizi kura tunapiga za hapana za kitu gani.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso atachangia kwa dakika saba, atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Lyimo atachangia kwa dakika tano na Mheshimiwa Joseph Mkundi ajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu ya Kamati ya *LAAC* na mimi pia ni Mjumbe wa Kamati na ninaunga mkono hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza pia nitumie fursa hii kukipongeza chama changu kwa kufikisha miaka 28 toka kuanzishwa kwake, nawapongeza viongozi wote waliohudumu katika nyakati tofauti, lakini na wanachama wote ambao tumeendelea kukipigania chama katika maeneo mbalimbali, hongereni sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zangu zitajikita katika maeneo makuu mawili; kwanza ni kuhusiana na manunuzi na usimamizi wa mikataba mbalimbali ambayo inaingiwa katika Halmashauri zetu za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* ameonesha mapungufu makubwa sana yaliyoko katika suala zima la usimamizi wa manunuzi katika Serikali zetu za Mitaa hapa nchini. Katika Halmashauri za Wilaya 185 ambazo zimefanyiwa ukaguzi ni Halmashauri 115 zimeonesha kuwa na kasoro nyingi sana katika suala zima la manunuzi na katika hizo Halmashauri 185 ambazo zimetumia shilingi trilioni 1.6 kufanya manunuzi unaona ni kwa kiasi gani hizo Halmashauri 115 ambazo zina mapungufu mengi jinsi ambavyo lengo halisi halijafanikiwa kwa kuhakikisha sheria zinafuatwa za manunuzi

na kuingiwa kwa mikataba mbalimbali ili kuwaletea wananchi wetu maendeleo hazijaweza kufikiwa kwa kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *CAG* ameonesha katika ripoti yake kwamba kwa nini haya yanatokea, kwa nini kunakuwa kuna kasoro nyingi sana kwenye suala zima la manunuzi na usimamizi wa mikataba mbalimbali ambayo inaingiwa katika Halmashauri zetu za Wilaya hapa nchini. Ameonesha mambo kadhaa kwa mfano ameonesha jinsi ambavyo Halmashauri hazifuati ipasavyo muda wa utekelezaji wa mikataba mbalimbali ambayo inaingiwa, lakini imeonesha pia Halmashauri hazifuati bei halisi ya manunuzi mbalimbali ambazo zinafanya katika mamlaka yake, pia muda wa mikataba na nyongeza zinazofanyika haifuatwi kwa mujibu wa sheria na taratibu zinavotaka, pia ameanisha malipo kufanyika bila kuwa na ankala mbalimbali za malipo; pia kumekuwa na mapungufu makubwa sana ya fomu za kuainisha mahitaji halisi ya manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano tu wa baadhi ya fedha ambazo zimeainishwa katika upungufu huo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano kuna manunuzi ya bidhaa na huduma yasiyoshindwanishwa na hakuna sababu za msingi ya shilingi bilioni 32.4 katika Halmashauri za Wilaya 74. Sasa tuna Halmashauri za Wilaya 185, lakini *CAG* anatuonyesha katika Halmashauri 74 tu kuna bidhaa zilizonunuliwa bila kushindanishwa maana yake wanakiuka sheria za manunuzi ambazo zimegharimu shilingi bilioni 32.4.

Pia kuna manunuzi bila kupata idhini ya bodi ya zabuni ya shilingi bilioni tisa katika Halmashauri 47 tu, sasa unajiuliza katika Halmashauri 47 *out of* halmshauri 185 ambazo ziko hapa nchini maana yake kuna matatizo makubwa sana ya kutokufuata au kutokupata idhini ya bodi ya manunuzi katika Halmashauri zetu hapa nchini. Pia kuna manunuzi yaliyofanywa bila mpango wa manunuzi ya kiasi cha shilingi bilioni 25 kwa Halmashauri 38 tu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi tu unaona kabisa kwamba kuna matatizo na mapungufu makubwa sana katika suala zima la manunuzi katika Halmashauri zetu za Wilaya. Sasa Halmashauri za Wilaya 38 wamefanya manunuzi bila mpango wa manunuzi wa shilingi bilioni 25, vipi kuhusu Halmashauri zingine zilizobaki maana yake kwa kweli tuna tatizo kubwa zaidi ambalo lipo katika suala zima la manunuzi.

Pia kuna bidhaa za shilingi bilioni moja zililipwa lakini hazikupokelea, tunajiuliza zimeenda wapi wahusika wa jambo hili wamechukuliwa hatua gani, unanunuaje bidhaa hewa ambazo hukuzipeleka kwenye mamlaka husika au kwenye eneo husika? Lakini pia kuna matumizi ya bidhaa ya thamani ya shilingi bilioni mbili hayakuthibitishwa na mamlaka husika kwa maana ya Kamati ya Fedha na Baraza la Madiwani zimefanya manunuzi bila kupata idhini husika. Kuna manunuzi ya shilingi bilioni 1.3 hayakutolewa taarifa popote pale maana yake haijulikani kama kweli yamenunuliwa, hayakununuliwa, fedha imeenda wapi, imefanya nini, haijulikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna nyongeza ya shilingi bilioni moja kwenye mikataba isyodhinishwa na Bodi ya Zabuni, tunafahamu kuna Bodi ya Zabuni, kuna taratibu zinazotakiwa lazima Bodi ya Zabuni idhinishe, lakini manunuzi na nyongeza inafanyika bila taratibu kufuatwa. Kuna mikataba ya thamani ya shilingi bilioni 36 ilitekelezwa na wakarandasi mbalimbali bila dhamana ya utendaji, tunafahamu miradi hii inapotekelezwa lazima kuwepo na dhamana pale ambapo kunatokea na *risk* yoyote basi hiyo *risk* inaweza kuwa *covered* na hizo dhamana mbalimbali zinazotolewa. Lakini Halmashauri zinafanya miradi, Wakandarasi wanafanya miradi bila kuwepo na dhamana ya utendaji katika kazi husika wanayopewa. Kwa hiyo, huu ni udhaifu na upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri za Wilaya 29 ambazo zimefanyiwa ukaguzi na *CAG* zenye mikataba 71 ambayo ina thamani ya shilingi bilioni 111 *CAG* ameonesha

kuna upungufu wa makosa ya kimfumo 64 katika utekelezaji wa miradi hii. Sasa ukiangalia jumla yote ya shughuli hizi chache nilizozichambua kwa kuainisha kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* kwamba kuna shilingi bilioni 224.293 zimetekelezwa na Halmashauri zetu za Wilaya bila kufuata taratibu za sheria na kanuni za manunuzi. Hapa kwa tafsiri hii ya ripoti hii ya *CAG* maana yake vitengo vyetu vya manunuzi katika Halmashauri zetu za Wilaya ama hazina uwezo au watumishi walioko hawana sifa au watumishi walioko hawana weledi au watumishi walioko hawana ujuzi, pia inatupelekea kufikiri kwamba hata Maafisa Masuuli wetu walioko kwenye Halmashauri zetu za Wilaya hawana uwezo wa kusimamia Halmashauri zetu za Wilaya na ndiyo maana huko mwanzo tulikuwa tumedai na kupiga kelele kwamba hawa Maafisa Masuuli/Wakurugenzi wanapoteuliwa kushika nyazifa hizi lazima wawe ni watu ambao wanazielewa *Local Government*, wanafahamu sheria, wanahamu taratibu, wanauwezo wa kusimamia fedha zote zinazopelekwa katika Halmashauri zetu za Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni lazima sasa Serikali kupitia ripoti hii ya *CAG* kuangalia namna bora na ya haraka ya kuhakikisha vitengo vyetu vya manunuzi vinasimamiwa na kufanyiwa maboresho kwa upya, lakini watendaji wote waliohusika kwa namna moja ama nyingine kukiuka sheria, kanuni na taratibu zilizoko katika suala zima la manunuzi wanachukuliwa hatua, lakini kuangalia suala zima la kushindanisha wazabuni mbalimbali ambao wanaomba kazi katika Halmashauri zetu za Wilaya ili kuona ufanisi unaotakiwa kwenye suala zima la manunuzi unafikiwa bila tatizo lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za miradi ya maendeleo, katika Halmashauri zilizofanyiwa ukaguzi 157 hapa nchini Halmashauri hizo ziliomba shilingi trilioni 1.185 kwa ajili ya fedha za miradi ya maendeleo, lakini kilichotolewa ni kiasi cha shilingi bilioni 628 na kuna pungufu ya shilingi bilioni 556 kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* ambayo tunaijadili hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini kuna upungufu huu, kuna mambo mengi ambayo *CAG* ameweza kuainisha na kuna changamoto nyingine nyingi ambazo *CAG* amejaribu kuzionesha na Kamati pia tumeonesha katika ripoti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuna ucheleweshwaji mkubwa wa fedha za maendeleo kutoka Serikali Kuu, fedha haziendi kwa wakati, fedha zinachelewa, fedha zinazowahi ni ile *quarter* ya kwanza, ya pili na kuanzia *quarter* ya tatu na ya nne kunakuwa kuna ucheleshwaji mkubwa sana wa fedha hizi za maendeleo. Tafsiri ni kwamba tunapoenda kwenye *quarter* ya nne au mwaka wa fedha unapoisha fedha zinapelekwa kwa mkupuo kwenye Halmashauri zetu kiasi kwamba ufanisi wa miradi ya maendeleo unakuwa siyo wa kuridhisha kwa sababu fedha haziendi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani ifike mahali sasa ni bora fedha hizi za miradi ya maendeleo inayopelekwa katika Halmashauri zetu za Wilaya zipelekwe kwa *quarter* tatu tu ili tuone ufanisi wa hicho ambacho kinatarajiwa katika miradi yetu ya maendeleo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna tatizo kubwa sana la fedha za miradi ya maendeleo ambazo zinatolewa nje ya bajeti iliyoombwa. Hili ni tatizo kubwa ambalo lipo limeonyeshwa na ripoti ya *CAG* kuna Halmashauri zinapelekewa fedha zaidi ya kiasi kile ambacho wamekiomba kwenye bajeti, kuna zingine hazipewi, kuna zingine zimepewa lakini miradi haijatekelezwa, kuna zingine zimepeleka fedha kwenye matumizi mengine ambayo nje kabisa na yale yaliyokusudiwa. Ni wakati muafaka sasa kwa Serikali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele imegonga, nilitaka umalizie sentensi naona unaendelea kuorodhesha.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimalizie kwamba ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kufanyia kazi mapungufu yote yaliyoainishwa kwenye ripoti ya *CAG* ili kuleta ufanisi ambao tunatarajia kwenye Halmashauri zetu, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo atachangia kwa dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mkundi na Mheshimiwa Pascal Haonga ajiandae.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa nafasi uliyonipatia na niipongeze sana Kamati ya *LAAC* kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa sababu wote tunajua kwamba asilimia kubwa ya fedha tunazozipitisha katika bajeti kuu zinaenda kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa masikitiko makubwa niseme kwamba kumekuwa na tatizo kubwa sana la upelekaji wa fedha na wote tunajua kwamba ili tuendelee tunahitaji mambo makubwa manne, watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Lakini *the basic one* ni watu, lakini hawa watu wako wapi, hawa watu wako kwenye Halmashauri zetu na lengo la *D by D* ilikuwa vilevile ni kusogeza maendeleo na madaraka kwa watu, lakini sasa ni kwa kiasi gani Serikali Kuu inatekeleza. Itakumbukwa kwamba hapa katikati fedha nyingi zile *own source* nyingi za Halmashauri zetu zimechukuliwa na Serikali Kuu, jambo hilo lilipingwa kwa kiasi kikubwa, lakini baadae tuliambiwa kwamba Serikali inakusanya kwa sababu Halmashauri zinatofautiana, lakini ni kweli kwamba Serikali Kuu hairudishi zile fedha kwa wakati na hii imejidhiirisha katika ripoti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kwamba kwa mwaka 2015/2016 kwa mfano walipeleka asilimia 39 tu asilimia 61 hawakupeleka, sasa ukichukua hiyo miaka mitatu unakuta kwamba kwa wastani ni asilimia 53 hazikwenda

kwenye Halmashauri. Sasa hawa watu watapataje maendeleo kama fedha haziendi kwa kiwango kikubwa namna hiyo.

Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kuna kila sababu sasa kwa sababu haya mambo yamekuwa yakijirudia na bahati mbaya sijaona pendekezo la Kamati kwamba walau kiundwe chombo ambacho kitakuwa kinafuatilia kwa karibu hizi hoja zote zinazotolewa kwa sababu zinakuwa zikijirudia na siyo tu kujiridia kwa kiwango kidogo kwa kiwango kikubwa kwa mfano ukiangalia hili suala la makato ya wafanyakazi kwenye mifuko unaona kwamba kwa miaka mitatu iliyopita mwaka ule wa tatu ilikuwa shilingi milioni 960, lakini mwaka uliofuata ikawa shilingi bilioni 1.05, mwaka unaofuata tena ikawa shilingi bilioni 1.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo unaona kwamba malimbikizo yanaendelea kuwa makubwa badala ya kuendelea kupungua. Kwa hiyo, kama kungekuwa na chombo ambacho kinafuatilia mimi ninahakika haya mambo yasingekuwa mabaya kiasi hicho. Kwa hiyo, niipongeze sana Kamati, vilevile *CAG* kwa kazi kubwa ambayo ameifanya ya kuonesha mapungufu ambayo Serikali Kuu inayo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikija pia kwenye suala la Madiwani; wote tunajua kwamba Madiwani ni nguzo muhimu sana ya uwepo wetu katika Bunge hili. Madiwani wanafanya kazi kubwa usiku na mchana, lakini Madiwani baadhi ya Halmashauri unakuta Madiwani wanakopwa, yaani hawakai hata kwenye vikao na hata wakikaa vikao hivyo hawalipwi.

Sasa tulikuwa tunaomba wakati ambapo tunajua tayari imeshatolewa barua ya kwamba Mabaraza haya yanaenda kuvunjwa ndani ya wiki moja au mbili zijazo. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba sana Serikali Kuu ihakikishe inalipa Madiwani hawa posho zao. Lakini niombe pia kwa kuwa tunajua wanahitaji pia vyombo vya usafiri kama ambavyo Wabunge tunahitaji, nilikuwa naomba na Madiwani kama itawezekana Waziri wa Fedha aangalie hawa watu pia

wapate *exemption,* kama ambavyo sisi Wabunge tuna *exemption,* wapate *exemption* kwa kiwango ambacho kitaonekana kitawasaidia ili waweze kufanya kazi zao kwa urahisi zaidi kwa sababu kwa kweli wanafanya kazi ngumu sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilitaka nimalizie kwa kusema kwamba hizi fedha za makato ya wafanyakazi ni ya muhimu sana kwa sababu watu wengi wanapostaafu wanazihitaji hizi fedha na imekuwa watu wanatumia hata miaka miwili, mitatu, minne hawapati fedha kwa sababu fedha hizi zinakuwa hazijaingizwa na waajiri na waajiri wengi ni kutoka kwenye Halmashauri kwa mfano walimu, manesi na kadhalika. Kwa hiyo, nilikuwa na naomba sana hilo lifanikiwe. Lakini tulipitisha sheria ya kuhakikisha kwamba tuna ile *ten percent,* nilikuwa tunaomba sana hiyo ndiyo iwe kipaumbele kwa sababu katika Halmashauri zetu tuna wanawake wengi wenye matatizo tunavijana, tuna watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba *priority number one* iwe hiyo ili wanawake na vinaja na watu wenye ulemavu waweze kupata gawio hilo ili waweze kufanya shughuli zao. Ni wazi kwamba kuna baadhi ya Halmashauri hazijatekeleza agizo hilo. Kwa hiyo, ni ombi kwamba hilo litafanikiwa ili watu waweze kufanya kazi zao kwa uhakika na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Mheshimiwa Joseph Mkundi, atafuatiwa na Mheshimiwa Pascal Haonga, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa fursa hii, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, pia niipongeze Kamati ya *LAAC.* Nimepata fursa ya kuhudumu

kwenye Kamati hii kwa miaka miwili na nusu ya mwanzo, ninatambua ni Kamati yenye Wajumbe wenye weledi na ndiyo maana taarifa yao ni taarifa iliyosheheni uchambuzi, lakini na maoni ambayo ni ya msingi sana katika kusaidia Halmashauri zetu, Serikali lakini hasa wananchi ambao wanategemea huduma kutoka kwenye Halmashauri hizi na kwa sababu hiyo mapema kabisa nianze kwa kuunga mkono Taarifa ya Kamati ya *LAAC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Taarifa ya *LAAC* kuwa nzuri imesheheni mambo mengi, lakini nilihitaji kusisitiza kwenye maeneo machache kama yalivyotolewa na Kamati kwa mujibu wa ukaguzi uliofanywa na *CAG.*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni juu ya hoja ya marejesho ya pesa ambazo *NHIF* walipaswa kurudisha kwenye Halmashauri zetu. Kama ilivyoelezwa na Kamati hili ni tatizo kubwa na tatizo hili kimsingi linaathiri sana huduma zinazopaswa kutolewa na Halmashauri zetu hasa kwenye eneo la afya. Utakumbuka sasa hivi tuko kwenye kampeni ya kuhamasisha wananchi kujiunga na bima ili kuwasaidia kupata huduma za afya katika mazingira yaliyo mazuri. Sasa inapotokea kwamba *NHIF* imeshindwa kurejesha pesa kwenye Halmashauri, Halmashauri hizi hazitakuwa na uwezo wa kununua tena madawa ambayo yatapelekwa kwa ajili ya kuhudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukichukua kwa *case study* kwa mfano wa Ukerewe ambayo *NHIF* imeshindwa kupeleka shilingi milioni 298 ni pesa nyingi sana matokeo yake ni kwamba Halmashauri sasa haiwezi kununua tena dawa na matokeo yake vituo vyetu ambavyo vinapaswa vitoe huduma za afya vinakuwa havina madawa. Kwa hiyo, wananchi wanapoenda kupata huduma wakati unawashawishi kujiunga wawe na bima halafu wanaenda kupata huduma hawazipati kwa sababu madawa hakuna inawa-*demoralize,* hawawezi tena kuwa na moyo wa kuweza kufanya nini kuingia kwenye Mfuko wa Afya ya Jamii au kwa namna nyingine yoyote kwa sababu wanaona haina manufaa yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama iivyotolewa taarifa na Kamati tuna kila sababu ya kuisukuma na kuiomba Serikali iingilie jambo hili, hata kama kuna madeni ambayo kwa mujibu wa taarifa kwamba *MSD* wanaidai Serikali, lakini sasa kisitumike kama ndiyo kigezo cha kuwahukumu wananchi wakapata shida ya kutopata huduma ya madawa kitu ambacho siyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya wakati mwingine *MSD* wanapokuwa wanapeleka madawa, achilia mbali hii kutopeleka pesa, hata pale ambapo Halmashauri zinakuwa zinaweka *order* ya kupelekewa madawa, madawa yanayopelekwa na *MSD* wakati mwingine yanakuwa hayafikii kiwango kile ambacho walipaswa kupeleka kwa mujibu wa pesa ambazo wamelipwa na Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili si jambo jepesi tunalohitaji kulitazama tu, ni lazima sana Serikali iweze kuingilia jambo hili ili *MSD* waweze kupeleka madawa kwa mujibu wa maombi ambayo yanakuwa yamepelekwa na Halmashauri. Lakini hasa *NHIF* ni lazima hizi pesa za Halmashauri zipelekwe kwa sababu mwisho wa siku wananchi kama nilivyosema hawapati zile huduma ambazo zinatakiwa zitolewe na vituo vyetu kwa sababu madawa hakuna na Halmashauri imeshindwa kununua madawa kwa sababu pesa walizopaswa kupelekewa kwa ajili ya kununua madawa haya hawajapelekewa na *NHIF* kitu ambacho sio sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo lingine nililofikiri ni vizuri nikalisisitiza ni kwenye eneo la makato ya kisheria ambayo Halmashauri zetu hazipeleki, hii watumishi wanaathirika sana. Upande mmoja watumishi ambao wanalipwa na Serikali Kuu moja kwa moja, lakini kuna watumishi ambao bado wanalipwa na Halmashauri kupitia mapato yao ya ndani. Wengi wa watumishi hawa wanapata shida sana inapofikia muda wao wa utumishi kukoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Ukerewe kwa mfano nimewahi kukutana na kesi moja amekuja mstaafu mmoja amestaafu, ametumikia Halmashauri kwa zaidi ya miaka 20.

Mwisho wa siku anakuja kustaafu analipwa shilingi milioni tatu. Hebu tunaweza tukafikiria huyu mzee ataishi maisha gani? Sana sana tunapelekea maisha yake kuwa mafupi kwa sababu anakuwa na *frustration* nyingi, anakuwa na mambo ambayo wakati mwingine yanamvuruga kiakili, jambo ambalo tunapaswa tuliangalie na kusukuma sana ili Halmashauri hizi zipeleke makato ya kisheria ambayo zinapaswa zipeleke. Lakini tusipofanya namna hiyo, watumishi wetu wanapofikia muda wa mwisho wa utumishi wakastaafu, wanapata shida kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo lingine ni eneo la wawakilishi tulionao kwenye maeneo ya ngazi za chini kwa maana ya Madiwani, Wenyeviti wa Mitaa na Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji. Baadhi wamekwishaliongelea lakini nimekuwa ninalisema mara kwa mara, ifike wakati sasa kwa sababu pamoja na juhudi kubwa tunazozifanya pesa nyingi zinaenda kwenye Halmashauri zetu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo tunatarajia itoe huduma kwa wananchi wetu, lakini shughuli hizi zinapoenda kwenye ngazi za chini kule kwa ajili ya utekelezaji, wasimamizi wakuu ni Madiwani, wasimamizi wakuu ni Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Mitaa. Lakini bado malipo yao yanakuwa na shida sana. Wengi wameongelea malipo ya Madiwani lakini kuna watu Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji ni watu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna shida kubwa sana kwenye malipo yanayotolewa kwa viongozi wetu hawa. Halmashauri nyingi zina utaratibu wa kuwalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ambapo wanalipwa shilingi 3000, 5000 na kadhalika, ni pesa ndogo sana. Lakini achilia mbali kwamba ni pesa ndogo, lakini hata namna zinavyotolewa kwa kulipwa, wengi wanakopwa jambo ambalo linawakatisha tamaa viongozi hawa na ndio maana mara nyingi nimekuwa ninalisemea hili nikitoa wito tuone sasa utaratibu mpya wa namna gani tunaweza tukawatia moyo viongozi wetu hawa wa ngazi za chini ambao ndio wasimamizi wakuu wa miradi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wa vijiji, viongozi wa vitongoji kuwe na mfumo ambao hata kama hatutakuwa tunaweza kuwalipa kwa mwezi hata kama tutaweka utaratibu Halmashauri ziwalipe, lakini basi Serikali Kuu iwe na wajibu wa kuzisukuma Halmashauri kuhakikisha kwamba malipo haya kweli yanalipwa kwa mujibu wa utaratibu kwa namna ilivyokubalika. Lakini tukiiacha tu namna hii, viongozi wetu hawa wanapata shida sana, wanafanya kazi miaka mitano wakati mwingine kwenye Halmashauri zingine miaka yote mitano au miaka minne hawajalipwa posho zile pamoja na kwamba ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni lazima tuliingilie hili ili kwamba Halmashauri zetu ziweze kuwalipa viongozi wetu hawa wa ngazi za chini hawa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji ambao wanafanya kazi kubwa sana, lakini pesa wanayolipwa kama posho ni kidogo sana ukiachilia mbali kwamba maeneo mengine hawalipwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nichangie kwenye maeneo haya, lakini kwa kumalizia nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi ametufanyia kama wananchi wa Taifa hili, lakini kwenye kipindi hiki ambacho tulikuwa kwenye sakata la ugonjwa wa Corona. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana kutuongoza na kutuonesha njia na kimsingi ni jambo lililo wazi kwamba amekuwa kiongozi wa kidunia kwamba maono anayoyaona yale anayoyafikiria na yale anayoyaelekeza ndio ambayo viongozi wengi wa kidunia wamekuwa wanayafuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo haina shaka amekuwa Rais na Kiongozi wa kidunia tunapaswa kumtia moyo na nina kila sababu ya kumpongeza na kumtia moyo tuko nyuma yake, tuko tayari kumsaidia kwa kila namna, Mwenyezi Mungu aendelee kumsimamia na kumtia moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana kwa kunipa fursa, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Pascal Haonga atachangia kwa dakika saba atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko kwa dakika tano, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ajiandae.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi naomba niungane na waliotangulia kwamba siku ya leo chama chetu Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), chama makini kimetimiza umri wa miaka 28 na mimi naomba kukitakia kila la kheri chama chetu na chama ambacho kwa kweli kimeendelea kupigania maslahi mapana ya Watanzania bila kujali kwamba kinapitia katika changamoto mbalimbali, bila kujali kwamba kinapitia katika tanuri la moto, lakini siku zote tunajua kwamba ili dhahabu ing'ae lazima ipite kwenye moto naamini kwamba tutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* ni jicho la Bunge, *CAG* kwa kweli amejitahidi, amefanya kazi yake na kikubwa zaidi pamoja na kufanya kazi yake na kwa sababu pia ni jicho la Bunge naamini pia kwamba ni jicho la Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nichangie lile eneo la muhtasari wa mambo muhimu katika Taarifa ya *CAG* na ambalo amezungumzia ni ukurasa ule wa xviii ambao umezungumzia upungufu wa watumishi katika Halmashauri 169.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* ametuambia kwamba kuna upungufu wa watumishi wa umma katika sekta mbalimbali katika Halmashauri 169 na watumishi hao ambao wametaja upungufu hapa wamesema kwamba upungufu wa watumishi 162,342. Kama hali ipo hivyo kwenye Halmashauri hizi 169, je, hali ipoje katika Halmashauri 185?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Serikali ya Awamu ya Tano ajira imeonekana kwamba sasa sio kipaumbele tena

kwa Watanzania. Tumekuwa tukizungumza mara nyingi sana hapa Bungeni kwamba Serikali ya Awamu ya Tano kuna tatizo la kuajiri. Wapo watoto wetu, ndugu zetu waliohitimu vyuo vikuu, wapo wenye shahada, wapo wenye stashahada lakini pia wapo waliofikia kwenye ngazi mbalimbali, Serikali imewaacha waendee kusajili laini mtaani huko wakati nafasi nyingi 162,342 kuna upungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizungumza na amesema kwamba sekta ya afya na elimu ndizo ambazo zimeathirika zaidi. Mimi kwenye Wilaya yangu Halmashauri ya Mbozi kuna upungufu wa watumishi 583, Halmashauri ya Mbozi tu watumishi 583 ambapo ukiangalia kwa mfano ukienda elimu sekondari kuna upungufu wa walimu 70, lakini ukienda kwa mfano elimu msingi kuna upungufu wa walimu 609, elimu msingi. Ukienda hivyo hivyo kwenye afya kuna upungufu wa watumishi 583. kwa hiyo ukichukua elimu na afya peke yake kwa Mbozi unaona kuna karibu ya upungufu wa watumishi 1,262.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa lazima ijue kabisa kwamba miaka hii mitano haijatimiza wajibu wake wa kutoa ajira kwenye afya, kwenye elimu kwenye na kwenye kada mbalimbali katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani ni vizuri Serikali ione kwamba pamoja na kwamba imefanya makosa haya, ione kwamba ijitathimini ione je, inafaa kuendelea kuwepo kuomba ridhaa ya Watanzania iendelee kuwatumikia au ijitathmini ikiwezekana basi waingie wengine ambao wataenda kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiendelea kuwa na upungufu wa watumishi maana yake ni kwamba kutakuwa na hoja nyingi sana ambazo zitashindwa kujibiwa. Atakayekuwa amesababisha ni Serikali Kuu imesababisha kwa sababu haiajiri.

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa msemaji kwa kumuambia kwamba anapaswa arejee kumbukumbu sahihi kwama katika Serikali hii ya Awamu ya Tano imeongoza sana kutoa ajira mbalimbali za walimu, madaktari na kila mwaka kumekuwa na ongezeko ambalo ni kubwa sana. Kwa hiyo, nimpe taarifa kwamba ni vizuri aka *acknowledge* hiyo badala ya kusema kwamba Serikali hii haijatoa ajira kwa Watanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, unapoona mtu ambaye ni daktari ambaye anabishana na takwimu za *CAG* halafu ni daktari maana yake lazima tujue hapa kuna tatizo aidha kama sio ugonjwa wa uteuzi basi kuna kingine ambacho labda kinaendelea. Kwa hiyo, naomba nisiipokee hii kwa sababu hawezi kubishana na *CAG. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga ngoja tuweke vizuri. Kikanuni taarifa inaweza kupokelewa au kukataliwa halafu unaendelea. Haya mengine haya hayapo kwenye utaratibu wetu. Unaipokea Taarifa ya Mheshimiwa Chegeni au hapana?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba niikatae taarifa ya Mheshimiwa Chegeni, lakini nafahamu kwamba tupo kufanya kazi ya Watanzania na asipende kubishana na *CAG* maana yake tunamuamini *CAG. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala lile la malipo ya mishahara kwa watumishi waliokoma utumishi wao. Ukisoma ukurasa ule wa 64 na 65 wa Taarifa ya *CAG*

inaonekana bado katika Serikali hii ya awamu kuna watumishi hewa. Watumishi waliofariki wanalipwa mishahara, watumishi ambao wamestaafu wanalipwa mishahara, watumishi ambao ni watoro kazini wanalipwa mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Serikali imetuambia na imejipambanua kwamba eti ni Serikali ambayo imekuwa ikidhibiti wizi na kila kitu. Sasa ituambie kwa mwaka wa fedha 2018/2019 *CAG* anatuambia kwamba shilingi milioni 167.4 zililipwa kwa watumishi ambao utumishi wao ulikoma katika Halmashauri 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hali bado ni mbaya sana. Sasa Serikali ituambie kwa nini mtu amefariki analipwa, kwa nini ni mtoro analipwa, kwa nini huyu mtu hayupo kazini analipwa. Kwa hiyo, kuna tatizo naliona hapa lazima Serikali hii pia iendelee kujitathmini ione kama inatosha au namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la kuhusu Halmashauri kutopelekewa fedha za maendeleo. Kumbuka kwamba Halmashauri zetu zimepokonywa vyanzo mbalimbali vya mapato, wamepokonya ushuru wa mabango, wamepokonya ushuru mbalimbali kwenye Halmashauri. Sasa leo Serikali haijapeleka pesa kwenye Halmashauri karibu 157, karibu shilingi bilioni 556.8 fedha za ruzuku za maendeleo hazikupelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwaka 2017/2018 kiasi cha shilingi bilioni 480 hazikupelekwa. Kama Serikali Kuu haipeleki fedha za ruzuku za maendeleo kwenye Halmashauri, maana yake Halmashauri zimepanga maendeleo, hakuna kitakachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ni mbaya kweli kweli Halmashauri zitakufa. Tumezipokonya vyanzo vya mapato, halafu hazipelekewi ruzuku, tafsiri yake ni nini? Huku ni kwenda kuziua Halmashaur zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jambo hili lakini bado kuna fedha za maendeleo ambazo zinacheleweshwa kupelekwa kwenye Halmashauri zetu. Unapeleka fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha, kwa mfano unapeleka mwezi wa tano, unapeleka mwezi wa sita hao watu wanafanyaje maendeleo? Matokeo yake ni kwamba hizi fedha zinarudishwa Serikali Kuu, zinaporudishwa miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye Halmashauri inakwama, inakuwa haifanyiki kwa wakati na hali inakuwa ni ngumu sana. Kwa hiyo niseme tu kwamba Serikali iangalie iwahishe fedha za maendeleo kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu suala hili la kuchelewesha hili suala la malimbikizo ya mishahara na madai mengine.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga kengele ya pili imeshagonga. Ahsante sana.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba nimalizie kwa dakika moja kwamba Serikali iangalie hii malimbikizo ya mishahara na madai mengine kwa watumishi wa umma, lakini pia Serikali imeendelea kuchelewesha kuidhinishwa upandishwaji wa madaraja na nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa umma.

Kwa hiyo iangalie namna ya kuweza kurekebisha hali hii kwa sababu mwisho wa siku watumishi wa umma hawajaongezwa mishahara. Wakati huo huo wanacheleweshewa hata wanapopandishwa madaraja au vyeo wanacheleweshewa na vile ambavyo ni haki yao

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali haijafanya vizuri kabisa. Nimpongeze sana *CAG* kwa kweli naamini atafanya kazi vizuri tumpe ushirikiano na tusibishane naye tuamini kwamba ni mtu mwema atafanya kazi vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naomba kuunga mkono hoja ya Kamati, Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko atachangia kwa dakika tano, atafuatia Mheshimiwa Daimu Mpakate na Mheshimiwa Yosepher Komba ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na kabla sijachangia naomba tu ku–*register* kwamba kumekuwa na mwendelezo, kuna baadhi ya Wabunge hapa hasa wa CHADEMA tukichangia ukitaka kupata kumbukumbu zako kutoka Bunge huzipati. Lakini kwa mfano sasa hivi Bunge linaoneshwa *live,* mtu aliyepo kwenye kiti kama Mheshimiwa Spika au wewe Mheshimiwa Naibu Spika hapo nikishakutaja tu anafuatia Mheshimiwa Esther Matiko halafu wanakata yaani unakuta sionekani kile ninachokichangia. Kwa hiyo, ningependa ku–*register* hili kwamba wanachokifanya sio vizuri kwa sababu tupo hapa kushauri Serikali kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika ulizonipa ni chache sana. Ukisoma ripoti ya *CAG* utaona ameainisha kabisa kwamba kwa miaka yote mapendekezo ya *CAG* kwenye Mamlaka zetu za Halmashauri hayatekelezeki kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano kwa mwaka 2018/2019 kulikuwepo na mapendekezo takribani 10,428 lakini ambayo yalitekelezwa hayo mapendekezo au hoja yalikuwa ni asilimia 32 tu ambayo yalikuwa ni 3,334.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukiendelea ripoti inaainisha kwamba hata mapendekezo au hoja zilizoenda kwenye ripoti kuu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilikuwa 11 lakini zilitekelezwa hoja mbili tu au mapendekezo mawili tu ambayo ni asilimia 18. Sasa kama tunam–*task CAG* anafanya kazi halafu mapendekezo hayafanyiwi inatoa taswira mbili *either* Maafisa Masuhuli hawako *competent* kuweza kujibu hizo hoja na ndio maana hata wenzangu waliotangulia wame–*pledge* hapo kwamba hawa ambao

wamekuwa wanateuliwa bila kufuata *merits* za utendaji imekuwa inaleta shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine kubwa zaidi Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa ambayo ndio tumeiweka pale kusimamia hili Bunge. *CAG* ameainisha kwamba Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa asilimia kubwa hayatekelezeki. Mathalani amesema maagizo ya Kamati ya Kudumu yalikuwa 950 kwa Halmashauri 158, lakini yametekelezwa kwa asilimia 41 kwa maana maagizo 388 tu yametekelezwa. Sasa hapo inaonesha kabisa kwamba hata Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge tu inadharaulika labda, inakuwa inatumia muda mwingi kuliwakilisha Bunge kufanya hivi lakini inadharaulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye utoaji wa fedha nyingi kwenye baadhi ya Halmashauri huko Halmashauri nyingine zilikuwa hazipati kabisa. Wameainisha hapa Halmashauri 26 na kwa sababu ya muda sitazitaja zote ila zipo ukifanya rejea, utaona kabisa kwamba ibara ya 4.5.1 imeainisha hizo Halmashauri 26 zimepelekewa zaidi ya shilingi bilioni 22.8 wakati mahitaji ya bajeti yalikuwa ni shilingi bilioni 73 tu wakapeleka shilingi bilioni 96.3. Halmashauri hizi mathalani unaona kwa mfano Halmashauri ya Mji wa Lindi waliomba shilingi bilioni 1.2 wakapelekewa shilingi bilioni 3.4. Halmashauri ya Sumbawanga shilingi bilioni 3.7 wakapelekewa shilingi bilioni 8.65 wakati huo huo Halmashauri ya Bagamoyo waliomba shilingi milioni 398 wakapelekewa shilingi milioni 22 tu yaani asilimia sita tu ya walichokiomba, wakati wengine wanapelekewa shilingi bilioni nne na kitu yaani zaidi ya ile bajeti waliyoiomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hii sio sawa, hata Halmashauri yangu ya Mji wa Tarime waliomba shilingi bilioni 1.6 wakapelekewa shilingi milioni 500 tu huku mtu anaomba shilingi bilioni tatu unampelekea shilingi bilioni 8.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu ya muda, tunaomba tu. Hii kwa kweli haiwezekaniki tunaomba usawa uwepo kwenye kupeleka fedha kwenye Halmashauri.

Vinginevyo ije ifanyike *forensic audit* tujue kulikuwa kuna msukumo gani kuweza kupeleka fedha nyingi kwenye hizi Halmashauri ambazo zipo 26. Pamoja na ile ambayo Mheshimiwa Rais anatoka ile ya Chato na yenyewe imepelekewa fedha nyingi kuliko bajeti iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni hii ya neno la bakaa, tumeshuhudia na wenzangu wamesema hapa. Kwa mfano kwa mwaka 2018/2019 walipeleka fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 913; zilizotumika ni shilingi bilioni 655 tu zikabaki bakaa shilingi bilioni 258 hizi fedha zimeenda zimechelewa na haziendi kwa utoshelezi. Lakini kwa sababu wanazipeleka *quarter* ya mwisho zinatumika unakuta *quarter* imeisha zinarudi Hazina. Hii inakuwa hatuwatendei haki wananchi wetu ambapo hii Wizara ndio inatumikia kutoa huduma kwa wananchi kule chini.

Kwa hiyo, naliomba Bunge likemee na liazimie kwamba wawe wanalipa fedha kwenye *quarter* ya kwanza na ya pili wamechelewa sana ya tatu yamebaki kidogo basi ndio wamalizie ya nne, maana yake sasa hivi wanapelekea *quarter* nne makusudi tu wanajua baada ya muda zitarudi na miradi itakuwa haijafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Dakika tano zimeshaisha Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. ESTHER N MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaniongeza mbili tu?

**NAIBU SPIKA:** Nina majina mengi hapa Mheshimiwa.

**MHE. ESTHER N MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize kwamba zile hoja zote ambazo zimeainishwa kwenye *report* ya *CAG*...

**NAIBU SPIKA:** Muda umeshaisha Mheshimiwa wenzako hawatapata fursa ya kuzungumza.

**MHE. ESTHER N MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sekunde moja tu.

**NAIBU SPIKA:** Fanya kwa maandishi Mheshimiwa.

**MHE. ESTHER N MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono zile hoja zote zilizoainishwa na Kamati ziweze kutekelezwa, lakini na *report* ya *CAG* iweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tujitahidi tukisikia kengele kwa sababu nikishika *microphone* hapa mbele maana yake unachokisema chote mwishoni hakitaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kwa hiyo utakuwa haujafanya kitu chochote sasa najitahidi kutokushika *microphone,* lakini mnatumia muda mrefu halafu wachangiaji bado wako wengi.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate atafuatiwa na Mheshimiwa Yosepher Ferdnand Komba, Mheshimiwa *Engineer* Ngonyani ajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii kuongea/kuchangia taarifa ya *LAAC*. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama siku ya leo na namshukuru mke wangu pamoja na familia yangu kunivumilia katika kazi hii ya Ubunge kwa kipindi cha miaka mitano pamoja na wapiga kura wangu wa Jimbo la Tunduru Kusini.

Pamoja na shukurani hizo zote naishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa yale yote ambayo yamefanyika katika Jimbo langu la Tunduru Kusini pamoja ikiongozwa na Jemedari wetu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mungu ampe maisha marefu, afanye kazi kwa uvumilivu ili aendelee kututumikia kama mpango wa Mwenyezi Mungu ulivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye hoja niwashukuru sana wenzetu wa Kamati ya *LAAC* kwa taarifa yao nzuri ambayo imedadavua vizuri taarifa ya *CAG* kwa ufupi na *CAG* wenyewe wamefanya kazi nzuri, wameonesha hali halisi ya utendaji wa Halmashauri zetu katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri. Lakini niwapongeze sana Wakurugenzi wa Halmashauri ambao wamepata hati safi, wamefanya kazi nzuri na imeonesha namna gani Wakurugenzi hawa wanamuelewa Mheshimiwa Rais, idadi ya hati chafu zimepungua kwa asilimia kubwa, kwa hiyo, tuwapongeze hawa Wakurugenzi pamoja na watumishi wenzao ambao wamefanya Halmashauri hizi ziweze kupata hati safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo niwashukuru *LAAC* kwa kuonesha hoja mbalimbali ambazo zinatakiwa Serikali zifanyiwe maboresho ili ukaguzi wa *CAG* uendelee kuwa mzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya hoja ambayo nimeona ni ya msingi Serikali iweze kuiangalia wa makini zaidi hili suala la matumizi mabaya au matumizi yasiyo sahihi ya *POS*. Ni ukweli usiopingika *POS* imesaidia katika maeneo mengi kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na Serikali kwa ujumla, lakini kwa kuwa imeongeza makusanyo na bahati mbaya kuna watumishi ambao walikuwa wanafaidika na mtindo wa zamani wa kukusanya mapato *to* India kutumia na *POS* na *POS* inaonesha matumizi yote yanayopatikana, kwa hiyo, changamoto inayotokana na matumizi yasiyokuwa sahihi ya *POS* imesababisha na aidha binadamu kwa bahati mbaya au kwa bahati nzuri, kwa makusudi ili kuhakikisha kwamba mapato yale yanayopatikana mengine yanaenda mifukoni mwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ifike wakati sasa kila halmshauri iwe ni lazima izi *poss* katika maeneo ambayo tunakusanyia mapato yapatikane na wote ambao wamekabidhiwa hizi *POS* basi wapimwe kutokana na makusanyo yanayotokana na zile *POS* katika maeneo yao.

Naamini bajeti zote za Halmashauri zinaanzia kwenye ngazi ya vijiji kwenda kwenye kata, Halmashauri, Mkoani mpaka inafika Wizarani. Kwa hiyo mapato na matumizi mengi mapato yanatengwa yanapangwa na wao wenyewe, sasa kutokukusanya maana yake kwamba wameshindwa kutekeleza wajibu na kile ambacho wameweza kukipanga. Kwa hiyo, sasa nashauri Serikali itumie mtindo wa kuweza kupima hawa watendaji wetu kwa namna ambavyo wanakusanya mapato ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na matumizi haya ya *POS* kuwa mabovu kuna tabia ya watendaji ambao wapo kama wale ambao sio waaminifu wafanyabiashara wakubwa wale wanaotumia zile *EFD,* anakwambia leo bei yangu ni shilingi milioni mbili kama hauna *EFD*, ukiwa na *EFD* basi itabidi ulipe 2,360,000 wako watumishi wa namna hiyo wanatumia kwenye hizi *POS* kwamba nikuandikia *POS* utalipa shilingi 200,000 bila *POS* lipa 100,000 huko njiani usiwe na wasiwasi utasaidiwa kupita na wenzangu. Hili jambo inatakiwa tuwe makini kwa sababu ni matumizi ambayo sio sahihi ya hizi *POS*, basi ni vizuri Halmashauri iangalie wale wote ambao sio waadilifu wanaotumia hizi *POS* kwa ajili ya kujinufaisha wenyewe basi na wao wachukuliwe hatua ikiwezekana waweze kufukuzwa kazi wawapishe wale ambao wana uchungu wa kuweza kukusanya mapato ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zetu mapato yake yamekuwa ni madogo kutokana na watu kama hawa, kwa hiyo, nashauri Serikali iangalie kwa sababu hizi posho tunazolalamika za Madiwani, posho ya Mwenyekiti wa Vijiji zote hizi zinatokana na makusanyo haya yanayotokana na hawa wetendaji ambao wanapewa *POS* na kama wanakwenda vibaya maana yake Madiwani hawatapata posho, wala Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji hawatapata posho.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbeshe wenzangu Wabunge bajeti ya mwaka 2017/2018 ya TAMISEMI, Waziri wa kipindi kile Mheshimiwa Simbachawene alitoa kauli hapa

Bungeni kwamba Halmashauri yoyote ambayo itashindwa kufikisha makusanyo yake ya ndani asilimia 80 basi wataanza kuzishughulikia kwa maana ya kuzifuta. Kwa hiyo naomba hili jambo lichukuliwe maanani ukionesha mfano Halmashauri mbili, tatu hawa watumishi pamoja na Madiwani wao watakuwa kipaumbele katika kuhakikisha kwamba mapato ya Halmashauri ambao wamepanga wenyewe kutokana na vikao vyao halali vinafanikiwa ili tuweze kusonga mbele kwa sababu mahitaji ya fedha kwenye maeneo yetu ni makubwa na uwezo wa Serikali kugharamia kila jambo imekuwa ni mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaenda ukurasa wa 10 suala la mfumo wa *EPICAR*. *EPICAR* imekuwa ni kichaka cha kujifichia, kuchelewesha malipo mbalimbali aidha ya wazabuni au ya watumishi mbalimbali, mtu au mtumishi anaamua kusema *EPICAR* leo imegoma, unakaa siku tatu, siku nne mpaka tano *EPICAR* imegoma, mtu anakaa mjini siku saba, nane anasubiria *EPICAR* ifunguke kumbe pesa hakuna, lakini wanashindwa kuwaeleza kwamba jamani pesa hamna. Kwa hiyo *EPICAR* hii naomba waiangalie sana kwa sababu inachelewesha malipo ya watumishi pamoja na wazabuni wetu ambao wanapewa kazi mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa nishauri ni suala la watumishi. Ni kweli watumishi katika Halmashauri yetu ni tatizo, ukiangalia miradi mingi inayofanyika vijijini inatakiwa isimamiwe vizuri, Halmashauri nyingi hazina wahandisi ambao wanaweza kusimamia hii miradi ambayo iko katika maeneo mengi. Pamoja na wahandisi lakini bado kwenye vijiji vingi kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru vijiji tunavyo 157 lakini vijiji 40 havina watendaji wa vijiji ambao kwa namna moja au nyingine ndio wataalam ambao wanaweza kuishauri Halmashauri ya kijiji. Kwa hiyo utakuta anaye kaimu hajakwenda shule, hajui chochote, hana semina, hana uchungu, anafanya vile ambavyo anaviona vinafaa ili kuendesha Halmashauri ya Kijiji. Nadhani katika kuangalia haya matumizi mabovu ya fedha basi ni vizuri Serikali ione ni

muhimu sana suala la watumishi kuwaongeza kwenye Halmashauri zetu ili kupunguza matumizi mabovu ya fedha katika miradi mbalimbali ambayo inapelekwa huko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa nichangie ni suala la mgao wa fedha katika Halmashauri hasa zinazotokana na ruzuku. Ni kweli haileti afya kwenye masikio ya watu kusikia Halmashauri nyingine imepewa pesa nyingi zaidi ya ruzuku kinyume na kile walichokadiria na Halmashauri nyingine hata nusu ya ile walichokadiriwa hawajapata. Kwa kweli haileti picha nzuri, hii nchi ni yetu wote, Halmashauri zote ni mali ya Serikali, basi waone angalau ile bajeti iliyotengwa katika kila Halmashauri kwa ajili ya shughuli za maendeleo basi ile pesa iende ikiwa na ziada basi waangalie hayo maeneo ambayo yana uhitaji zaidi wa fedha ili kuhakikisha miradi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili kwa kweli linaleta sura tofauti ukiangalia namna ambavyo Halmashauri imekisia kulingana na bajeti kwamba tutafanya miradi moja, mbili, tatu, nne, tano, kwa hiyo na mwingine anapewa hela nusu miradi aliyoikisia haiwezi kukamilika kwa sababu pesa haiwezi kutosheleza kwa miradi ile ambayo wameikisia. Naomba sana Serikali hili iliangalie ili kuleta usawa katika Halmashauri zote ili wao nao waweze kufaidika na hii keki yetu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nimelisikia kwenye taarifa hii ni suala la nyaraka mbalimbali wakati *CAG* anakuwepo kwenye ukaguzi. Ni kweli maeneo mengi kukiwa na matatizo tunashirikisha wenzetu wa TAKUKURU kwa ajili ya kuleta ufanisi au kuangalia matumizi sahihi ya zile nyaraka ambazo zilizopo. Nadhani wenzetu watumishi wanatumia hiki kama kichaka cha kuficha baadhi ya *document,* sheria inasema kabisa kama wanatoa *document* unapeleka TAKUKURU basi kuna nakala ambayo imekuwa *certified* na mwanasheria ibaki katika ofisi, sasa inaonekana kila wanapokwenda TAKUKURU karatasi zikichukuliwa hakuna nakala yoyote inabaki katika ofisi. Hili jambo linaleta ukakasi na *CAG* hata anapotoa siku zile 21

kwa ajili ya kuhakikisha wanafanya *reconciliation* hao wenzetu wa Halmashauri wanashindwa kwenda kuzichukua zile *document,* basi uweke utaratibu ambao utasaidia watu wa TAKUKURU wanapochukua *document* waandike *in writing* kwamba *document* hii tunaichukua, nakala hizi wanaziacha ili ziweze kufanya kazi ya *CAG* iwe rahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana Halmashauri nyingi zimepata hati chafu kwa sababu ya *document* hizi kuwepo TAKUKURU na wao kutokuwa na nakala ya aina yoyote wakati ni sahihi zile *document* zimechukuliwa na wenzetu wa TAKUKURU. Kwa hiyo, naomba sana hili jambno liangaliwe ili kupunguza hati chafu kwenye Halmashauri zetu nazo zionekane zinaenda sambamba na suala la fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi narudia kushukuru kwa kunipa nafasi ya kuongea jioni hii lakini nishukuru Serikali kwa yale yote ambayo yamefanywa kwenye Jimbo langu la Tunduru Kusini, lakini nashukuru kwa wananchi wenzangu wa Jimbo la Tunduru Kusini kwa kuniamini kuwa Mbunge wao miaka hii mitano na ninaamini kwa kuwa mambo yamekuwa mazuri wataendelea kuniamini ili tuweze kuendelea kusukumua gurudumu letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba atachangia kwa dakika saba, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Ngonyani, Mheshimiwa Rose Kamili ajiandae.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia na mimi namshukuru Mungu kwa zawadi ya afya njema niko salama, nashukuru na familia iko salama, lakini kwa namna ya kipekee napenda kukipongeza chama changu kukitakia *birthday* njema leo kinafikisha miaka 28 na bado kiko imara, kinaendelea kuwa imara na ndio maana unakuta kelele zinakuwa nyingi kwa sababu kinaonekana kina *impact* kwenye nchi hii. Ingekuwa

nia kama vile vyama vingine kingekuwa hata hakitajwi, lakini usiku na mchana ni CHADEMA, kwa hiyo nazidi kumuomba Mungu chama hichi chenye dhamira ya dhati kiweze kutufikisha katika malengo ya demokrasia na haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naunga mkono mawazo ya Kamati na mapendekezo waliyoyatoa. Naomba nianze na suala la ukiukwaji Sheria za Manunuzi, kwenye ripoti ya *CAG* ameonesha mwaka 2018/2019 kuna zaidi ya shilingi bilioni 9.2 zimefanya manunuzi tofauti na kinyume na utaratibu ambazo zipo kwenye Halmshauri zetu, Bodi ya Zabuni haijatoa idhini. Pia kuna Halmashauri zimefanya manunuzi lakini pia zimeanza kutumia zile bidhaa kabla hazijakaguliwa na hazijapitishwa na zile bodi. Wakati nasoma taarifa ya *CAG* inawezekana kuna jambo lipo nje ambalo *CAG* labda kwa nafasi yake hawezi kulisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamizi mkuu au Afisa Masuuli wa Halmashauri ni Mkurugenzi wa Halmashauri, haya yote yanafanyika kwa maana ya Wakurugenzi kwa namna moja au nyingine wanabariki haya mambo, wao ndio wasimamizi. Mimi natokea Mkoa wa Tanga, ukiangalia changamoto nyingi kwenye Halmashauri zipo kwenye Wilaya ya Mji Korogwe, zipo Lushoto, ziko Mkinga, ziko Bumbuli. Mimi niiombe Serikali ifuate taratibu pale inapoajiri watumishi, hizi changamoto zote zinaonekana kuna taratibu za uajiri zinarukwa na sisi tunafahamu kwamba Wakurugenzi wengi ukifuatilia kwenye Halmashauri zetu ni wale ambao labda walishindwa kura za maoni za CCM au walifanya jambo la kufurahisha mtu fulani au kikundi fulani au Serikali, ndio wakapewa kuwa Wakurugenzi, wengi wao hawana misingi ya utendaji kazi kwenye Halmashauri. Unakuta zinatokea hizi changamoto wanafanya manunuzi, wanafanya matumizi ambayo yako nje ya taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nataka kuongelea ni la ruzuku la fedha za maendeleo, tumeona hapa wameongea wengi, yako maeneo yamepelekewa zaidi, na zaidi ya Halmashauri 26 zimepelekewa 22.8 bilioni, yako maeneo yamepelekewa pungufu, yako maeneo

hayajapelekewa kabisa. Nimekuwa nikijuliza kwa taratibu za malipo ya Serikali zilivyokuwa na taratibu nyingi na za uhakiki za kila hatua inakuwaje Halmashauri iombe shilingi milioni 100 labda tusema halafu ipelekewe shilingi milioni 200. Lazima sisi kama Bunge tuwe *serious* kwenye hili suala, inavyoonekana Halmashauri ambazo zinapelekewa fedha zaidia ambazo zimeomba ndiko kwenye vichaka vya watu kupiga hela, haiwezekani Halmashauri iombe kiasi fulani ipelekewa zaidi na kuna Halmashauri ambayo imeomba kiasi fulani haijapelekewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Fedha aje atuambie utaratibu gani unafanya haya makosa yanaendelea kutendeka, nini kinatokea kiasi kwamba wanaofanya malipo ya kupeleka fedha za miradi ya maendeleo wanapeleka fedha zaidi kuliko kile ambacho kimeombwa wakati tunajua kuna *cealing* ya bajeti, nani anayeidhisha hizi hela kwa kiwango kikubwa tofauti na ambacho kimeombwa. Naomba hilo tupatiwe majibu sahihi, hivi tutaamini hii ndio mlango ambao watu wanautumia kupiga hela za Serikali kutumia hovyo hela za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine limeoneshwa kwenye taarifa hapa kukosekana kwa hati miliki za ardhi, majengo na mali nyingine ambazo zinafikia shilingi bilioni 85.8 na moja ya maeneo imetajwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kwenye shilingi bilioni 1.4 kwenye eneo la pale Darajani ni eneo ambalo ninaamini ni lile eneo ambalo limejengwa tenki la maji/mradi wa maji, lakini pia kwenye Jiji la Tanga na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ni moja Serikali hii ambayo inasema ndani ya siku 90 unaweza ukapata hati, ni Serikali hii ambayo ina mali za zaidi ya shilingi bilioni 85 ambazo hazina hati miliki, tunashindwa kuwaelewa, kama mwananchi wa kawaida unamwambia siku 90 atapata hati miliki, lakini ninyi wenyewe Serikali mnaendelea kupata upotevu kuwa na mali za zaidi ya shilingi bilioni 85 ambazo hazina hati wakati michakato yote mnafanya ninyi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtueleze haya maeneo haya majengo ambayo hayana hati miliki mpaka sasa hivi ni *either* mmeyachukua kwa watu kinyume na taratibu, *either* mmeyachukua kwa wananchi hamna uhakika kwamba au hamjalipa fidia, haiwezekani kama ni maeneo yenu, ni maeneo ya Serikali mpaka sasa hivi yanakosa hati miliki.

Kwa hiyo, nataka nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kama atapata nafasi atuambie kwa nini maeneo ya Serikali yanakosa hati miliki wakati nilitegemea Wizara ingekuwa na jukumu la kuhakikisha mali za Serikali zinalindwa kwanza kuwa na hati miliki kabla ya mali za wananchi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nilitaka nizungumzie ni malipo ya hasa Madiwani wetu kwenye Halmashauri. Yapo malipo ya afya kuna Halmashauri wanachelewesha kupeleka, lakini pia yako malipo ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inacheleweshwa, lakini pia kuna kesi nyingine ambayo nadhani *CAG* hajai-*point* moja kwa moja mikopo yao inapofikia mwisho wanajikuta kuna kiasi wanatakia walipe kama vile *penalt* ya kucheleweshwa mikopo na wakati wanaolipa mikopo ile sio wao ni Halmashauri.

Kwa hiyo, niwaombe wapeleke fedha kwa wakati kama ni madeni ya Madiwani, kama ni fedha kwa ajili ya mambo ya afya walipe wka wakati ili Mdiwani wetu wasipate usumbufu lakini pia waongezewe posho yao, wanalipwa shilingi 350,000…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, kengele ya pili imekwishakugongwa, ahsante sana.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa *Engineer* Ngonyani atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Kamili, Mheshimiwa Japhary Michael ajiandae.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa fursa hii leo kuongea mbele ya Bunge lako tukufu. Pili, nikushukuru wewe kwa kunipa hii fursa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache ya kuyaongelea; kwanza ni kuhususiana na changamoto za baadhi ya Maafisa Masuuli kushindwa kukusanya *VAT* katika miradi ambayo inafadhiliwa na wahisani.

Mimi niiombe Serikali, masharti ya wafadhili wengi wanataka hela zao zitumike kwenye miradi. Hawajisikii kabisa hela zao zikakatwa kodi na *VAT,* hii kwao ni kodi. Nimuombe Waziri wa Fedha ajaribu kuliangalia hili kwamba miradi yote inayofadhiliwa na wahisani basi iwe *VAT exempted* ili tuondokane na hii changamoto ya *CAG* kila wakati atakuja na hii hoja ya Maafisa Masuuli kushindwa kukusanya *VAT* kwenye miradi ambayo inafadhiliwa na wahisani.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ningependa kusisitizia tu wenzangu wengi wameliongelea, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutozingatia sheria, kanuni na taratibu. Kwa kweli niiombe sana Serikali hakuna njia nyingine ya kurekebisha hili zaidi ya kuchukua hatua pale ambapo changamoto hizi zinajitokeza. Tusipochukua hatua tunalea makosa hayo na miaka hadi miaka watu watatumia mwanya huo kutumia vibaya fedha za walipa kodi. Niziombe mamlala husika zichukue hatua kwa Maafisa Masuuli ambao wanapitisha malipo katika malipo ambayo hayajakamilika kwa mujibu wa taratibu, sheria na kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya Hazina kutokupeleka fedha kwenye Halmashauri, ni hoja ambayo hata ninakotoka ni changamoto kubwa. Niiombe Serikali miradi ile ambayo inapitishwa na Halmashauri ni miradi ambayo imeibuliwa na wananchi, ni miradi inayogusa maisha ya siku hadi siku ya wananchi, niombe sana Waziri wa Fedha atoe kipaumbele. Kwanza thamani ya ile miradi ni ndogo, fedha zinazohitajika ni kidogo, hebu toeni hizo fedha, zinawagusa wananchi wengi, zinatatua changamoto za

Wananchi wengi. Tunaongelea fedha zisizozidi milioni 100, milioni 200 kwa ajili ye ujenzi wa zahanati na vituo vya afya.

Nikuombe sana Waziri wa Fedha hebu liangalie hili. ni kweli mnatoa vipaumbele katika miradi ya kimkakati, lakini kwetu sisi ambao tunawawakilisha Wananchi wengi, kipaumbele chetu ni zile shida ambazo Wananchi wanahangaika nazo siku hadi siku. Kwetu sisi kukamilisha ujenzi wa zahanati, kituo cha afya ni muhimu zaidi kwasababu inagusa maisha ya Wananchi ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya *NHIF* kutorudisha gharama; ni hoja ambayo hata kwenye Halmashauri yangu inaguswa na mimi naunga mkono mapendekezo ya Kamati ya *LAAC.* Kwa kweli hii hoja inasumbua sana. Inawezekana, niliwahi kusikia kwamba wanaojiunga na nikichukulia *CHF* wengi ni wagonjwa, kwa hiyo ile dhana ya kuwa na *CHF* haitekelezeki sana kama wanaojiunga wote ni wagonjwa, lakini nadhani *NHIF* kwa sehemu kubwa ni watumishi wa Serikali. Niiombe Serikali iwasiliane kwa karibu na *NHIF* warudishe hizi gharama ili huduma za afya ziweze kutolewa huko tuliko ambako watumishi wengi sana walioko huko kwenye Halmashauri wanapata shida. Wanakatwa kila mwezi, lakini wanapokwenda hospitali hawapati huduma inayostahili kwa sababu ni kwamba Serikali au *NHIF* haitoi mafungu yale yanayotakiwa kurudi katika Halmashauri waweze kununulia madawa na vitendanishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana tuweke mkazo zaidi kwa *NHIF* kutekeleza wajibu wake isilete hivi visingizio vya kutokujazwa fomu kikamilifu, mimi hiyo naita kisingizio kwa sababu kama mtu hajajaza fomu kikamilifu lakini huduma kapata, kinachotakiwa ni kurekebisha tu ile fomu, lakini siyo kukataa kurudisha gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee vilevile suala la urasimu katika kupitisha hati za malipo kwa wakandarasi na katika Halmashauri zetu wanaoathirika zaidi ni wakandarasi ambao ni wazalendo. Tunatakiwa tuwalee. Siyo wote wenye

uwezo wa kifedha wa kuweza kutekeleza mradi kikamilifu na baadae aendelee kuidai Serikali kidogo kidogo, uwezo huo hawana. Niwaombe hati zote za malipo zinazotokana na kazi ambazo wakandarasi wameshazifanya zilipwe ili tuweze kuwaendeleza hawa wakandarasi ambao kwa sehemu kubwa ni hawa wakandarasi wazalendo waweze kukua na hatimaye eneo hili la ukandarasi tuweze kulitawala sisi wenyewe Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto za *POS;* nimeisikia Kamati ya *LAAC* ilivyosema, lakini mimi nilitakja kuongezea kitu kimoja ambacho *CAG* naomba anisikilize. Kwetu sisi na kuna maeneo mengine *POS* inafanyakazi lakini watumishi hawawasilishi fedha benki kwa visingizo mbalimbali. Tumeletewa hizi *POS* mpya ambazo kama hujapeleka fedha benki zinajifunga. Sina uhakika sana na ufanisi wake, lakini bado tuna changamoto ya watumishi wengi wanakusanya fedha, wanatumia *POS* vizuri, lakini fedha hawa-*bank* kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Halmashauri labda zinatakiwa kuchukua hatua za kuwafukuza, kuwasimamisha kazi watu kama hao, lakini wakiwa wengi sana linakuwa ni tatizo. Tutafute namna ya kutatua kwa maana ya kimfumo kuliko kusema tuwatafute wale ambao wanachezea huo mfumo itakuwa ni rahisi sana kama tutaimarisha zaidi mfumo ili usiwe *tempered* kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho; kwa kweli ninaunga mkono mapendekezo yote nane ambayo Kamati ya *LAAC* wameyatoa yote nayaunga mkono na vilevile nichukue fursa hii kumshukuru sana Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya. Haya maendeleo tuliyoyapata kwa sasa ya Halmashauri nyingi kupata hati safi siyo dhamira njema za Maafisa Masuuli, ni usimamizi imara wa Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba usimamizi huo uendelee lakini wakati huo huo tuimarishe mifumo ili michezo hii ya Maafisa Masuuli ku-*temper* na hela za walipa kodi

upungue au uondoke kabisa ili tuweze kupata *value for money* kwa zile hela ambazo wananchi wanalipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mwisho; nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa namna alivyotuongoza katika kipindi hiki cha changamoto za *Covid-19.* Kwa kweli nirudie, niliwaambia wananchi wangu wakati wa kampeni mwaka 2015, Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ni zawadi yetu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Amepakwa mafuta kuliongoza Taifa hili katika kipindi hiki. Tumuunge mkono na sasa tunaona matunda yake. Hongera sana Mheshimiwa Rais na kwa kweli nirudie kile ambacho Wananamtumbo walikisema; wanamtaka aendelee kukaa hapo mpaka akamilishe ujenzi wa reli ya kutoa Mtwara hadi Mbambabay hata kama itamchukua miaka 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Rose Kamili atachangia kwa dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Japhary Michael dakika tano, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ajiandae dakika tano.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii kuweza kuchangia taarifa ya Kamati yetu ya *LAAC* na mimi pia ni Mjumbe wa Kamati hii, kwa hiyo, tumezingatia miongozo na stahiki ya ukaguzi wa fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninakwenda kwenye sehemu ambayo taratibu za Serikali Kuu zilizochangia kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; inahusu urasimu katika kupitisha hati za malipo ya wakandarasi. Hii imesababisha kutokutekelezwa kwa miradi ya maendeleo kwa wakati katika Halmashauri zetu zote na pia ni kuvunja mioyo ya wakandarasi na pia wananchi kukosa huduma ipasavyo kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia utaratibu huu ulivyo mgumu ni kwamba utaratibu wa kupitisha hati ya madai, mkandarasi akishapitisha anapeleka kwa Mkurugenzi na Mkurugenzi anapeleka kwa *RAS* Mkoani, Mkoani *RAS* akipitisha anapeleka TAMISEMI, TAMISEMI wakimaliza wanapeleka sasa ka Wizara ya Fedha. Uangalie huo urasimu unavyotokea kiasi kwamba miradi ya maendeleo inachelewa kwa kutekelezwa kwa muda unaotakiwa na fedha pia kutokuwafikia hawa wenzetu ambao wanasimamia au wanafanya ujenzi wa miradi yetu ya maendeleo ndani ya TAMISEMI. Na pia hili linakuwa ni tatizo kubwa sana kwa sababu linasababisha kuwa na hoja kwenye Halmashauri husika sasa hizi hoja hazitokani na Halmashauri wao kuwa na tatizo, tatizo linakuwa Serikali Kuu. Kwa hiyo, tunaomba kwamba Wizara ya Fedha iangalie mbinu nyingine ya kuweza kutekeleza haya masuala ili Halmashauri isiwe na hoja za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni kwamba miradi ya maji kutokukamilika mapema na yote ni kwa ajili ya urasimu huo. Hakuna miradi ya maji inatekelezeka kwa sababu ya huu urasimu wa kupitisha madai ya wakandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ujenzi wa Halmashauri; Halmashauri nyingi kama vile Bariadi, kuna Halmashauri ya Mbulu, kuna wapi, sehemu mbalimbali utakuta Halmashauri zinashindwa kutekeleza kwa wakati kwa sababu ya kuchelewa kupitishiwa hayo madai ya wakandarasi wanaohusika na miradi hiyo. Na pia inawagusa sana wale wa barabara kama *TARURA* na kadhalika. Kwahiyo, ninaiomba Serikali Kuu iliangalie hilo, Waziri wa Fedha aliangelie kwa undani jinsi gani tunaweza kutatua hili tatizo ili kuweza kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo linahusu Serikali Kuu ni kuhusu hoja za Serikali kutokuwasilisha ipasavyo ruzuku ya fedha za maendeleo kwa Halmashauri; hii imekuwa tatizo kubwa sana kwani utakuta fedha zinapelekwa nyingi kuliko kiasi kilichoombwa na Halmashauri; na Halmashauri ni chache tu, ni kama 26 lakini Halmashauri

nyingi karibu 157 na hazikupelekewa hizo fedha, sasa tunajaribu kuangalia kuna tatizo gani kwenye Wizara ya Fedha. Ni kwa nini hizo fedha hawazipeleki kwa wakati na kwa nini wengine wapalekewe fedha nyingi kupita kiasi?

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake Halmashauri wanaanza kutumia zile fedha vibaya kwa sababu kama fedha zimepelekwa hazitoshi wanaona ngoja wakope wapeleke mahali kwingine kumbe ni kosa kufanya matumizi kama hayo kulepeleka mahali pengine kwa sababu haitoshi kwa ule mradi ambao waliuombea. Sasa kuna tatizo gani tunapenda kujua. Mfano mzuri; kuna Halmashauri 26 zilipokea fedha jumla ya shilingi bilioni 22.8 na ukiangalia zaidi ya hizo fedha utakuta kwa mfano Halmashauri ya Songwe imepelekewa zaidi ya shilingi bilioni moja, Halmashauri nyingine ni ya Busokelo imepelekewa zaidi ya shilingi bilioni 1.4 na zingine shilingi milioni 100, zingine shilingi milioni 400 na kadhalika, lakini je, tunauliza, kwanini mpeleke fedha nyingi kwenye hizo Halmashauri halafu Halmashauri zingine hamkuwapelekea fedha? Kwa sababu hizo Halmashauri 157 ambazo zilihitaji kupokea hizo fedha hawajapelekewa fedha za shilingi bilioni 556.8 hawakupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unafaidisha Halmashauri 26 unawanyima Halmashauri 157 fedha nyingi za maendeleo kwa hiyo ni kuwanyima maendeleo kwa kweli kwenye Halmashauri hizo na siyo sahihi kabisa. Hiyo yote hizi hoja zinatokana na Serikali Kuu au Wizara yetu ya Fedha kutokupeleka hizo fedha inavyopaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ninapenda kuizungumzia ni baadhi ya Halmashauri kutozingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha na manunuzi ya umma katika kutekeleza miradi ya maendeleo, wanakiuka sana hawa wenzetu na ukiliangalia hili kwa kweli Halmashauri unajaribu kutumia fedha ambazo wewe hukustahili kuzitumia kabla ya zabuni kuzipitisha. Kwa hiyo, ni kosa kubwa sana ambalo halistahili kwa kweli kufanyika kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba uvunjifu huu uliofanyika wa Sheria za Manunuzi wachukuliwe hatua.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele imeshagonga, ahsante sana. Mheshimiwa Japhary Michael dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu dakika tano, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye hoja hii ya Kamati ya *LAAC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kupata nafasi hii ya kuwa Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini kwa kipindi sasa cha miaka mitano na nimshukuru Mungu sana kwa kunifanya nikawa ndani ya jengo hili na kupata uelewa ambao nimeweza kuupata lakini pia kuwawakilisha wananchi wa Moshi Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii ya Kamati ya *LAAC* nishukuru sana kazi ambayo *CAG* ameifanya ambayo imeweza kusaidia namna ambavyo tunaweza tukasaidia Halmashauri zetu kufanya vizuri zaidi, lakini niipongeze sana Kamati ya *LAAC* kwa kupitia maeneo mbalimbali na kuonesha maeneo ambayo yanapaswa kuangaliwa kwa umakini ili kuboresha utendaji wa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika baadhi ya hoja, hoja kubwa ambayo inaonekana ni hoja ya kutopelekwa kwa fedha za miradi ya maendeleo katika Halmashauri nyingi kama ilivyozungumzwa na ripoti ya *CAG* na ukiangalia katika ripoti ya *CAG* tangu mwaka 2015 mpaka 2014/2019 ni karibu shilingi trilioni 2.1 ambazo hazikupelekwa kama fedha za miradi ya maendeleo. Maana yake ni kwamba mara nyingi nimekuwa nikijaribu kushauri na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ikishauri kwamba katika kosa ambalo tunalifanya lakini hatulitazami vizuri ni uamuzi wa kufanya *centralization***,** uamuzi wa kuanza kuchukua vyanzo vya mapato ya Halmashauri kuvipeleka Serikali Kuu na kuibakizia majukumu

Serikali Kuu kuanza kuzihudumia Halmashauri kwa kila jambo hata mambo ambayo Halmashauri ingeweza kufanya peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa matokeo yake ni haya kwamba fedha zinakusanywa na Serikali Kuu lakini kupelekwa kwenye Halmashauri kwa wakati imekuwa ni vigumu. Kwa hiyo, Halmashauri zina-*paralyze*, zinashindwa kufanya kazi zake vizuri na kulingana na ripoti ya *CAG* miradi mingi sasa ya Halmashauri inashindwa kukamilika kwa wakati na inaonekana kama miradi ile watu wamekula fedha na kuna hujuma ambazo zimefanyika wakati kosa ni la kuchelewa kupeleka fedha kwa wakati na miradi mingi inabaki kuwa sasa ni magofu ambayo yanahitaji kushughulikiwa kwa haraka na fedha hazipo kwa hiyo hawashughulikii kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niishauri Serikali kwamba ni vizuri kwanza ipeleke fedha hizi ambazo zinahitajika kupelekwa kwenye Halmashauri kwa wakati na ni vizuri wawe na utaratibu wa kuingia mkataba wa Halmashauri kwamba kama Halmashauri bajeti yake ni shilingi bilioni mbili na fedha za kutoka Serikali Kuu ni shilingi bilioni moja basi waonyeshe namna gani watahakikisha zile fedha zinaenda katika muda ambao umeupanga kama ilivyokuwa imependekezwa kwenye *policy* ile ya *reform* ya *decentralization.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili ni lazima sasa waone ni namna gani wanaisukuma sera ya ugatuaji wa madaraka ili itengenezewe sera itakayoweza kuhakikisha kwamba ile tuna-*adopt* ile sera kama njia mojawapo ya kutusaidia kuzifanya Halmashauri zijitegemee kwa kiwango cha kutosha zipunguze utegemezi wa Serikali Kuu ili Halmashauri ziweze kuendesha miradi yako. Hiyo ni *solution* muhimu sana ambayo waliyoifikiri ambayo ni Serikali ya CCM iliyofikiri miaka ya 1995 mpaka 1998 mpaka 2000 walifikiri kwa sababu waliona kuna hiyo haya na kutokana na *record* za huko nyuma, kwa hiyo, ni vizuri na Serikali hii ya Awamu ya Tano na itakayokuja baada ya hii mfikiri kwa upana ni kwa

namna gani mnazipa uwezo na nguvu Halmashauri zetu ziweze kujitegemea zaidi kuliko kuendelea kila siku kupiga magoti Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la upungufu wa watumishi wenye weledi katika Halmashauri zetu. Kwanza kuna upungufu wa watumishi lakini hata watumishi wenye weledi wataalamu kwenye Halmashauri zetu ni tatizo kubwa sana ni jambo ambalo limepunguza sana ubunifu wa watumishi wetu kwenye Halmashauri, ubunifu ni mdogo, fursa za kuibua miradi mingine ni midogo, fursa ya kuinua vyanzo vya mapato ni mdogo, lakini *the reason behind* ni pamoja na namna ya ajira zinazofanyika katika Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba ikiwa nafasi ya Ukurugenzi ni ya uteuzi lakini ilipaswa iangalie sana uwezo mzuri na uzoefu wa Wakurugenzi wanaoteuliwa kuliko kuangalia haiba nasaba katika kuteuana jambo hili limezidi kuziumiza na kuziangamiza Halmashauri. Nadhani ni vizuri sana Serikali Kuu ifanyie kazi haya maoni ya *CAG* na kwa ujumla wake naunga hoja ya mkono ya maoni ya Kamati ya *LAAC,* ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mheshimiwa Hasna Mwilima ajiandae.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa hii na ninakupongeza sana kwa namna ambavyo unaendesha majadiliano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niungane na wengine katika kushukuru Kamati ya *LAAC* pamoja na *CAG* kwa kazi nzuri waliofanya ambayo matokeo yake ni Halmashauri nyingi kupata hati safi na Halmashauri zile ambazo zilikuwa zinapata hati chafu kuachana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo mengi ya Tanzania yanatokana na Halmashauri kwa sababu watu wote wako kule, kwa hiyo, usimamizi mzuri wa fedha za

Halmashauri ndiyo ambao utaleta maendeleo mazuri kwa nchi hii kwa hiyo naipongeza sana Kamati hii pamoja na *CAG.* Ninaomba sana tuendelee kuzisimamia Halmashauri ili ziweze kutumia fedha zao vizuri, kimoja kilisema kwamba makusanyo ya mapato yaangaliwe, haitoshi tu kuangalia fedha ambazo zimefika Halmashauri kutumika vizuri. Lakini mapato nayo inavyopatikana kama kweli yanaleta yote Halmashauri yaangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo limenisimamisha hapa niipongeze *LAAC* kwa sababu kwa kweli mapendekezo ya mikopo ya kina mama, vijana na walemavu kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa za mwaka 1982 imesaidia sana sana kina mama, vijana na walemavu kupata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nikuambie Wilaya ya Hanang mwaka 2016/2017 ilitowa shilingi milioni 20, mwaka uliofuata ilitoa shilingi milioni 103, mwaka 2018/2019 ilitoa mkopo shilingi milioni 234.5 na mpaka sasa hapa tulipo imeshakusanya imetoa mikopo ya shilingi milioni 192 na bado muda nina hakika itakuwa zaidi.

Mhshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mtaona kwamba sheria hii kurekebishwa imeleta... na mimi nakumbuka nilikuwa nikigombana na Halmashauri yangu kwamba watoe mikopo hiyo mpaka siku moja wakamshawishi Mkuu wa Wilaya kutaka kuniweka ndani Rais wangu akanisaidia namshukuru na Mungu ampe afya njema kuweza kuona kwamba mambo mengine ambayo hayafai hayafanyiki, lakini nataka niwaambie kwamba jamani tukazane na wanawake kwa sababu ndiyo watakao leta maendeleo hawajui kwenda kilabuni kwenda kunywa pombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua vijana wanataka kujitegemea kwa hiyo wakipata mikopo na wakasimamiwa vizuri wataleta maendeleo ya Watanzania na walemavu wetu wanandugu ambao ni maskini kwa hiyo tukiwapa mikopo hii na kwamba mikopo haina riba hilo ndiyo jambo ambalo siyo la kawaida na tuishukuru Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulisema ni ya posho ya Madiwani na watumishi wa Halmashauri, jamani Madiwani wanapata fedha kidogo na hizo ambazo zilikuwa zimepangwa baadaye zikarekebishwa muangalie kama ni haki ili marekebisho yale yaliyofanywa kama siyo ya haki sana warudishiwe fedha hizo na waweze kumaliza kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kurekebisha ngazi za watumishi na wao wenyewe hawajawahi kuomba wawe sehemu fulani au ngazi fulani, lakini baadaye bila maelezo wanajikuta kwamba wamerudishwa chini na Serikali inapaswa kuwaeleza wajue ili wasiwe na malalamiko ni jambo ambalo linaumiza kama maisha ya mtu yaliwekwa inavyotakiwa halafu unateremsha mshahara wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba muangalie kama wanastahili kubaki pale au wanastahili kurudisha chini, chini basi kwa ngazi waweze kusaidiwa ama maisha yatakuwa *very uncomfortable* na Mungu ataisaidia Halmashauri ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Waziri aweze kuangalia hilo wanaotakiwa kurudi chini sawa, lakini wale ambao hawastahili kurudishwa chini labda umerudishwa kwa hila basi wasaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana nilitaka kuyasema haya ambayo kwa kweli *LAAC* na *CAG* wamesaidia sana kuifanya Halmashauri zifanye kazi vizuri ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Shukrani sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mheshimiwa Profesa Jumanne Kishimba ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu.

Awali ya yote nichukue nafasi hii inawezekana ikawa ni mara yangu ya mwisho kuchangia kwenye Bunge hili. Niwashukuru sana wapiga kura wangu Wana Liwale wote kwa ujumla, mimi nikiwa kama Mbunge niliyechaguliwa na vyama vyote vya upinzani na chama tawala nawashukuruni sana. Lakini naendelea kuwasisitiza Mwenyezi Mungu akijalia bado nia ninayo, uwezo ninao, kama chama kitanipa ridhaa basi naomba mniunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo naomba nijielekeze kwenye hotuba hii, kwanza kabisa kuunga mkono mapendekezo yote ya Kamati ya *LAAC,* lakini vilevile napenda kumpongeza sana Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG)* kwa namna anavyotusaidia sisi Wabunge kutupa mwanga wa nini kuishauri Serikali. Naomba mchango wangu pamoja na kupongeza au kuongezea kidogo yale yaliyotajwa na kwenye Kamati, mimi naomba nichangie hasa kwenye upande wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yuko Afisa Masuuli wa Halmashauri yetu ambaye ni Mkurugenzi, lakini Mkurugenzi huyu anasaidiwa kwa karibu sana na watendaji. Mtendaji Mkuu hasa nikizungumzia sehemu ya uhasibu, yuko Mhasibu, Afisa Mipango na Afisa Manunuzi. Lakini hapa mchango wangu ni kwamba mimi naiomba Serikali hebu jaribu kuangalia namna ya watumishi hawa wanavyodumu kwenye Halmashauri zetu. Unakuta kwenye Halmashauri Mtendaji Mkuu ambaye ni Afisa Masuuli/Mkurugenzi ana miaka mitatu, miaka minne anahamishwa anakuja mwingine, lakini Mhasibu, Afisa Manunuzi au Afisa Mipango wamekaa kwenye Halmashauri hiyo miaka 10. Hii inapunguza sana utendaji kazi wa huyu Afisa Masuuli kwa sababu anakuta hawa watumishi wengine kwenye Halmashauri wemekaa muda mrefu sana, wanajifanya wenyeji, yeye kila anachowashauri wanaona kuwa yeye mgeni. Kwa hiyo, mimi nawaomba sana hasa wahasibu, wasikae kwenye Halmashauri kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nakumbuka miradi hasa miradi ya majengo, shule na hata kwenye Idara

ya maji sasa hivi tunaenda kwenye haya mambo ya matumizi ya *Force Account.* Lakini miradi mingi ya ujenzi inapatwa na matatizo kwa sababu ya kukosa wahandisi kwenye Halmashauri zetu. Kama mnakumbuka wahandisi wengi walishakwenda *TARURA,* lakini hakuna *replacement* iliyofanywa kwenye Halmashauri nyingi ili waweze kusimamia hayo majengo. Matokeo yake ni kwamba majengo mengi kwanza yanajengwa chini ya kiwango, lakini vilevile yanachelewa kwa muda mrefu, majengo yetu mengi yanachukua muda mrefu kukamilika ni kwa sababu kukosa utaalamu.

Kwa hiyo, naomba kuishauri Serikali kwamba ione umuhimu wa kuleta wahandisi wenye sifa kwenye Halmashauri zetu ili fedha zinazopelekwa kwenye miradi hii iweze kusimamiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine Sheria ya Manunuzi; Sheria ya Manunuzi mimi naomba Serikali hii waifanyie mapitio. Miradi mingi hasa hii ya *Force Account* inakwama sana kwenye Afisa Manunuzi, *procedures* zetu kwenye manunuzi zimekuwa na mchango mkubwa sana kuchelewa hasa kwa kukamilika kwa miradi mbalimbali ya kwenye Halmashauri zetu. Kwa hiyo, naiomba Serikali kuangalia upya kwenye hii Sheria ya Manunuzi, ni sheria ambayo inatuchelewesha sana, ni sheria ambayo inaleta urasimu mkubwa hasa kwenye hii Sheria ya Manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo ambayo niliona niyachangie kwenye kuboresha hii hotuba au taarifa ya kamati yetu. Kwa hiyo baada ya kuyasema hayo mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii dakika tano na nimeweza kuchangia hotuba hii na nimeunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, kwa hayo, machache naunga mkono hoja mia kwa mia, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hasna Mwilima atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Jumanne Kishimba, Mheshimiwa Ikupa Stella Alex ajiandae.

**MHE. HASNA S. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi nianze kwa kumpongeza *CAG* kwa taarifa yake hii iliyowasilishwa juzi, lakini pia kupongeza Kamati ya *LAAC* kwa kuwasilisha taarifa njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,mimi ninao kama ushauri tu kwenye maeneo machache, la kwanza ni hili suala la Waheshimiwa Madiwani ambapo tumeona Madiwani wengi kwenye Halmashauri nyingi nchini wamekuwa wanafanyishwa Vikao vya Kikatiba na Kikanuni lakini bila kulipwa posho zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala linatokana na ukosefu wa makusanyo mapato ya Halmashauri kushuka kwenye Halmashauri zetu. Sasa nikadhani kwa uzoefu wangu wa miaka mitano kama mwakilishi huko chini sasa hivi ushirikishwaji wa ukusanyaji wa mapato umekuwa kidogo hauwashirikishi Serikali za vijiji. Huko nyuma Serikali za Vijiji zilikuwa zinashiriki asilimia 100 kuhakikisha kwamba makusanyo yale yanayokusanywa chini na wao wanakuwa ni sehemu kusimamia yale makusanyo na baadae asilimia 10 ya makusanyo yale yaliyokusanywa ndani ya kijiji husika huwa inabadi kwenye kijiji na asilimia 90 inakwenda kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilifikiri kwa vile mwakilishi wa Wizara ya TAMISEMI yuko hapa mngejaribu kuangalia ile *D by D* sasa hivi inafanya kazi kwa kiasi gani. Ni kweli kwamba hizi Serikali za Vijiji wanashirikishwa? Hawashirikishwi kwenye miradi, hawashirikishwi kwenye makusanyo, kwa hiyo inawapelekea ugumu Wakurugenzi kupata asilimia kubwa ya makusanyo katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona malalamiko ni mengi kwenye upande wa miradi, kwamba kuna miradi ambayo haikidhi thamani ile *value for money.* Lakini sote

tunafahamu kwamba tunayo ile Sheria ya *Local Government,* ile Sheria ya mwaka 1997 Sheria Na. 4 kama sikukosea Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI yuko hapa ataniongoza, ile Sheria Na. 4 inamtaka Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya waweze kuzisimamia Halmashauri katika ufanisi wao wa kazi. Tumeona sasa hivi katika hiki kipindi cha miaka mitano Wakurugenzi wanafanya kivyao, ma-*DC* wanafanya kivyao, Ofisi za *RAS* zinafanya kivyao. Hata ule utaratibu wa huko nyuma ambao *RS* walikuwa wanaweza kutembelea Halmashauri kwa Halmashauri, kutembelea miradi, kutembelea kujua Halmashauri zinafanya kazi gani, kwa kufanisi upi sasa hivi hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika,kwa hiyo mimi nilitaka niishauri Wizara ya TAMISEMI, hebu turudishe yale Mamlaka ya Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa watambue mamlaka zao ni nini, waweze kuwa anazisimamia Halmashauri. Kwa sababu Wakurugenzi wengi walioteuliwa sasa hivi hawakupita kwenye mfumo wa Serikali, kwa hiyo unakuta labda Mkurugenzi ametoka kwenye *private organization,* hajui namna gani anaiendesha Halmashauri. Kwa hiyo anatakiwa aweze kupata watu wa kumsimamia na kumuongoza.

Kwa hiyo, tunaweza tuka-*blame* sana hapa nimeona kwamba kuna Halmashauri ambazo hazitumii zile mashine za *POS* kwa hiyo mapato yanakuwa hayaendi Serikalini ni kwa sababu ya uelewa. Kila mmoja yule uliyemtoa kwenye *Local Government* au umemtoa kwenye *civil servant* anakuwa anaelewa kwamba mimi kazi yangu kama Afisa Masuuli natakiwa kufanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikawa pia nafikiria wengi wamejadiliana hapa, tumetoa ushauri, tumesoma mapendekezo. Hivi *way forward* sisi kama Bunge ni nini, hili Bunge mwisho kabisa tunatoka na maazimio kwamba Azimio la Bunge kuhusiana na masuala ya *LAAC* mapendekezo ya Kamati ya *LAAC* ni hili. Lakini nani anayesimamia Maazimio ya Bunge?

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nataka nitoe ushauri, kuna maazimio mengi tunayaazimia hapa Bungeni, tukishaazimia tunategemea kwamba Serikali itafanyia kazi. Matokeo yake tunakwenda tena mwaka unaisha, Serikali hawajafanyia kazi na hakuna mtu wa kuhoji hivi lile Azimio la Bunge labda la Kumi na Tisa limefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nilitaka nitoe ushauri kwamba kwenye ile Taarifa ya *PAC,* Taarifa ya *LAAC* hebu sasa Bunge tuangalie kwa mapana ikiwezekana kwa sababu kuna mabadiliko ya kanuni hebu tuone tuwe na Kamati mojawapo ya Bunge itakayokuwa inafuatilia maazimio yote ambayo yameazimiwa hapa Bungeni ili kufuatilia kwenye Serikali. Hivi azimio fulani tulilolitoa pale Bungeni limetekelezwa kwa ufanisi upi? Tukifanya hivyo Maazimio ya Bunge yanaweza yakawa yanafanyiwa kazi, badala yake hapa tutaishia tu kumpongeza *CAG. CAG* taarifa yake nzuri, *CAG* amefanya ukaguzi vizuri, *CAG* amefanya hivi lakini mwishoni azimio litatoka hapa, tunakwenda kwenye uchaguzi wale watakajaliwa kurudi najua na mimi *Inshallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitakuwa miongoni tutakuja kukuta yale maazimio pengine hayajafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa mimi niseme tu tunaweza tukawalaumu sana Wakurugenzi hapa, lakini nishauri watakapoteuliwa tena Wakurugenzi baada ya Uchaguzi Mkuu hebu wawe wanapata semina ikiwezekana hata ya mwezi mzima, wawe wanajua majukumu yao ni nini katika utekelezaji kwenye *Local Government.* Mnawaita siku mbili, siku tatu mnasema semina elekezi, semina elekezi mtu alikuwa mfanyabiashara amepewa Ukurugenzi hiyo semina elekezi ya siku tatu atajua mfumo mzima wa Serikali unavyokwenda. Kwa hiyo mimi nadhani tusiwalaumu sana, lakini tujipange ni namna gani tutawajengea tena uwezo Wakurugenzi ili waweze kuzisimamia hizi *Local Government.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya mimi nashukuru sana naendelea kumpongeza *CAG* na

Kamati zote mbili. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Profesa Jumanne Kishimba atafatiwa na Mheshimiwa Ikupa Stella Alex, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa ajiandae.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwanza nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye mjadala huu wa *LAAC.* Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuonesha uongozi imara na ushujaa wa hali ya juu sana wakati huu wa ugonjwa wa Corona na mtiririko wa uchumi na kuporomoka kwa uchumi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kahama Mjini kwa kuniazima kura zao kwa miaka mitano na mimi nimejitahidi kwa kadri ya uwezo wangu na Serikali ya Chama cha Mapinduzi wajibu na kutimiza kile tulichoahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeisoma vizuri ripoti nzima ya Kamati ya *LAAC* na nimefuatilia michango mingi sana ya Waheshimiwa Wabunge, ya *CAG* alivyoeleza na mapendekezo yake. Lakini tatizo kubwa sana ninaliona hapa ni suala la wizi na ukiangalia kesi zilivyo sasa hivi ni nyingi sana za wizi kwenye Mashirika ya Umma na kwenye Halmashauri zetu na hata ukifatilia ziara ya Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Mawaziri asilimia kubwa wanalalamikia wizi kila mahali. Hata juzi hapa bahati nzuri Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho kinafundisha wahasibu na chenyewe kimeibiwa hata Bodi ya Uhasibu na yenyewe imeibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* na Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko hapa, hawa vijana wanaoajiriwa kwanza lazima anatoka shule kwenye shule ambayo inafundisha maadili mema, inafundisha uwe mwaminifu na *file* lako likienda lazima usiwe na doa. Sasa wanaenda kupambana

na wizi, wengine wamesoma seminari, kwa nini Serikali haifikirii sasa kuanzisha chuo cha wizi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yangu anapochaguliwa mtu kwa sifa ya uaminifu kwenda kupambana na wezi anaenda kupambana nao namna gani afadhali apite kwenye chuo hicho kwa miezi mitatu ajue *brain* ya wizi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wanafundishwa bunduki lakini hawajawi kuwa majambazi, Wanajeshi wanafundishwa mpaka mabomu hawajawahi kusikia wameteka, lakini hawa vijana wetu tutawamalizia gerezani, hali ya wizi ni mbaya sana. Hata sisi kwenye taasisi binafsi hali ya wizi ni mbaya sana, tungeomba sana najua ni suala gumu sana na ni geni, lakini tutafanya namna gani mtu hajui wizi na *file* la ajira linataka uwe mwaminifu, mwadilifu unatoka *Mzumbe University* unaenda kupewa *National Housing* lile dude kubwa kama lile hujui chochote.

Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na *CAG* mnaweza mkatafuta jina lingine kama kulitamka jina kwamba ni chuo cha wizi mnaweza mkafikiria jina lingine lakini kuna haja ya msingi sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tufikirie sana kuna hii sheria yetu ya Sheria ya Manunuzi, ni kwa nini *tender* isiwe wazi. Nchi nyingi sasa hivi duniani zimeanza *tender* kuwa wazi kama wewe unajenga hospitali unawaruhusu watu wote wanaleta *tender* kila mtu anasoma ya mwenzie na huyu anasoma ya mwenzie kitakachotokea hata kama wewe ulipanga shilingi milioni 200 wale wanaweza wakafika shilingi milioni 100. Kwa hiyo, Serikali itakuwa ndio mnufaika mkubwa zaidi, kuliko sasa hivi wewe unajifungia unasema walete watu *tender,* wewe unasema una 200 na siri zikivuja mle ndani wale wanao-*tender* wataishia pale pale ulipoishia wewe, lakini kama itakuwa wazi Sheria ya Manunuzi itatusaidia sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kumalizia tu ni suala la *consultant.* Mimi ukinipa ushauri wa hili jengo siwezi

kulipunguza sana nitaongeza kwa sababu mimi nalipwa asilimia kumi ya gharama, kwa nini sheria isibadilike yeye alipwe *percent* ya ku-*save* au *percent* ya faida kama shughuli ile ni ya kibiashara. Unapompa ushauri au *consultant percent 10* ya mradi ataongeza vitu vingi mno ili *percent 10* yake ipatikane. *(Makofi)*

Tunaomba sana wenzetu wa *CAG* na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ingawa muda wetu wa kurudi kwenye kura unakaribia kama tutakaporudi ni sheria ambayo inaweza ikatusaidia sana kupunguza huu mgogoro, suala la wizi kweli ni kubwa sana sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata mimi nina wasiwasi humu ndani *CAG* hajaona wizi mwingine, kuna miradi mingine haina faida yoyote lakini imependekezwa, lakini kilichojengwa ni sawa, lakini mradi ule una faida au una sababu? Ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo naunga mkono hoja, nawapa pongezi Kamati, asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mtagundua kwa nini ametunukiwa cheo cha kuwa Profesa, kila wakati lazima aje na jambo jipya.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunawapongeza sana kwa uongozi wenu uliotukuka kwetu, wewe na Spika, Mola awapatie wepesi na mafanikio mema kwa haja zenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokurejeshewa gharama za matibabu kutoka *NHIF* kwa Halmashauri zetu kunasababisha migogoro na kutokuwa na imani na madaktari wao na kulalamikia Serikali kuhusu na upungufu wa dawa, na wakati bajeti ya afya ni kubwa na ina mwelekeo wa kutatua tatizo la upungufu wa dawa.

Pia kutokuwa na mapato hayo kunasababisha sasa ubora wa huduma za matibabu kwa wananchi wetu na hata upotevu wa mapato hapa ndipo upendo mpya wa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba mrejesho huu kufanyiwa kazi haraka, kufanikisha marejesho kwa Halmashauri zetu ili huduma zifanyike na zenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana kwa TAMISEMI kuona na wajipange kuwatendea haki Madiwani kwa hatima ya haki zao katika ukamilifu wake. Kwani ifahamike kuwa Madiwani hawa wamefanya vikao vyao kikamilifu na baadhi ya vikao wamekopeshwa yaani wamefanya bila malipo, walichukua mikopo kadhaa kwenye vyombo vya fedha kwa kutegemea kurejesha kupitia posho zao na ambazo hawazipati kwa wakati. Hakika Madiwani wenzetu hatima yao iangaliwe kwa jicho la aina yake, kwani tarehe 10 Juni,2020 wanavunja Mabaraza yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilishindikana kwa TAMISEMI basi Serikali Kuu kuingilia kati ili hawa Madiwani kwa kazi kubwa waliofanya, wasisononeke na kutupatia athari kwenye Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani walipwe pesa wanazodai kabla ya Mabaraza kuvunjwa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipeleke fedha kwenye Halmashauri ili ziweze kujiendesha. Miradi mingi haitekelezeki sababu ya ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, *force account* imefeli kwani asilimia kubwa ya majengo yaliyojengwa katika kipindi hiki

cha miaka minne yameonekana kuwa chini ya kiwango na yana nyufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipandishe mishahara kwa watumishi hasa walimu kwa sababu hili ni takwa la kisheria na si hiyari.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* itekeleze miradi ya kutengeneza barabara kwa kuzingatia vipaumbele vya Halmashauri badala ya kupanga peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya wastaafu si hiyari, ile ni pesa inayowafanya waendelee kuishi vizuri baada ya utumishi wake uliotukuka. Wapelekewe pesa zao kwa wakati na hii iende sambamba na kuwaongezea kiwango cha malipo kwa mwezi kwa kuzingatia gharama halisi ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa walipwe mishahara kama ilivyo kwa Wabunge, hawa ni wawakilishi wa wananchi na wanafanya kazi katika mazingira magumu usiku na mchana.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza *CAG* kwa kazi nzuri anayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupata maendeleo makubwa yanayotarajiwa inabidi Halmashauri zikusanye fedha nyingi za kutosha na asilimia kubwa ya fedha za ndani za Halmashauri zielekezwe kwenye miradi ya maendeleo. Makusanyo kwenye Halmashauri hayaongezeki inavyokusudiwa sababu bado wanaendelea kutumia vyanzo hivyo hivyo. Napendekeza wataalam kwenye Halmashauri wafanye kazi ya kuibua vyanzo vipya vya mapato kwenye Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani wanafanya kazi kubwa katika uibuaji wa miradi kule chini kwenye vijiji na kusimamia utekelezaji wa Ilani. Bahati mbaya malipo ya Madiwani ni madogo na Halmashauri nyingine hadi leo zimeshindwa kulipa posho hizo na pia zimeshindwa

kuwasilisha makato mbalimbali kunakohusika kama benki, bima na kadhalika. Napendekeza posho stahiki za Madiwani ziwe zinalipwa kila mwezi tena kwa wakati na naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwaongeza posho au mshahara Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri na maendeleo; kumekuwa na kutopeleka pesa ya maendeleo kwa wakati na kusababisha ukosefu wa maendeleo katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za mikopo ya 10% ya maendeleo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; vikundi vingi havipati mikopo na hasa idadi ndogo ya wafanyakazi katika Halmashauri nyingi hivyo tunaomba ajira ya wafanyakazi hawa ili kurahisisha maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Madiwani Halmashauri nyingi hazipeleki madeni ya Madiwani kwenye mabenki hasa pesa ya mikopo na malimbikizo hayo kuwapatia madiwani hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba mwaka ujao Halmashauri ziachiwe mapato ili kurahisisha maendeleo ya majimbo na mikoa, baadhi ya vyanzo vya mapato ikiwepo *property tax* zibake Halmashauri.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kukiukwa kwa Sheria za Fedha na Manunuzi ya Umma hapa changamoto ni kubwa kwa baadhi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria, kanuni na taratibu za manunuzi ya umma vipo kwa ajili ya kuhakikisha kuwa manunuzi hayo yanakuwa na tija kwa nchi. *LAAC* imebaini kuwa baadhi ya Halmashauri zinakiuka miongozo hiyo. Kutokana na ukiukwaji huo, hivyo Taarifa ya *CAG* kwa mwaka 2018/2019 inaonesha kuwa jumla ya shilingi bilioni 9.2 zilitumika kufanya manunuzi ya huduma na bidhaa

mbalimbali bila idhini ya Bodi ya Zabuni katika Halmashauri zetu, ni rai yangu Serikali kusimamia changamoto hii.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika hoja hii kama ifuatavyo; nianze na Madiwani waongezewe posho maana muda mwingi wanawahudumia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Manunuzi irekebishwe maana sheria hii imekuwa ikikwamisha miradi mbalimbali wakati mfumo wa *force account* inafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *D by D* kwenye Halmashauri zetu halifanyi kazi maana miradi mingi sasa hivi inasimamiwa na Serikali Kuu. Naomba kuishauri Serikali kuona ni namna gani kuhakikisha *D by D* inafanya kazi. Naomba kuwasilisha.

**MHE. ESTHER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mawazo yangu katika hoja iliyoko mbele yetu.

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa utendaji wake uliotukuka kwa kuwezesha miradi mingi kutekelezwa katika Halmashauri mbalimbali nchini. Pongezi hizi pia zimfikie *CAG* pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na maoni yangu, makusanyo yote yakusanywe kwa njia ya kielektroniki ili kuepuka upotevu wa fedha za umma. Fedha za ukamilishaji wa miradi zipelekwe kwenye Halmashauri kwa muda muafaka kwani miradi hii yote ni ile inayogusa maisha ya wananchi siku kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, maazimio ya Kibunge dhidi ya taarifa ya *LAAC* yatafutiwe namna nzuri ya ufuatiliaji kama kweli yanatekelezwa kama yalivyoazimiwa.

Pia, wakandarasi wengi wamekwama kuendelea na kazi kwani madai yao kuchukua muda mrefu bila

kushughulikiwa. Hii inapelekea wakandarasi hawa kuuziwa dhamana walizokopea benki ili kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zipelekwe kwa uwiano unaolingana badala ya hali ilivyo sasa ya Halmashauri zingine kupelekewa kiasi kikubwa kuliko mahitaji yao na wengine kupokea chini ya kiasi walichoidhinishiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya awamu ya tano imefanya kazi kubwa sana ikiwemo miradi mikubwa ambayo ikikamilika italeta tija kwenye maendeleo ya nchi yetu na kupeleka nchi yetu kwenye uchumi wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na kukupongeza wewe mwenyewe pamoja na Mheshimiwa Spika pamoja na Wenyeviti wetu wote wa Bunge kwa jinsi mlivyoendesha Bunge letu kwa miaka mitano. Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naomba kuunga hoja mkono.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote kwa miaka yetu hii mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nzima ya Awamu ya Tano kwa utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2015 - 2020. Nawaomba Watanzania wote kuendelea kuiombea nchi kwa Mungu kutuepusha na majanga mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu kupitia hoja hii ya taarifa ya *CAG* kupitia taarifa ya Kamati ya *LAAC*; kwanza Serikali itazame kwa upana wake suala la baadhi ya Halmashauri kutokutumia mashine za *EFD* hadi sasa, hali hii inasababisha sana

udanganyifu mkubwa, hivyo basi Serikali iagize kila Halmashauri kutokutumia vitabu vya risiti ifikapo tarehe 30 Juni, 2020.

Pili, kwa kuwa sababu za baadhi ya Halmashauri kutumia vitabu hadi sasa ni mpango wa baadhi ya maafisa na viongozi wa Halmashauri kuwa na ubia na maslahi kwenye vyanzo vya mapato ya ndani vya kila Halmashauri kupitia mawakala wanaokusanya ushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kwa kuwa kila Uchaguzi Mkuu unapofanyika Madiwani wengi wanaochaguliwa ni wapya, ni vema basi Serikali ikaandaa mafunzo ya majukumu, taratibu, usimamizi, Sheria za Serikali za Mitaa kwa Waheshimiwa Madiwani mara baada ya uchaguzi ili kuleta ufanisi zaidi.

Nne, kwa kuwa kilio cha posho kwa Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa ni ya muda mrefu na kwa kuwa uwezo wa baadhi ya Halmashauri kutoa posho kwa kada hizo kwa vyanzo vyake vya ndani ni ngumu, hivyo basi Serikali ione utaratibu wa kuagiza kutenga 10% ya mapato ya ndani ya kila Halmashauri na kuziwasilisha TAMISEMI hatimaye kutolewa na Hazina kila mwezi.

Kuhusu upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali na kwa kuwa hatuwezi kuwaajiri kwa mara moja Serikali ifanye mapitio ya watumishi waliopo ili kubaini maeneo ambayo yana upungufu mkubwa sana na maeneo ambayo watumishi wako wengi huku tukiendelea kuajiri zile kada muhimu kulingana na uwezo wa Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Bima ya Afya *(NHIF)* kusainisha wagonjwa fomu ambayo haioneshi uhalisia wa gharama ya matibabu wakati wa ujazaji mfano, miwani ambayo dukani hupatikana kwa shilingi 120,000 kupitia Bima miwani hiyo ni shilingi 600,000; suala hili halina uhalisia kabisa hasa upande wa wananchi hivyo basi Serikali ilitazame upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itazame upya hatua za kuchukua kwa Halmashauri zinazoshindwa kupata hati safi kwa miaka mitatu mfulilizo, kwa kuangalia uwezo wa watendaji waandamizi na kubadilisha baadhi ya watendaji kutokana na sababu mbalimbali ili kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga hoja mkono 100% na naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa Stella Alex atachangia kwa dakika 10 atafatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa dakika tano Mheshimiwa Dkt. Mollel ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE WALEMAVU (MHE. STELLA A. IKUPA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi ya kuweza kuchangia katika hoja hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Ninaomba niweze kuchangia kwa ufupi sana katika eneo la mikopo ambayo inatolewa na Halmashauri zetu. Mikopo hii inayotolewa na Halmashauri zetu kwa kweli imekuwa na mafanikio makubwa sana kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameweza kuchangia na hasa niweze kuzungumzia kwenye eneo la watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Bunge lako tukufu liliweza kupitisha ile sheria ya tengeo la asilimia mbili katika Halmashauri zetu kwa kundi la watu wenye ulemavu tunaona kabisa kwamba eneo hili limekuwa na mafanikio makubwa sambamba na matarajio ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba mikopo hii imewekwa ama imeweza kuridhiwa kutokana na hali ya watu wenye ulemavu ilipokuwa hapo awali. Tunafahamu kabisa kwamba kundi la watu wenye ulemavu lilikuwa linakutana na changamoto nyingi sana kwenye taasisi zetu za fedha, kwa hiyo, watu wengi walikuwa wanashindwa

kukuposheka katika maeneo haya ya taasisi za fedha kulingana na masharti kwamba yalikuwa ni magumu ambayo wao walikuwa hawayawezi. Lakini kupitia uwepo wa mikopo hii Serikali yetu ya Awamu ya Tano inayo mafanikio makubwa sana ambayo inajivunia kupitia uwepo wa mikopo hii. Mheshimiwa Rais wetu mpendwa aliweza kuridhia kabisa kwamba sheria hii iweze kuwepo na Bunge lako tukufu liliweza kuona kwamba kuna umuhimu kabisa wa kuwepo kwa tengeo la asilimia mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ni makubwa, mafanikio ni mengi ya uwepo wa asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu na hata wenyewe wamekuwa ni mashahidi na mashuhuda wakubwa sana wa uwepo wa mikopo hii. Ikumbukwe kwamba mwezi Februari watu wenye ulemavu ndani ya nchi yetu ya Tanzania waliweza kuandaa kongamano kubwa sana mimi mwenyewe nilihudhuria kongamano lile lilijumuisha watu wenye ulemavu kutoka Tanzania nzima, lakini wengi walikuwa ni kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. Waliweza kuishukuru Serikali sana kwa kusema sasa sisi watu wenye ulemavu tumeacha kuwa ombaomba, tumeacha kuwa tegemezi na hatimaye pale kitu ambacho kilifanyika kilikuwa ni kitu kikubwa na cha kufurahisha kwa kuonesha hilo waliweza kuchanga shilingi milioni moja kwamba sasa tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uwepo wa mikopo hii, sasa hivi sisi siyo ombaomba, tunachanga hela ya kuchukua fomu ya kugombea Urais kwa Rais wetu, Mheshimiwa John Pombe Magufuli na fedha hii iliweza kukabidhiwa kwa Katibu Mkuu wa chama ambaye aliwakilishwa na Katibu wa CCM wa Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ambayo imekwishakutolewa mpaka sasa hivi ni ya thamani ya hela nyingi zaidi ya shilingi bilioni 3.9 imekwishakutolewa kwa makundi ya watu wenye ulemavu na wanaendelea kunufaika nayo katika maeneo mbalimbali ambayo mimi nimefanya ziara ndani ya nchi ya Tanzania, nimefanya ziara karibu mikoa yote daima zilikuwa ni salamu za pongezi, salamu za shukrani kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa

Mheshimiwa Rais wetu na kwa viongozi wetu wote kwamba hakika wanaishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa sababu sasa hivi wao siyo ombamba tena siyo tegemezi tena na hatimaye watu wenye ulemavu wamekuwa na matani yao. Mwingine anakwamba mimi sasa hivi bwana hata nikipita barabarani nimependeza, niko *smart* na wadada wananigombea. kwa hiyo wamekuwa wakisema hivyo kwamba kwa kweli hali zao zimekuwa nzuri sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ambalo ninaomba niweze kulizungumza ni kwamba sasa Halmashauri zetu ziendelee kujitahidi kutenga hii asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili sasa zile ndoto za watu wenye ulemavu ziendelee kufikiwa kila iitwapo leo.

Pia niendelee kutoa rai kwa watu wenye ulemavu wenyewe kuendelea kujitokeza kwa kuchangamkia fursa hizi kwa sababu katika maeneo mengi ambayo nimefanya ziara kumekuwa na changamoto kwamba watu wenye ulemavu fedha zinakuwepo lakini wao wenyewe wamekuwa hawajitokezi kuchangamkia fursa hizi. Kwa hiyo nitoe rai sana kwa watu wenye ulemavu kujitokeza kuchangamkia fursa hizi, mifano tunayo waige mifano ya wenzao ambao tayari wamekwishakukopeshwa mpaka bajaji, wengine wamefungua mpaka viwanda, shukrani ni nyingi mno za watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe rai kwa wenzangu wenye ulemavu kwamba kupitia mikopo hii hebu tuoneshe uaminifu, nimekuwa nikisema kwamba ukiaminiwa kwa kidogo hebu aminika. Kundi la watu wenye ulemavu tuonyeshe mfano kwamba tunakopeshwa lakini tunakopesheka kupitia urejeshaji wetu, tuwe mfano katika kurejesha mikopo hii ili sasa na wengine waweze kupatiwa mikopo hii. Wengi wamekuwa wakisema kwamba kwa nini isitolewe kama ruzuku, bado hatujafika huko kwa kutoa mikopo hii kama ruzuku, sasa hivi ni mikopo ambayo inatakiwa irejeshwe kwa sababu kundi la watu wenye ulemavu ni kubwa kwa hiyo unapokopa na kurejesha unatoa fursa kwa wenzako kuweza kukopa mikopo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache ninaomba niendelee kuunga mkono hoja hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkta Mary Mwanjelwa atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mollel, Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia kwa ufupi hoja hii ya Taarifa ya *CAG,* lakini kipekee naomba nimshukuru sana Mungu kwa kutupatia Rais bora duniani ambaye ni mbeba maono na hakuna mwingine zaidi ya Dkt. John Pombe Magufuli na dunia nzima hiyo inakiri hata ardhi ukipita inakiri kwamba hakika huyu ndiye mbeba maono wa Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Vilevile kupitia janga hili la *Covid-19* nchi yetu na Serikali imekuwa ya mfano. Kwa nini ninasema hivyo hakuna mtumishi wa umma yeyote ambaye hajawahi kulipwa mshahara tena kulipwa mshahara kwa wakati na watumishi wa umma wote wamekuwa wakifanya kazi 24/7 wakitoa huduma kwa wananchi. Kwenye hili nichukue nafasi hii kuwapongeza watumishi wa umma wote nchini ambao wamekuwa wakitoa huduma zao bila kuchoka na wamekuwa wakilipwa mishahara bila kukosa na stahiki zao zingine zozote ambazo zinastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Waheshimiwa Wabunge hapa wamezungumza baadhi ya hoja na mimi naomba nitoe *clarification* moja kwa ufupi. Ni kweli kwamba huko nyuma kulikuwa na watumishi hewa, lakini Serikali ya Awamu ya Tano ya Dkt. John Pombe Magufuli Serikali iliyojaa uaminifu naomba niliambie Bunge lako tukufu mpaka sasa hivi tumeshafanya *data cleaning* zaidi ya asilimia 94.7 na tunaelewa *data cleaning* ni zoezi ambalo lilichukua pesa nyingi na kweli huko nyuma unakuta huko nyuma unakuta

mtumishi mmoja anaweza akalipwa mishahara zaidi ya watu tisa au 10 wengine unakuta walishatangulia mbele za haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba niliambie Bunge lako tukufu kwamba uwezekano wa kuajiri watumishi hewa kwenye Serikali ya Awamu ya Tano haupo, kwa sababu hii Serikali imejipanga kikamilifu na imejaa utawala bora, uadilifu na uwazi kwa sababu tumeanzisha Sekretarieti ya Ajira. Sekretarieti ya Ajira tumeanzisha kutumia *Ajira Portal* ambayo ni mtandao, uko kwa uwazi na una uadilifu na tunafanya kwa ushirikishwaji na zile taasisi nyingine zote kwamba kupitia huko watumishi wote ajira mpya zote zitakuwa zinapitia kupitia Sekretarieti yetu ya Ajira na kila mwaka huwa tunaajiri kulingana na ikama na mahitaji ya waajiri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa nataka nifanye ufafanuzi huo nimeona Mheshimiwa Yosepher na Mheshimiwa Haonga wanazungumzia masuala ya watumishi hewa, hakuna watumishi hewa kwenye Serikali iliyojaa uadilifu ya Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa ufupi kabisa nikushukuru tena, ahsante kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii ya msingi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mollel atafatiwa na Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula, Mheshimiwa Kwandikwa ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kusema machache, lakini nianze kwa kutoa shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uteuzi na heshima aliyonipa na watu wa Siha kikubwa ambacho mimi naenda kumwambia tutaenda kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa na kuhakikisha matumaini yaliyowekwa kwake na watu watanzania yanaenda kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwashukuru wananchi wa Siha ambao kwa nyakati zote wameniamini na imani niliyopewa na nchi yangu ni imani iliyotolewa kwao na imani hiyo nitaenda kuitunza kwa niaba yao na sitawaaibisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikushukuru wewe pamoja na Spika, Wabunge wenzangu wote mmetulea tumekuwa pamoja niwashukuru sana na tuko pamoja tunaenda mwisho na naamini tutarudi pamoja hapa tuendelee kupambana kujenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme Mheshimiwa Rais wetu amekuwa kinara duniani kwa kupambana na suala zima la *Covid-19.* Kuna maeneo duniani ambayo walikuwa hawaijui Tanzania, lakini leo wanaijua Tanzania kupitia uwezo wa Rais wetu kufanya maamuzi sahihi wakati sahihi ambayo maamuzi hayo ndio yamekuwa mkombozi wa mwanadamu yeyote duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo duania nzima inaenda kurudi nyuma kufata yale ambayo Rais John Pombe Magufuli amaeyaona miezi mitatu iliyopita sasa dunia ndio inagundua kwamba yeye alikuwa sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna suala la nyungu na mambo mengine lakini watu waelewe kuhusu tiba asilia ni suala la kibibilia ukisoma Ezekiel 47:12 utaona jinsi Mungu alivyomuumba mwanadamu lakini akamkabidhi bustani na akamwambia utakula matunda yake lakini majani yake yatakuwa dawa. *(Makofi)*

Mzee wangu Jafo wa nyungu anatumia majani na nataka kukwambia sio wiki mbili tutakuja na Jafo *part three improved* ambayo ina wazungu na Watanzania wakipiga nyungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Rais huyu hakuona tu mbali kwenye suala zima la *Covid-19* mwanzoni kabisa alipoapishwa alisema Watanzania wote tutatibiwa hapa

hapa Tanzania na alifanya hivyo ili iwezekane tuliweka teknolojia kubwa ndani ya Tanzania *operation* za moyo ambazo zilikuwa hazifanyiki zimekuwa zinafanyika, *operation* za ubongo hata bila kupasua zinafanyika; *operation* ya kupandikiza figo inafanyika sasa hivi Tanzania na ilikuwa haifanyiki na inafanyika tena Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake nini, ingekuwa hizo teknolojia zote hazikununuliwa mwaka 2016, 2017, 2019 dunia ingefungwa sasa kama ilivyofungwa na *Covid,* wagonjwa wote waliokuwa wanaenda nje wangetibiwa na nini wakati huu ambao dunia nzima imefungwa. Hayo ni maono makubwa ambayo Rais aliyafanya hata kabla ya *Covid-19* kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikubwa sisi mbeba maono huyu anaenda kurudi kwa asilimia 100 mwaka 2020 akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu Watanzania wamegundua anabeba maono ya nchi yetu kwa miaka 200 ijayo. Tunakwenda kumtumia kwa miaka mitano ijayo ili kuhakikisha tunakwenda kuitengeneza Tanzania salama na ambayo itakwenda kuishi na kuheshimika duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yamezungumziwa mambo mawili; imezungumziwa *MSD* pamoja na Bima ya Afya. Yamezungumzwa mambo *genuine* ambayo *CAG* ameyaona na ni *CAG* ambaye wakati anaingia baadhi ya watu walifikiri ni wa mchezo mchezo. Leo imethibitika kwamba ni mbeba maono wa kuangalia mafisadi na inawezekana amepitia chuo anachopendekeza mwenzetu cha kuwaangalia wezi vizuri wasiweze kuipenyeza mahali popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *MSD* kuna mambo, mimi niseme Serikali imefanyia kazi eneo hili sana na ripoti ya kuonesha kwamba kuna tatizo kwenye haya madeni imefanyika na ripoti imekabidhiwa Serikalini na kuna *documents* ambazo ziko sasa TAKUKURU.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme kwanza nishukuru Wizara ya Fedha. Mimi ni muda mfupi nimekaa,

lakini nimeona mambo ambayo Wizara ya Fedha wakati wote wamekuwa wakiuliza baadhi ya Wizara yako *genuine* na ni mazuri kwa upande wa Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Waziri wangu, dada yangu ambaye amenipa ushirikiano mkubwa, amenifundisha mambo mengi kwa muda mfupi, sisi tutakwenda kukupa ushirikiano kuhakikisha matumizi ya fedha ya Serikali kwenye eneo la dawa na Wizara ya Afya yanakwenda kuwa ya uadilifu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi ninapendekeza kwenye eneo hili ukiangalia *percent* ya deni lenyewe na ukiangalia kwa mwaka huo ambao tunasema deni hilo limetengenezwa, ukiangalia *percent* ya upatikanaji wa dawa kwenye vituo vyetu haviendani hata na mkopo ambao unasemekana umetokana na dawa hizo ambazo zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali inakwenda kufuatilia tatizo liko wapi ili tunapozungumzia bima, leo ukiangalia kwenye hospitali zetu wengi wanasema hospitali nyingi za Serikali hazipati gawio kubwa kutoka bima, pesa nyingi zinakwenda *private.* Mojawapo ya vitu *MSD* isipokuwa vizuri maana yake dawa hazitakuwa kwenye hospitali zetu na fedha nyingi za bima zitaelekea kwenye sehemu *private. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, twendeni tukaboreshe bima tukalete huo mkakati ambao unafanyiwa kazi sasa hivi ili kuwepo na uadilifu na ndiyo maana Rais ameanya mabadiliko *CEO* wa *MSD* sasa hivi ni mpya, maana yake hatua zimeanza kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bima wanasirikiana na bima kuona jinsi ambavyo kazi itafanyika kwa umoja ili tutakapokwenda kwenye *comprehensive health insurance* maana yake Watanzania wote watakapokuwa na Bima ya afya itaenda kwamba dawa zikipatikana *MSD* hata tutaweza kuweka pesa *MSD* kwa mara moja na zikaonekana kwenye mzunguko na kupunguzia Serikali mzigo wa kila siku kupeleka pesa kwa ajili ya kununua dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme Serikali imefanya kazi kubwa kutoka shilingi bilioni 31 kwa dawa mpaka sasa hivi kuna shilingi bilioni 269; ni hatua kubwa sana. Hizi fedha ni nyingi sana na kama asilimia kubwa zinakwenda *MSD* ni lazima kuhakikisha uadilifu unakuwepo kwa hali ya juu ili fedha nyingi zinavyokwenda ziende kutumika kwa walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali ambalo Wabunge wote tujiulize; unaweza ukaenda *MSD* ukakosa dawa ambayo ukienda kwenye *pharmacy* ya kawaida kabisa unakuta dawa hiyo. Ni lazima tujiulize swali ni kwa bahati mbaya au ni kwa kutengenezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tujiulize hayo maswali, tukiweza kujiuliza haya maswali kama ni *catalogue* ya Mwongozo wa Serikali wa Dawa haina hizo dawa kwamba hazitakiwi kununua, lakini *MSD* inashindwa nini kuwa na mpango wake *private* na wameruhusiwa kuwa na madawa *private* wakaweka hizo dawa hizi hizi pesa ambazo zinakwenda kwa watu binafsi ambao huko pesa nyingi za Serikali zinakwenda kuibiwa ziende *MSD* na ziingie kwenye mzunguko wa *MSD* ili uwezo wa *MSD* wa kujitegemea uendelee kuongezeka. Huko ndiko Serikali inakotuelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachoweza kusema kuhusu eneo la *MSD* na Bima ya Afya ni hayo mawili lakini kikubwa kwenye Bima ya Afya shida yetu ni ujazaji wa fomu. Wenzetu kule ukiangalia kwenye *private* wanajaza fomu vizuri, ukienda kwenye vituo vyetu hawajazi fomu vizuri. Unaweza ukakuta mtu *diagnosis* ni malaria, ameonekana ana malaria lakini ukiangalia kwenye fomu dawa alizopewa ni dawa za kichocho, ni lazima bima wajiulize, je, huu ugonjwa kweli kuna kitu kilichotokea hapa? Ni lazima hiyo fomu iwe *rejected.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ukiangalia vizuri utakuta tatizo liko kwa ma-*in charge* wa hospitali, tatizo liko kwa viongozi wa vituo vyetu na ni kwa sababu sisi tunapeleka mshahara hawana shida ya mshahara, ukiangalia kwenye

*private* kwa sabbau hiyo bima ndiyo inalipa na mishahara watu wako *serious* kwenye kujaza hizo fomu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu tunakwenda kwenye *comprehensive health insurance* tunakwenda kwenye *competition* ya hizi fedha za bima, maana yake ni lazima watu wetu wawe na *discipline* ili tuweze ku-*compete* na hospitali zetu sasa zianze kupata pesa na ziweze nazo kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo mimi ndicho ninachoweza kusema na ndiyo mwelekeo wa Serikali, ninashukuru kwa muda mfupi dada yangu, mama yangu, Mheshimiwa Ummy, amenionesha vitu, nimevielewa na ndicho ambacho nimeoneshwa Wizara ya Afya inafanya. Ni *vision* kubwa na ina matumaini makubwa kwa afya ya Tanzania. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula, atafuatiwa na Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Mheshimiwa Omary Mgumba ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kunipa fursa hii kuongea ili kuweza kuchangia katika hoja inayoendelea mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa namna anavyotujalia afya na kutuwezesha kuweza kutimiza majukumu yetu na vilevile niwashukuru sana wapigakura wangu ambao kwa ridhaa yao walinipa kura zao na baadaye Mheshimiwa Rais akaniteua kumsaidia. Naomba tu niwaambie kwamba niko kwa ajili ya kuwatumikia wao na Taifa kwa ujumla na vilevile niwafahamishe tu natambua wazi kuna watu wanapitapita kule, mimi nawaambia mchezo ni dakika 90 kwa hiyo wasubiri mchezo utakapoanza ili tuweze kwenda vizuri zaidi kwa sababu wanajua wapi tumetoka, wapi tuliko na wapi tunakwenda. Kwa hiyo hiyo pitapita hainipi shida sana, nawathibitishia

kwamba mwakilishi wao niko vizuri sana; na wanasema kelele za chura hazimzui tembo kunywa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo analiendesha Taifa hili. Wachangiaji waliopita wamezungumza, wengine wamesema ni Rais wa maono na mambo mengine, ni Rais ambaye sasa amejenga jina kitaifa na kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi niseme tu nampa neno Rais wangu kutoka Yoshua 1:5 ambalo linasema kwamba; "Hapatakuwa na mtu yeyote atakayeweza kusimama mbele yake siku zote za maisha yake. Na Bwana anasema kama alivyomwongoza Musa ndivyo atakavyokuwa pamoja na yeye na vilevile Mungu anasema hatampungukia na wala hatamuacha na siku zote atakuwa naye." Na sisi wasaidizi wake tunasema tuko pamoja naye mpaka ukamilifu wa dahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nizungumzie baadhi ya hoja ambazo Wajumbe wamezitoa, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Yosepher amezungumzia habari ya umiliki wa ardhi kwamba ni kwa namna gani tunasema tunatoa hati ndani ya siku 90 halafu majengo hayo hayo ya Serikali hayana hati, umiliki wa aina gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu nimhakikishie kwamba umiliki wa ardhi au wa *property* ulionayo siyo lazima uwe na karatasi hiyo hati tunayoisema, umiliki unaweza ukawa wa kimila, unaweza ukawa wa mirathi umepewa, lakini hujakamilisha taratibu zote na ndiyo maana sasa hivi tunasema umiliki wowote unaweza ukawa wa kutwaa, unaweza ukawa wa kumilikishwa na kumilikishwa na kupewa ile hati inakuwekea usalama wa miliki yako, unakupunguzia migogoro na jirani yako. Si kwamba unapokuwa huna hati maana yake hauna ule uhalali, lakini inapunguza migogoro, lakini inaleta pia usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi niseme, tunasisitiza kuwa na hati ili kuwa na miliki salama, ili kupunguza

migogoro kati ya jirani na jirani, taasisi na wananchi, wafugaji na wakulima, hiyo ukiwa na nyaraka hizo zinakusaidia zaidi. Yeye ametoa kauli anasema majengo yote yanayomilikiwa na Serikali kwa sababu hayana hati pengine yaliporwa kwa wananchi, hapana, hakuna kitu kama hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo utoaji wa ardhi unafanyika kwa mujibu wa sheria na katika umiliki wake kuna umiliki wa kimila, kuna huo umiliki wa kawaida ambao unapewa hiyo *certificate* yako, hati yako ya kuweza kumiliki. Kwa hiyo mimi nimwambie anachokisema si sahihi, asipotoshe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwenye Taarifa ya Kamati, mimi niwapongeze Kamati pamoja na *CAG* kwa namna ambavyo ameweza kuona. Yale waliyoyatoa au aliyotoa *CAG* ni ushauri kwa Serikali, na anaposema na lile ni jicho la Serikali, maana yake ni kwamba anakumbusha tu Serikali kwamba kuna moja, mbili, tatu ambayo inatakiwa kusimamia na sisi kama Serikali tunaheshimu sana mawazo ya *CAG* kwa sababu ni *CAG* ambaye ana uwezo mkubwa, ameweza kuyaona mengi na sisi tunayafanyia kazi. Kwa hiyo, hoja za Wajumbe kwenye Kamati ya *LAAC* waliyopendekeza sisi tunazichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wamezungumzia moja la kusema kwamba Serikali Kuu inawanyima mamlaka Halmashauri kwa kuziondolea pesa na nini. Lakini tukumbuke Serikali Kuu hii hii yenyewe imetoa pesa nyingi katika miradi ya kimkakati na kila Halmashauri ambayo ilikuwa imeweka andiko lake vizuri wamepewa miradi ya kimkakati ambayo itawaingizia pia kipato ambacho kitakuwa ni kipato kinachotokana na mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika miradi mingi ambayo ipo kuna ujenzi wa masoko maeneo mengi. Dodoma wana soko na wana stendi ambayo nayo tunajua inakwenda kuingiza mapato zaidi ya kile ambacho walikuwa wanapata; lakini kuna wengine wame-*opt* kujenga machinjio kama kule Dar es Salaam - Vingunguti, kuna ambao

wanajenga viwanda kule Itumbula kule Songwe ambao wanaweka kiwanda cha chumvi. Kwa hiyo hii yote ni kuwezesha zile Halmashauri ziweze kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia hata kwenye ile miradi ya barabara ambayo ilikuwa ya kuboresha majiji, majiji kama manane yalikuwa yamepata pesa hiyo na Halmashauri yangu ikiwa moja wapo. Imependezesha miji kiasi kwamba hata unapokuwa na *parking fee* ambayo ni *own source* ya Halmashauri unadai mahali ambapo pia panafanana fanana na kimji. Kwa hiyo si kwamba tu Serikali Kuu ilisema inachukua mapato halafu wao hawajapewa uwezo na kazi inayofanywa na Serikali Kuu sasa hivi ni kubwa kuliko ambayo ilikua inafanywa na Halmashauri zetu wakati zinatumia mapato yake ya ndani moja kwa moja. Kwa hiyo mimi niseme Serikali inapoamua kufanya kitu haifanyi kwa dhamira mbaya, inafanya kwa nia nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija upande wa elimu bila malipo ambapo wote tunaona *capitation* ambavyo inatumika kule sasa hivi, na wale wamejengewa uwezo na wengine wanasema watumishi ni wezi, ni wabadhirifu na nini, lakini muone Serikali hii hii pia imetoa mafunzo kwa watumishi zaidi ya 800 kwa ajili ya kuweza kupewa weledi katika namna ya kujikinga na ushauwishi wa rushwa.

Lakini vilevile inaimarisha miundombinu katika sekta mbalimbali ikiwemo elimu, afya na nini. Haya yote ukishamjengea mazingira mazuri mtumishi hawezi tena kwenda kinyume na taratibu. Kwa hiyo tunasema Serikali hii iliona mbali sana na ndiyo maana Naibu Waziri, Wizara ya Utumishi amezungumza namna ambavyo wameweza kufanya kazi kubwa kwa maana ya Serikali kuondoa watumishi hewa na nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya kuwaondoa TAMISEMI nao watasema hapo baadaye, lakini wamewajengea uwezo sasa. Halmashauri zote 185 walikwenda Wakurugenzi, walikwenda Wakaguzi wa Ndani, walienda Maafisa Utumishi wakawa wanajengewa uwezo

namna ya kuweza kusimia. Na hii inaendelea pia kwa taratibu ambazo zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi ninataka kuwapa tu uhakika Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali hii namna inavyotenda kazi ni tofauti kabisa na namna ambavyo tumezoea. Kila Serikali inakuja na utaratibu wake katika kusimamia na katika kuendesha shughuli za Serikali. Hauwezi ukafanya kitu kile kile kila siku, lakini kila unapoboresha unaona matokeo yake jinsi yalivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa namna ambavyo sekta yangu ninayoingoza kwa maana ya ardhi sasa hivi imeshuka kule chini. Watumishi hawa walikuwa TAMISEMI sasa hivi wako Wizarani, lakini haina maana ya kwamba madaraka yamepokonywa kwa Halmashauri ambazo ndizo mamlaka za upangaji, ispokuwa kama Wizara tunaimarisha sasa ili kuweza kuwafikia watu kwa ukaribu zaidi, badala ya kwenda kwenye kanda sasa unaishia kwenye mkoa na tunashuka mpaka kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, na sasa hivi hata Wabunge wengine walikuwa wanatoa ushuhuda kwamba hii ni Serikali gani inayokuja sasa hivi kwa mtumishi anahamishwa kupelekwa sehemu fulani anaanza kuwatafuta viongozi wa pale kuwaambia jamani kwa masuala ya ardhi mimi nipo. Haijawahi kutokea. Maana yake ni kwamba kuna *reform* kubwa imefanyika ndani ya Serikali katika Wizara nyingi na ndiyo maana uadilifu unakua mkubwa, kazi zinakuwa kubwa. Mashahidi wengi watatuambia; Mkoa wa Kigoma watu wamefanya, Tanga wamefanya, anafika anaripoti anasema mimi nipo sasa ndiyo Kamishna Msaidizi tutashirikiana na wanafanya kazi vizuri na mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba katika haya ambayo tunafunuliwa kuoneshwa maana yake ni kwamba tunajipanga tunaoneshwa kwamba kuna mahali fulani panahitaji kuongeza nguvu. Si kwamba pamelegalega kihivyo lakini tunatakiwa kuongeza nguvu katika suala zima

la usimamizi na ndiyo maana utaona kila anayesimama kuongea anazunguzia habari ya Taarifa ya *CAG,* anazungumzia habari ya *LAAC,* anazungumzia *PAC* kule ambapo tumeshamaliza toka juzi. Lakini haya yote sisi kama Serikali tunayachukua kulingana na ushauri wa Mkaguzi Mkuu kwa maana ya *CAG.* Lakini pia maoni na mapendekezo ya Kamati zetu tunayachukua kama Serikali kuyafanyia kazi kwa sababu mnapotushauri maana yake tunakwenda kujenga zaidi pale ambapo pengine palikuwa pamelegalega.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi niseme nishukuru sana wachangiaji wote. Hapakuwa na hoja nyingi sana ambazo pengine zingehitaji *clarification* ya kwenda *deeper,* lakini nilitaka tu niyazungumzie hayo ambayo pengine yametusaidia zaidi na nisisahu *TARURA* ambayo nayo imefanya kazi kubwa na nzuri ndani ya muda mfupi. Miji imebadilika sasa hivi, miji iko vizuri kwa hiyo Serikali inaposhauriwa inafanya. *(Makofi)*

Mlizungumzia mambo ya *TARURA,* tumefanya; mkazunguzia masuala ya maji, yamefanyika. Kwa hiyo lengo letu ni kuboresha utendaji lakini kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, Mungu akubariki na niwaombee wote, niwatakie kila la heri mtakapokwenda kusimama Oktoba nitafurahi nikiona sura zote zipo na mimi sina shaka Mwenyezi Mungu atatushika mkono, kazi tuliyoifanya inaonekana na mwenye macho haambiwi tazama, Awamu ya Tano ni awamu ambayo ni ya kazi na si awamu ya mchezo. Ahsanteni sana, Mungu awabariki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Amina, ahsante sana. Mheshimiwa Elias Kwandikwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Mgumba, Mheshimiwa Selemani Jafo ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze na mimi kuchangia

kwenye hoja hii muhimu iliyowasilishwa na Kamati ya Bunge ya *LAAC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini niseme tu kwamba kupokea taarifa hizi mbili tulizozipokea za Kamati wakati *CAG* amewasilisha ripoti zake kwa maelekezo ya Rais kwamba zifanyiwe kazi na Bunge lako mimi nimpongeze na kumshukuru Rais, ana-*demonstrate* namna nzuri alivyokuwa na uwajibikaji wa hali ya juu. Leo hii tumepokea hizi ripoti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi na wapiga kura wa Ushetu, jimbo limetulia na saa nyingine walikuwa wanatamani iwe kesho tu waweze kuweka vitu vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipekee niwashukuru Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Shinyanga hasa hasa wa Viti Maalum namuona dada yangu Mheshimiwa Lucy Mayenga yuko hapa kwa ushirikiano walionipatia kwa sababu iko miradi mingi tuliipata kwenye Jimbo la Ushetu kupitia hawa akina mama Wabunge, Mheshimiwa Lucy Mayenga hapa na dada yangu, Mheshimiwa Azza Hillal. Kwa hiyo, kipekee nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana *CAG* kwa taarifa zake na kwa kweli ushauri wake unaonesha kwa sababu ukijaribu kuangalia mifumo inaendelea kuboreshwa kwenye Serikali lakini ukiangalia pia kwamba yako mambo ya hati safi zimeongezeka kwa hiyo mapungufu yanaendelea kupungua kadri tunavyokwenda kutokana na ushauri wa *CAG* pamoja na watumishi walioko kwenye Ofisi hii. Kwa hiyo, tunamshukuru sana na naamini sisi kama Serikali tutaendelea kuzingatia ushauri na mapendekezo ya *CAG,* lakini tutaendelea pia kutekeleza maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Kamati kwa kuja na ripoti nzuri sana. Kulikuwa kuna maoni nane na unayaona ni maoni ambayo pia yanatekelezeka. Lakini wao wenyewe

kwenye ukurasa wa 23 wamesema, ninukuu, kwamba; "...Mapendekezo haya yanakusudia kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa na kuleta maendeleo kwa wananchi."

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni ukweli kwa hiyo uone kabisa Kamati zinafanya kazi nzuri na mimi niunge mkono maoni ya Kamati, kazi nzuri inayofanyika na sisi kama Serikali tutaendelea kutekeleza maoni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti ni muhimu sana, nilikuwa nimesoma ripoti hizi kwa wingi sana, hasa kwenye hizi Ripoti za Serikali za Mitaa kwenye Halmashauri zetu, lakini sambamba na hilo nimesoma pia ripoti za ufanisi na nilipenda nitumie nafasi hii niwashauri Waheshimiwa Wabunge kwamba tunavyozisoma hizi ripoti ambazo ziko kwenye matumizi ya fedha kwa maana ya *compliance,* ni vizuri pia sambamba tuzione ripoti nyingi ambazo sasa *CAG* anaziwasilisha za ufanisi. Kwa sababu ukizisoma ripoti zile zinaongeza umahiri wa ripoti kwa maana hiyo kwamba anafanya *study.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano nitaje ripoti tatu hapa ambazo zimewasilishwa na *CAG;* iko ripoti moja ni ya Ukaguzi wa Ufanisi kwenye Ubora wa Shughuli za Ujenzi na Ukarabati wa Barabara za Lami Mijini. Hizi ni barabara ambazo zinasimamiwa na wenzetu wa *TARURA,* lakini ukisoma ripoti hii ya ufanisi, ushauri uliopo na nimuahidi *CAG* kwa sababu yako mambo ambayo pia, yana-*cut across* yanaweza kutekelezwa pia na Mfuko wa Barabara kwamba tumeupokea na kuona kwamba yanalenga kwenda kuleta ufanisi kwenye miradi yetu ili ilete na iwe na ubora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini iko ripoti nyingine ambayo pia inagusa kwenye Serikali za Mitaa, lakini iko kwenye ufanisi ni Ukaguzi wa Ufanisi Juu ya Ukusanyaji Mapato toka Vyanzo vya Ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na iko ripoti nyingine yenye Ukaguzi wa Ufanisi Katika Usimamizi na iko Ripoti nyingine yenye Ukaguzi wa Ufanisi Katika Usimamizi na Utoaji Programu wa Kuwajengea Uwezo

Walimu Kazini. Kwa hiyo, utaona namna hizi ripoti zinavyo-*flow,* lakini anavyoona kuna maeneo ya kuyafanyia *study* kwa kupitia hizi *value for money reports,* tunapata ushauri mkubwa sana katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona niliseme hili, niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwa sababu, sisi ni Madiwani ni vizuri tukazisoma hizi ripoti pia za ufanisi, ili ushiriki wetu kwenye Mabaraza ya Madiwani uwe mahiri. Nasema hivyo kwa sababu naamini pia Waheshimiwa Wabunge wengi tutarudi, *Inshallah,* ili uzoefu huu tulioupata kwenye kuchambua ripoti, lakini pia tuweze kufanya vizuri zaidi siku za usoni, niliona niseme hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba katika maeneo mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia, lakini mimi pia nilikuwa najaribu kuangalia kwenye maeneo mengine kwa sababu, Wabunge wamekuja na *challenge* nyingi, lakini na sisi pia tunahusika kwenye mabaraza yetu. Kwa hiyo, ndio maana naona kwamba, yako maeneo mengine kama tunayagusa tunayaangalia na sisi tuweze kusaidia kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma ripoti hizi nimeona, kwa mfano niseme maeneo matatu ambayo nilikuwa nayaona; ziko mamlaka 126 kwenye Ripoti ya *CAG* zimetajwa hapa kwamba, kuna makusanyo, kuna mapungufu ya kutokana na makusanyo kwenye mamlaka zetu. Sasa ukitaja mamlaka 126 haiyumkini hata sisi tuliochangia hapa tunazo Halmashauri zetu ambazo sisi wenyewe tunashiriki, labda hatukuyaona kule kwenye Mabaraza, sasa kama ripoti tutakwendanazo kwa undani zaidi itatusaidia Waheshimiwa Wabunge tushiriki kuboresha mabaraza yetu na usimamizi wa rasilimali kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaona kwamba, kwa ripoti hii iliyowasilishwa na kamati, lakini na sisi Wabunge tumo humo ndani kwa sababu, tunao wajibu wa kusaidiana na wenzetu na sisi ndio ma-*senior councelor* kwenye

Mabaraza yetu. Kwa hiyo, tushiriki vizuri tukisoma ripoti hizi, lakini kule tuone, kama nimeiona Halmashauri ya Ushetu ina mapungufu na mimi ninao wajibu kule wa kusaidia kuona kwamba mambo yanaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona pia hata kwenye malalamiko mengi *ofcourse* na michango mingi ya Wabunge mizuri sana wamezungumza juu ya upelekaji wa fedha, lakini mimi naona pia kwamba yako maeneo mengine kwenye matumizi ya fedha. Matumizi hayaendi kisawasawa na Wizara ya Fedha nayo haiwezi kuwa inapeleka fedha tu lazima pia, iangalie kwamba misingi ya kupeleka fedha imezingatiwa. Kwa hiyo, nimeona hapa, iko kwenye ripoti nimeona kwamba, hata waliopelekewa fedha shilingi bilioni 258 ziko Halmashauri za mamlaka 182 hazikutumia fedha zilizopelekewa shilingi bilioni 258.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama kuna *under utilisation* lazima tuone ni kwa nini, saa nyingine inatokana na watu kutokutekeleza kanuni za fedha, hawawezi kuendelea kupewa fedha. Kwa hiyo, nilitaka niseme kwamba, wakati tukizungumza Waheshimiwa Wabunge pia, tuangalie kwa upande wa pili ni nini kimesababisha *flow* ya fedha isiende ili tuweze kuboresha na kuboresha mabaraza yetu katika usimamizi wa rasilimali hizi muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimeona kuna eneo lingine, yako maeneo mengi kwa mfano, mapato na vyanzo vya ndani shilingi bilioni 17 hazikwenda kwenye miradi ya maendeleo katika Halmashauri zetu. Sasa ukiangalia hapa mamlaka 60 hazikufanya hivyo kwa hiyo, inawezekana tumechangia hapa na sisi wenyewe tuko kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niyaseme tu hayo kwa ufupi kabisa kwamba, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuendelee kushirikiana na Madiwani katika maeneo yetu, lakini tushirikiane na Serikali katika kusimamia rasilimali, kwa sababu Rais wetu anapenda rasilimali tuzisimami ziende kwa walengwa. Sasa tunao wajibu wa

kutembea kwa pamoja, nchi ni yetu, lazima tuhakikishe matumizi yanakuwa mazuri na yanatoa manufaa makubwa kwa Wananchi wetu wa Tanzania na kama waliowasilisha taarifa walivyosema, Mwenyekiti namuona hapo, amesema, kama nilivyo-*quote* hapa kwamba iwe manufaa kwa ajili ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kuwapongeza na kuwashukuru Madiwani wa Halmashauri ya Ushetu. Ninajua na mimi nilikuwa nashiriki na nimeendelea kushiriki vizuri sana na Madiwani hawa ili kuona kwamba tunaweka tija katika usimamizi wa rasilimali. Mnaona hata *flow* ya hati kwenye Halmashauri ya Ushetu inakwenda vizuri na wananchi imewahamasisha kuchangia maendeleo yao kwa sababu wanaiona Serikali yao inafanya mambo kwa hiyo na wananchi wamezidi kujitolea katika miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko miradi ambayo wananchi wamejitolea. Ni fedha nyingi sana tukiweza kuzitengenezea hesabu kwa sababu wananchi wameiona Serikali yao inawajibika kwa wananchi, imeleta hamasa kubwa, iko michango mikubwa kwa hiyo, kipekee kwa wananchi wa Ushetu nawashukuru sana, tutaendelea kushirikiana, maendeleo ni ya kwetu sisi wote na mimi najivuna kuwa na wananchi wa Ushetu ambao wananipenda, wananchi ambao wananipa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mashaka, ila niwaombe tu wananchi wa Ushetu wapunguze jazba kwa sababu, leo hii mtu akipita kule wanakuwa wakali sana. Wasiwe wakali sana, tunao urataibu wa kwetu kule, ukali wao wakauoneshe kwenye kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana, naunga mkono Maazimio ya Kamati. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Kweli, naona joto la uchaguzi limesogea kwa kasi sana humu ndani.

Mheshimiwa Omary Mgumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Selamani Jafo, Mheshimiwa Vedasto, Mwenyekiti ambaye ndiye mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hoja hii iliyoko mbele yetu. Nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha uzima na tumefika siku hii ya leo na mimi nipate nafasi ya kutoa mchango kwenye hoja hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya *LAAC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kwanza kuwashukuru na kuwapongeza sana Kamati ya *LAAC* kwa taarifa nzuri, lakini pia nimpongeze sana *CAG* kwa kuibua na kutuonesha hoja mbalimbali na yeye ndio kama jicho la Watanzania kupitia Bunge lako tukufu, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuna hoja kama tatu zimejitokeza, hususan kwenye miradi yetu ya umwagiliaji inayotekelezwa kule katika Halmashauri zetu mbalimbali hapa nchini na hoja kimsingi zilikuwa kama tatu; hoja ya kwanza ni gharama kubwa ya miradi ya umwagiliaji, hoja ya pili ni miradi haisimamiwi vizuri na hoja ya tatu ni barabara mbovu kwenda kwenye miradi yetu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri hoja zote hizi zina ukweli ndani yake. Kuhusu gharama kubwa ya umwagiliaji; kwanza ni kweli miradi ya umwagiliaji kimsingi uasili wake ni miradi ambayo ina gharama kubwa sana. Na gharama hizi zinasababishwa na uasili wake kwa sababu, ni miradi ambayo inahusisha masuala ya ujenzi ambapo gharama zake ni kubwa sana kwenye vifaa hivyo vya ujenzi, lakini pia tukiri kuna sehemu kuna mapungufu ambayo kama alivyosema pale Profesa pale mwanzoni kwamba unakwenda kumpa yaani Mhandisi Mshauri na unamwambia kwamba, utamlipa kwa *10%.* Sasa kuna miradi mingine kwamba, inapandishwa gharama kwa ajili ya kinyume na utaratibu kwamba kwa mazingira tu ya kifisadi na rushwa

mbalimbali. Katika hilo Serikali tumeliona na tumezingatua katika mikakati yetu, baadhi ya miradi tunakwenda kuijenga kwa kutumia *Force Account* na imeleta manufaa makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika kukabiliana na hilo Serikali iliweza kuhamisha Tume ya Umwagiliaji na kuuboresha muundo wake kusimamia miradi kutoka ngazi ya Taifa kwenda ngazi ya Halmashauri kule ambayo tumelepeleka wakandarasi mpaka kwenye ngazi ya Halmashauri na imeleta ufanisi mkubwa sana. Katika kipindi cha miaka minne ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, pamoja na miradi hii kutumia gharama kubwa, lakini tumeweza kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 461,326 za mwaka 2015/2016 mpaka kufikia hekta 694,715 ambapo hekta zilizoongezeka zaidi ya 233,389 kwa gharama ya shilingi bilioni 96 tu ambayo sio kitu cha kawaida miradi hii kutekelezwa kwa huko nyuma ilivyokuwa; na niliambie Bunge lako mpaka sasa kuna miradi 56 iko tayari ambayo inasubiri kuzinduliwa nchi nzima mpaka sasa kati ya miradi 179 ambayo tumeianzisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hoja ya pili kwamba miradi haisimamiwi vizuri; ni kweli kulikuwa na mapungufu huko nyuma kwamba miradi hii ilikuwa kwamba Tume ya Umwagiliaji ilikuwa kwenye ngazi tu ya kanda, kwa hiyo, miradi hii ilikuwa inapelekwa pesa katika ngazi kule za Halmashauri na ambapo kulikuwa na kutokusikilizana kwenye ndani ya Serikali, wale Wahandisi wa Tume na Wahandisi wa Umwagiliaji na ndani ya Serikali tumeona upungufu huo kwa sababu, kama mradi unatekelezwa na taasisi mbili uwajibikaji wake unakuwa ni hafifu sana, ukienda na mapungufu hujui nani ambaye anawajibika na kurekebisha kasoro hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndio maana sasa katika ule muundo wetu tumeuboresha ili Tume ya Umwagiliaji wako mpaka ngazi ya Halmashauri, ili kwenda kuisimamia kwa karibu sana miradi yote hiyo, lakini pia tumeweka ngazi ya mkoa, pia ngazi ya kanda na ngazi ya Taifa. Hawa wote wakishirikiana na wenzetu Wahandisi wa Umwagiliaji ngazi

ya Halmashauri ili wafanye kwa pamoja na kuwa na usimamizi wa karibu sana badala ya kusimamia kutoka ngazi ya kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo bado majadiliano yanaendelea ndani ya Serikali, ikiwezekana Wahandisi wa Umwagiliaji waliokuwa chini ya Halmashauri basi waweze kuhamishwa wawe pamoja katika Tume ya Uwamgiliaji ili wote wawajibike kwenye taasisi moja. Kwa sababu kwa mujibu wa sheria sasa miradi yote ya umwagiliaji nchini inasimamiwa na Tume yetu ya Umwagiliaji ya Taifa ili miradi yote hii ya umwagiliaji isimamiwe na chombo kimoja na ilete tija na ufanisi uliokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu ni kuhusu barabara zetu zinazokwenda katika miradi ya umwagiliaji; ni kweli, barabara hizo ni mbovu na ndio zinaenda sehemu za uzalishaji, lakini kama Serikali cha kwanza kwenda kuimarisha hizi barabara iliunda Wakala wa Barabara Vijijini *(TARURA),* kimsingi ambao ndio wenye wajibu wa kusimamia barabara zote za vijijini, hasa zile zinazokwenda mashambani. Sisi kama Tume ya Umwagiliaji barabara ambazo tunawajibika ni zile ambazo za kwenye mashamba, ndani ya mashamba kule kwa wakulima. Hizo kwa sasa hivi yote hiyo miradi ambayo ndani ya mshamba tunahakikisha kwamba gharama zake zinajumuishwa kwenye gharama za mradi mzima, ili mradi unapotengenezwa pamoja na gharama za barabara ziwepo kwenye mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ushahidi kwamba upo, kwenye miradi sasahivi tunayoitekeleza kuna ile miradi ya *ERPP,* ya *PHRD* na *SSADP* yote hiyo miradi wanaona barabara kule za kwenda mashambani zote zinatengenezwa. Lengo ni kwamba huyu mkulima akilima mazao yake, basi kuwe na uhakika wa kuyafikisha masokoni kwa kwa wakati wote, ili barabara ziweze kupitika muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nichukue nafasi hii kutaka kuwashukuru sana Wananchi wangu na Wananchi wenzangu wa Morogoro Kusini Mashariki, hususan wana-CCM na wananchi kwa ujumla kwa

kuendelea kuniamini na kunituma hapa. Mimi niko tayari bado nina nguvu ya kuendelea kuwatumikia na hao wote wanaopitapita, tuna msemo wetu sisi Waluguru kule, *chonekee gagu,* lakini msimamo ni pale pale, muda ukifika Mgumba anatosha kwa siasa za maendeleo. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya Waheshimiwa Wabunge, mimi nasikiliza tu hapa; nasikiliza tu nikisema amen kwa maombi yenu.

Mheshimiwa Selamani Said Jafo, tutamalizia na Mtoa Hoja, Mheshimiwa Vedasto Ngombale.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza awali ya yote napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha tumeendelea kudumu humu katika Bunge letu mpaka siku ya leo, lakini binafsi naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya ya kutuongoza Watanzania, lakini kwa muktadha wa ajenda hii ya leo naomba nimshukuru sana na nimpongeze Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* na timu yake kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya, lakini ndani ya Bunge hili naomba nimpongeze sana Ndugu yangu Mheshimiwa Vedasto Kingunge Ngombale Mwiru na Kamati yake yote. Hakika naomba nitoe wazo jambo moja, kama ikiwapendeza sana kipindi tunachokuja kamati hii tuiangalie vizuri sana. Kwanza kuendelea kuipa weledi na maarifa mazuri ya kufanya kazi, hili kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu kwa kipindi hiki chote ambacho mimi nimeweza kufanya kazi na Kamati hii kwa kweli, Kamati hii kwa kiwango kikubwa imekuwa kama ni walimu wa kufundisha katika Halmashauri zetu na mimi najua wazi yasingeweza kufanyika hayo kama wasingepata *training* ya kutosha, kila mtu ametoka katika *field* mbalimbali, leo hii lakini ukiwaangalia Wajumbe wote kuanzia Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe

*combination* imekaa vizuri, kwa kweli mimi nina kila sababu kujivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wangu mimi haya yote yaliyozungumzwa ni ushauri na maelekezo kwa Wizara yangu iende ikafanye vizuri basi, ninatafsiri hivyo, lakini ukiangalia *trend* kwa mfano ripoti iliyotoka juzi tu ambayo leo hii imewasilishwa hapa Bungeni inathibitisha hayo. Tulipotoka huko nyuma hati chafu, hati zenye mashaka, unaona *trend* ilivyokuwa ikipanda kwena katika suala zima la ubora. Ripoti ya mwaka huu hatuna hati chafu hata moja, hati safi zimepanda mpaka asilimia 95 kwa mara ya kwanza katika historia, haijawahi kutokea, lakini zenye mashaka tumebakisha 5% peke yake, *disclaimer* na hizi nyingine zote hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba, *CAG* amefanya kazi yake, Kamati ya Bunge imefanya kazi yake ya kusimamia Halmashauri na Halmashauri japo mapungufu yako hapa na pale, lakini zimeendelea kufanya maboresho ndio maana leo hii tunajivunia katika Ripoti ya Kitabu cha Hezabu za Serikali za Mitaa hakuna hati chafu. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Kamati nikupongeze sana kwa hii kazi kubwa na Kamati yako. Naomba nikuhakikishie ni kwamba Serikali kwa jukumu letu tutaendelea kutekeleza yale maoni na maelekezo yote, lengo letu kubwa ni kwamba, twende tukafanye vizuri zaidi, *value for money,* rasilimali za nchi ziendelee kusimamiwa. Kwa hiyo, mimi niseme *Inshallah,* Mungu awabariki wote turudi salama katika kipindi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja mbalimbali zilijitokeza ambayo ni hoja hii ukiangalia suala zima changamoto ya watumishi ni kweli na hasa katika sekta ya elimu na sekta ya afya na ndio maana ukiangalia katika kipindi hiki Mheshimiwa Rais kwa sababu zimeibuliwa hoja hizi na kutolewa maelekezo mbalimbali na kipindi hiki mnaona kwamba, katika sekta ya elimu peke yake zaidi ya

watumishi 19,000 wameajiriwa na sekta ya afya juzijuzi tumemaliza tu watumishi 610 kati ya watumishi 1,000 Mheshimiwa Rais aliotoa, zaidi ya watumishi 9,014 wameenda katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika sekta ya afya na sekta ya elimu ni zaidi ya watumishi 19,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini maana yake; ni kwamba kweli changamoto bado ipo kubwa, lakini Serikali kwa agenda ile ile ya kwenda kutekeleza maelekezo mbalimbali ya Kamati ya Bunge, lakini hali kadhalika yaliyoibuliwa na *CAG,* Serikali inaendelea kuyafanyia kazi hayo, lakini ukiachia hayo ni suala zima la watu katika suala zima la kukaimu, kukaimu, kukaimu. Historia tulipokuwa tunazungumza mwaka 2016 tofauti na historia leo hii, kamati hii wakati ule *CAG* akipitia katika kuangalia Maafisa Elimu kila maeneo watu wanakaimu hakuna Maafisa Elimu, lakini leo hii ukijakuangalia tumeajiri, tumepeleka, tumeteuwa Maafisa Elimu katika Halmashauri zote, lakini kada mbalimbali watu waliokuwa wanakaimu wanakaimu kada hiyo. Niishukuru sana Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya kaka yangu *Comrade* Mheshimiwa Mkuchika, mzee wetu, wamefanya kazi kubwa. Karibu idadi kubwa ya watu waliokuwa wanakaimu sasa hivi wengi sana wamethibitishwa. Hii ni *trend* nzuri tunaenda kufanya kazi vizuri, lakini Kamati hii na Kamati ya TAMISEMI ilikuja na ajenda ya kwamba, watu mikopo ya asilimia ile 10 kwa mgawanyiko wake ilikuwa haiendi vizuri

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaofuata historia ya ripoti ya *CAG* ya 2013/2014 zaidi ya shilingi bilioni 37 zilitakiwa ziondoke katika makundi haya hazikuweza kwenda, leo hii nikizungumza katika kipindi hiki zaidi ya shilingi bilioni 93.01 mpaka mwezi Februari zilienda, lakini uwepo wa sheria inayoenda kusimamia jambo hili na hata hivyo tumeamua kuwaelekeza Wakurugenzi na hili nimemwambia Mheshimiwa Rais kabisa wazi, wale Wakurugenzi ambao itakapofika mwezi wa sita hawajapeleka zile 10% kwa mgawanyiko wa 4%, 4%, 2%, Wakurugenzi hao maana yake watakuwa wamevunja sheria ambayo imetungwa na Bunge lako tukufu, lakini *CAG* ameshaainisha jambo hilo na Kamati ya Bunge imesimamia,

*with good recommendations* tutapeleka kwamba, watu hawa hawastahiki tena, hawana *qualifications* kuwa Wakurugenzi wa Halmashauri na jambo hili tumeshawaeleza wazi, halina jambo la kificho. Maana yake ni kwamba tunaendelea kutekeleza maelekezo ya Kamati na hoja iliyoibuliwa na *CAG. (Makofi)*

Kwa hiyo, niseme kwamba tunajivunia na hata mnapoona miezi michache iliyopita mpaka leo hii *trend* kila Mkurugenzi anahangaika katika kupeleka zile asilimia 10 katika makundi mbalimbali, lakini hata hivyo tutaendelea kusimamia, kuimarisha usimamizi wa fedha hizo lazima ziende zikatekeleze vizuri matakwa ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala zima la ukusanyaji wa mapato katika mamlaka ya Serikali za Mitaa, ni kweli hali yetu ilikuwa mbaya na *CAG* ameendelea kuliibua jambo hili miaka yote. Ukusanyaji wa mapato na matumizi ya mapato hayo, hali yetu huko kutoka mwanzo ilikuwa ni mbaya sana, *trend* yetu tulikuwa hatufiki hata asilimia 80. Katika mwaka wa fedha uliopita tulifika takriban asilimia 81, tukaenda katika mwaka huu ulioisha tumefika asilimia 90 na ina maana kwamba kipindi hiki tunatarajia kwamba tuna imani ukusanyaji wa mapato utazidi kuimarika lakini changamoto kubwa ni kweli *POS machine* sehemu zingine hazikuwepo, hali kadhalika usimamizi wa hizo mashine umekuwa ni changamoto kubwa, Kamati imesema, *CAG* ameripoti na ndiyo maana katika ajenda moja ya upungufu wa hizi *POS,* tuliamua kununua *POS* 7,227 tukazigawa katika Halmashauri mbalimbali kuzijengea uwezo. Sasahivi jukumu letu kubwa ni kwenda kuweka/kusimika vizuri matumizi mazuri kwa ajili ya wale watu ambao wanafanya uharibifu wa zile *POS* zisiweze kukusanya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Kamati ya Bunge, naomba niwahakikishie kwamba jambo hili tunaenda kulisimamia kwa nguvu zote na hivi sasa naomba niwaambie tumewaagiza Wakuu wa Mikoa wote wahakikishe kwamba wale *defaulters* wote wa *POS* tunaainisha na watu zile fedha wanaendelea kulipa na mpaka juzi, Mkuu wa Mkoa wa

Morogoro ameniletea takwimu za jinsi gani mapato mbalimbali yaliyokuwa yamefisadiwa yamerudishwa katika Mamlaka ya Serikali ya Mitaa kwa lengo la kuhakikisha kwamba ziweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na ajenda hapa kubwa sana kuliko zote, mambo yako mengi lakini suala zima la posho ya Madiwani. Naomba niwaambie ni kweli mwezi mmoja uliopita wakati tunaanza mchakato wa bajeti, zaidi ya shilingi bilioni 17 ilikuwa inadaiwa karibu na *point* 8 maana yake yale madeni mengine yaliyokuwa benki na nanihii mbalimbali. Tumeweza kutoa maelekezo katika Halmashauri zote na kuzipa *deadline.*

Naomba niwaambie mpaka takwimu ya hapa juzi juzi hapa, zaidi ya shilingi bilioni 10 tayari zimeshalipwa katika maeneo mbalimbali na ndiyo hivyo ndiyo maana sasa hivi Halmashauri mfano kama Halmashauri 57 hazidaiwi kabisa deni lolote kutoka katika benki yoyote lakini Halmashauri takribani 112 hizi hawana madeni yoyote *either* ya posho ya Madiwani ama ile posho ya mwezi au posho ya vikao. Lakini hata hivyo, tumeendelea sasa kuhakikisha tunasimamia Halmashauri zote kuzielekeza, yale madeni ya Madiwani yote yaweze kulipwa lakini naomba niwaambie kuna madeni mengine yako nje ya zile posho za Madiwani yaani ina maana kwamba japokuwa Diwani ameomba, hata kama Halmashauri ikilipa madeni, bado yule Diwani anaendelea kudaiwa. Sitaki kuzitaja hizo Halmashauri.

Kuna Halmashauri nyingine unaona yaani iko nje hata Halmashauri ikilipa yote zaidi ya shilingi milioni 100 ina maana hiyo ni Madiwani wamekopa nje kabisa ya utaratibu huo. Ina maana katika hizi sasa ina maana *reliability* itaondoka kwa mtu ambaye ni mkopaji, lakini katika lile jambo ambalo linahusu Halmashauri yenyewe ambayo inapaswa ilipe posho hiyo, naomba niwaambie kwamba hili tumetoa maelekezo na hivi sasa timu yangu inahangaika jinsi gani kufanya posho hizo zote ziweze kulipwa, kama mtu atadaiwa, adaiwe lile deni lake tu ambalo yeye mwenyewe alili-*commit* zaidi ambalo ameshindwa kulilipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba niwaambie Halmashauri zingine lakini naomba niwaambie haziwezi kujiendesha. Kuna Halmashauri nyingine mpaka huu mwaka unaisha, pato lake kwa mwaka hata shilingi milioni 500 haijafika, Madiwani *allowance* zao na kila kitu zaidi ya shilingi milioni 940, Halmashauri hiyo maana yake *qualification* yake tulipaswa tuifute, tuelezane ukweli, yaani ina maana hata asipolipa asilimia tano au 10 yaani chochote ile posho ya Madiwani peke yake hawawezi kulipa kwa makusanyo yao yote ya mwaka mzima. Hili naomba niwaambie ndiyo maana hivi sasa hata *request* ya kuanzisha Halmashauri mpya tunaziangalia kutokana na uwezo wao kwa ajili ya kuepusha migogoro kama hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua muda umeisha lakini naomba niseme, sisi kama Serikali tumechukua maelekezo ya Kamati ya *LAAC,* tutaendelea kuyafanyia kazi. Ni jukumu la TAMISEMI, sisi ndiyo kioo kinatuonesha yale mapungufu kwa lengo la kuboresho na kwa maslahi mapana ya Watanzania. Mungu atubariki sote, aibariki Kamati hii, aibariki ofisi ya *CAG,* lakini ambariki sana Dkt. John Pombe Magufuli na Wabunge wote, Mungu awafunulie, mambo yenu yaende safi, tukashinde salama, tukutane tena. Ahsanteni sana na naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maombi hayo, nimeambiwa Mheshimiwa Jafo amefunga sita, kwa hiyo, yatakuwa yamepokelewa moja kwa moja. *(Kicheko)*

Tumalizie sasa na Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ahitimishe hoja ya Kamati.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, naomba kukushuru sana kwa kuiwezesha Kamati yetu

kuwasilisha taarifa yake Bungeni na kujadiliwa ipasavyo, niwashukuru pia Waheshimiwa Wabunge.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Ndugai kwa maamuzi yake ya kujadili Taarifa ya *CAG* baada ya kuwa imekamilika. Kama unavyofahamu, mwanzoni ilikuwa kwamba Taarifa yetu ya mwaka tunaifanya katika lile Bunge la Januari halafu mjadala wa Taarifa ya *CAG* tutakuja kuufanya mwezi wa nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa katikati Serikali inaendelea ku-*take action* wakati Bunge lako tukufu halijafanyia *verification* Taarifa ya *CAG.* Kwa hiyo, kwa maamuzi haya maana yake sasa tuko sawasawa kwamba hata Serikali iki-*take action* kwamba Bunge lako tukufu limeshapitia Taarifa ya *CAG,* nimpongeze sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ninampongeza kwa jambo moja ambalo sasa ameiweka hii nchi kuwa shwari. Jambo la kuwaondolea hofu Watanzania katika ugonjwa huu wa *Covid–19* kwa sababu Watanzania sio tu walikuwa wanaumwa Corona, lakini pia walikuwa wana hofu na kutokana na hofu hiyo Watanzania sasa wamekuwa na imani kwa wataalam wao, zaidi kumuomba Mungu na wamekuwa na imani kwa waganga wa jadi na taratibu zetu za nyungu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuwapongeza watendaji wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI chini ya usimamizi wa ndugu yangu Jafo, nikupongeze sana umetoa ushirikiano mzuri katika kipindi chote cha miaka mitano wakati Kamati yetu inafanya majukumu yake. Nichukue nafasi hii kupongeza Wizara ya Fedha, nichukue pia nafasi hii kupongeza Ofisi ya *CAG,* ndugu yangu Kichere nakupongeza sana kwa kipindi kifupi ambacho tumefanya kazi umetoa

ushirikiano kwa Kamati na Kamati imejisikia sasa iko katika hali nzuri ya kufanya kazi yake.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia Wajumbe wa Kamati ya *LAAC* na Msaidizi wangu Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota. Kwa kweli wamenipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu. Ni majukumu mazito lakini nawashukuru sana katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, niwapongeze wapiga kura wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, niwapongeze sana, wamenipa imani, wameniami na ninayo imani kwamba wataniamini tena na sisi Wamatumbi wa kule ilipoanza Vita ya Majimaji tunao msemo wetu kwamba *"ulongolongwana"* kwa hiyo wao wenyewe huko wanajua. Hao wanaojipitisha pitisha hao waaambiwe mwenyewe nakuja! Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee pia niipongeze familia yangu kwa namna ambavyo imenisaidia katika kutekeleza majukumu haya, majukumu mazito, lakini tumekuwa pamoja katika kutekeleza majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya, sasa Taarifa ya Kamati ilikuwa na jumla ya hoja nane na wachangiaji 41 wamechangia katika maeneo tofauti. Mapendekezo yao yamefanana kabisa na hoja ambazo Kamati yangu iliweka mbele ya Bunge lako. Naomba kutambua kwa majina yao kama ifuatavyo; Mheshimiwa George Malima Lubeleje *(Senator),* Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Dkt. Christopher Chiza, Mheshimiwa Conchester Rwamlaza, Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Franz Mwalongo, Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Tunza Malapo, Mheshimiwa Ahmed Salum, Mheshimiwa Alex Gashaza, Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Rhoda Kunchela, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Anastazia Wambura,

Mheshimiwa Martin Mtonda Msuha, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Aisharose Matembe, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mheshimiwa Pascal Haonga, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Yosepher Komba, Mheshimiwa *Engineer* Edwin Ngonyani, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mheshimiwa Japhary Michael, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mheshimiwa Profesa Jumanne Kishimba, Mheshimiwa Ikupa Alex, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Mheshimiwa Omary Mgumba na Mheshimiwa Selemani Jafo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya Kamati yalihusu Serikali kutekeleza masuala nane yafuatayo; moja, kupeleka kikamilifu fedha za ruzuku ya miradi ya maendeleo katika Halmashauri kwa kuzingatia sheria ya matumizi iliyotungwa na Bunge; mbili, kufungamanisha mifumo ya *EPICOR* na mifumo mingine ya fedha katika Halmashauri; tatu, kupunguza urasimu katika malipo ya hati za wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maendeleo; nne, kuweka utaratibu mahsusi wa kujaza fomu za matibabu kwa wagonjwa wanaotumia bima ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* utakaorahisisha marejesho za gharama za matibabu katika Halmashauri, tano, kuwasilisha kikamilifu makato ya kila mwezi ya mishahara ya watumishi katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, sita, kuimarisha usimamizi na udhibiti katika mashine za *POS,* saba, kuzingatia masharti ya Sheria ya Fedha za Umma katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na nane, kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* katika miradi iliyotekelezwa kwa fedha za wafadhili katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yote yaliungwa mkono na wahangiaji wote waliojitokeza. Nawashukuru sana, hivyo naomba Bunge lako tukufu kwa ujumla wake iunge mkono mapendekezo ya Kamati kwa ajili ya utekelezaji wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na kwa taratibu zetu nilitakiwa niwahoji lakini naangalia hapa kura zimeshapigwa kwa wingi kabisa na Wabunge walio wengi wameafiki. Kwa hiyo, naweza kusema kwamba Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa za Ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2019 imepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa za Ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2019 ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa muktadha huo, mapendekezo au maazimio nane ambayo Kamati ilikuwa imeyaleta na kama Waziri alivyosema hapa yamepokelewa na upande wa Serikali na watayafanyia kazi kwa kadri Kamati ilivyoagiza na kwa sasa kwa sababu Bunge limeshaamua kwa kadri Bunge lilivyoagiza.

Kwa namna hiyo na mimi niungane nanyi kama mlivyochangia kwa kirefu kabisa kumpongeza sana Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri anayoifanya yeye pamoja na watendaji wote walio chini yake amefanya

kazi nzuri. Taarifa ni nzuri, lakini pia Kamati imeweza kutujulisha sisi kama Wabunge kwamba walipata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali maana yake ni kwamba mambo yamebadilika kwa Taarifa hii ya Kamati maana yake utendaji wa *CAG,* lakini pia utendaji wa watumishi wale walioko kule wanafanya kazi nzuri. Hizi changamoto naamini kama alivyosema Mheshimiwa Jafo zitaendelea kufanyiwa kazi na Serikali ili mambo yote yaende sawa. Kwa hiyo tunawapongeza sana Kamati lakini pia tunawashukuru kwa kufanya kazi kwa niaba ya Bunge na hata tumeweza kusikia kwamba *CAG* anafanya kazi nzuri.

Waheshimiwa Wabunge, ni wazi na mimi niungane pamoja na ninyi tukizungumza kuhusu ukaguzi wa hesabu maana yake lazima kuwe na fedha ambazo zilikusanywa, baada ya kukusanywa zikapelekwa kwenye miradi mbalimbali ndiyo tunaweza kupata Taarifa ya *CAG,* hawezi kwenda kukagua kama fedha hazijakwenda.

Kwa hiyo, na mimi nichukue fursa hii kuipongeza sana sana Serikali kwa ujumla kwa kukusanya mapato, lakini pia kwa kupeleka hizo fedha kwenye miradi ambayo hata Bunge tumeweza kwenda kuangalia huko kupitia Kamati yetu na kuona kazi nzuri inafanyika.

Kwa hiyo, naungana nanyi kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa usimamizi mzuri kabisa wa utendaji mzima wa TAMISEMI na kwa kuwa iko chini yake, basi na yeye tuchukue fursa hii kumpongeza san asana na wasaidizi wake wote Mheshimiwa Jafo na Naibu Mawaziri wanaofanya chini yako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili; tangazo la kwanza linahusu Tamko la Rasilimali na Madeni la mwisho wa kutumikia wadhifa kwa kiongozi wa umma. Sheria yetu inatutaka kama ambavyo huwa kila mwaka tunapeleka hizi taarifa, tukianza tu Bunge huwa tunapeleka lakini pia kila mwaka tunapeleka hizi taarifa tunapokamilisha kipindi chetu cha uongozi pia tunatakiwa kutoa taarifa juu ya mali ambazo tunazo na pia madeni tuliyonayo.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ili tusikipungukie kifungu ambacho kinatutaka tufanye hivyo katika sheria zetu basi tuhakikishe tunafanya hivyo. Sasa tofauti na kile ambacho tulikuwa tukikifanya huko nyuma, safari hii mambo yamebadilika kwa hiyo yatafanywa kwa mtandao.

Waheshimiwa Wabunge, mtapokea taarifa kupitia simu zenu za mkononi ama za kiganjani ama wengine watapata taarifa hizo kupitia barua pepe namna ya kuingia kwenye mtandao wa Sekretarieti ya Maadili ili waweze kujaza hiyo fomu na waweze kuituma ili iweze kufika kwa wakati na fomu hii inatakiwa kujazwa kuanzia sasa mpaka kabla Bunge halijakwisha kwa sababu tunatakiwa wakati Bunge linakwisha tuwe tumeshajaza hizo taarifa za mali na madeni.

Sasa kwa sababu nimesema mtaletewa hiyo taarifa kwenye simu zenu za kiganjani namna ya kuingia na ukishaingia utatakiwa kubadilisha neno lako la siri ili mtu mwingine asiweze kuingia kwa sababu taarifa unazoziandika ni za siri na Sekretarieti/Tume ya Maadili inachukua hivyo kwamba hizo taarifa na siri na unashauriwa ukishamaliza kujaza ile fomu, ui-*print* ili ukae nayo kwa ajili ya kumbukumbu zako mwenyewe au wakati mwingine unaweza kuwa na mambo ambayo umejaza mle halafu baadae ukasahau kwamba una mali kama hiyo ni vizuri ukiwa na hiyo kumbukumbu itakusaidia hapo baadae. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna baadhi ya viongozi ambao watakuwa hawahusiki kujaza sasa, wao watatakiwa kujaza hapo baadae labda na wao niwaseme ambao hawatajaza hizo fomu kwa sasa ni Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Waziri Mkuu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Lakini pia Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wao hawatajaza sasa hizo fomu, watajaza wakati wao utakapofika mwisho kwa mujibu wa Katiba yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawakumbusha hilo ili mkumbuke kwanza kuna kujaza fomu lakini pia mtapata taarifa hizo kupitia kwenye simu zenu na pia kupitia kwenye barua pepe. Sasa kwa sababu hatujaelezwa kwamba hizo taaifa zitatumwa

lini, lakini baada ya tangazo hili zitaanza kutumwa na zitakapotumwa tuanze kuzifanyia kazi wakati wote tuko hapa ili kama kuna Mbunge anapata changamoto kwenye kuingia kwenye huo mfumo na kujaza, basi aweze kuwasiliana na Ofisi yetu ya Tume na hizi namba nadhani ni muhimu mkiziandika Waheshimiwa Wabunge, namba ambazo mnaweza kupiga mkipata changamoto kwenye hili zoezi zima la kujaza fomu kupitia njia ya mtandao. Namba ya simu ni 0734101040 na kwa upande wa simu ya mezani ni 0262160199.

Waheshimiwa Wabunge, kuna mtu hajapata hizo simu vizuri? Simu ya mkononi ni 0734101040 na simu ya mezani ni 0262160199. Lakini wengine wanaweza kuandika barua pepe ambayo ni *helpdesk@ethicsecretariet.go.tz.* Kwa hiyo, wengine wanaweza kutumia barua pepe, wengine wanaweza kupiga simu lakini ni pale ambapo umeshaingia umejaribu kujaza, usianze kupiga kwamba kabla hata haujajaribu maana watakapokuuliza umekutana na changamoto gani unaweza ukapata mtihani wa kuwajibu.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine mnatangaziwa kwamba Mheshimiwa Spika ameandaa mafunzo kwa ajili ya Wabunge wote ambayo ni ya mambo mbalimbali ambayo ni ya muhimu sana kwetu Waheshimiwa Wabunge katika kipindi hiki cha mwisho kwa wale ambao hawatabahatika na kwa wale ambao maombi yale wameitikia amina, watakaorejea pia yatawasaidia katika kipindi hicho.

Lakini Mheshimiwa Spika, ameandaa mafunzo mbalimbali ambayo yatafanyika kuanzia kesho tarehe 29 Mei, 2020 hadi tarehe 4 Juni, 2020. Yatafanyika kuanzia saa nane mchana mpaka saa 12 jioni, kuanzia tarehe 29 mpaka tarehe 4 Juni, 2020 na yatafanyika kuanzia saa nane mchana mpaka saa kumi na mbili jioni.

Waheshimiwa Wabunge, kumbi zitakazotumika kwa mafunzo hayo ni ukumbi wa Bunge huu ambao tupo sasa hivi, lakini pia Ukumbi wa Msekwa. Ratiba kamili naamini

mtakuwa mmeshawekewa ama kama hamjawekewa basi itawekwa mara baada ya hili tangazo kwamba lini kutakuwa na mafunzo gani. Itawekwa kwenye vishkwambi/*tablets* zenu.

Waheshimiwa Wabunge wote mnasisitizwa kuhudhuria mafunzo haya ambayo ni ya muhimu sana na yataanza siku ya kesho ambayo ni tarehe 29 Mei, 2020 mpaka tarehe 4 Juni, 2020 na yatakuwa yanaanza saa nane mchana mpaka saa 12 jioni. Kwa muktadha huo, vikao vya Bunge kwa maana ya Mkutano huu wa 19 vitarejea tarehe 5 Juni, 2020.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka saa nane kamili mchana siku ya Ijumaa, tarehe 5 Juni, 2020.

*(Saa 11:44 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Ijumaa, Tarehe 5 Juni, 2020 Saa Nane Kamili Mchana)*